**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 20 Aprili, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilisha Mezani na:-

**MHE. GIDEON A. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:-**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa Mwaka 2006.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH – (K.n.y. MHE. JUMA S. NH'UNGA) - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:-**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa Mwaka 2006.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 115

**Madaraka ya Meya wa Jiji**

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Meya wa Jiji na Diwani kama Madiwani wengine wa Kata, isipokuwa yeye huchaguliwa tena na Madiwani wenzake kuwa Meya; na kwa kuwa, yeye ndiye msemaji mkuu wa Madiwani na muongozaji wa Vikao vya Halmashauri (Mwenyekiti):-

Je, Meya na Jiji/Mji anao uwezo wa kusitisha Udiwani wa Diwani mwenzake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Meya wa Jiji na Manispaa anapata mamlaka yake ya kufanya kazi katika Sheria Na. 8 ya mwaka 1982. Mwenyekiti wa Halmashauri anapata Mamlaka ya kufanya kazi katika Sheria Na.7 ya mwaka 1982. Meya na Mwenyekiti wa Halmashauri ni Mwenyekiti wa Vikao vya Baraza la Madiwani na pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha au Kamati ya Mipango na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Madiwani wote katika Baraza la Madiwani wanatokana na Vyama vya Siasa. Chama cha Siasa kinawajibika kudhibiti Madiwani wake wenye matatizo. Baraza la Madiwani linadhibiti Madiwani waliokosa sifa za udiwani na mwenye utendaji mbovu wa kazi. Baada ya kujadili matatizo ya Diwani taarifa inatumwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Waziri atatoa ushauri na baadaye ataaamua juu ya suala lenyewe na kuiarifu Halmashauri husika. Kama Diwani atapoteza wadhifa wake wa udiwani, Waziri anapeleka taarifa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili ifanye utaratibu wa uchaguzi mdogo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Meya wa Jiji ni Msemaji Mkuu wa Madiwani na Mwongozaji wa Vikao vya Halmashauri (Mwenyekiti). Meya wa Jiji au Mji hana uwezo wa kusitisha udiwani wa Diwani mwenzake. Meya anapobaini kuwa Diwani amepoteza sifa za Udiwani, anachotakiwa ni kutoa taarifa kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Uamuzi kuhusu hatma ya Diwani anayekosa sifa za kuwa diwani utatolewa na Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa na siyo Meya wa Jiji, Manispaa, Mji au Mwenyekiti wa Halmashauri. Napenda kusisitiza kuwa Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Miji na Mameya wa Halmashauri za Manispaa na Majiji kuwa wanatakiwa kuzingatia Sheria katika kutekeleza majukumu yao.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Meya huyo tayari ameishamdhalilisha Diwani kwa kumfukuza katika vikao Diwani hahudhurii na anapohudhuria Meya anatishia kuwa yeye ataondoka katika vikao hivyo. Kwa hiyo, Diwani akishahakikishia kwamba vikao vinaendelea anatoka. Je, Mheshimiwa Waziri anatueleza nini juu ya hilo?

La pili, kwa kuwa Diwani ni mwakilishi wa wananchi katika Kata husika. Je, Wizara haioni kwamba wananchi wale wanakosa haki yao ya msingi ya uwakilishi katika Halmashauri? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ni bahati mbaya hasemi ni Meya gani, kwa hiyo kidogo linakuwa ni la ujumla. Lakini tunachoweza kusema ni kwamba endapo itatokea hali kama hiyo uko utaratibu unaomwezesha yule ambaye anaona hakuridhika kumwandikia Waziri anayesimamia eneo hilo la Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili hatua za kurekebisha kasoro hiyo ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwamba kwa kweli kama Meya atachukua hatua ya namna hiyo haoni kwamba kwa namna moja au nyingine anawanyima haki wananchi wanaowakilishwa na diwani huyo kwa kipindi hicho. Ni kweli kwa kipindi hicho ambacho atakuwa amechukua hatua hiyo watu wake watakosa mwakilishi katika Baraza la Madiwani.

Lakini huo ni utaratibu wa kawaida kama mnavyoona hata kwa Waheshimiwa Wabunge zinachukuliwa hatua za kisheria kunakuwa na kipindi ambacho huwezi kumwakilisha mpaka tatizo litakapokuwa limetatuliwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kama iko hali ya namna hiyo, basi atuletee jambo hilo tuweze kuliangalia na tulishughulikie.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Kabwe Zitto, niseme tu itakuwa rahisi kidogo leo kuruhusu maswali ya nyongeza kwa sababu maswali yako kumi tu. Mheshimiwa Kabwe Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo lilitokea katika Manispaa ya Tanga ambapo Meya alimfukuza Udiwani Mheshimiwa Diwani. Tatizo hilo hilo pia limetokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ambapo Mwenyekiti wa Halmashauri amesimamisha kwa miezi sita Diwani wa Viti Maalum Ndugu Zaituni Biongelwa kuhudhuria vikao vya Halmashauri kwa sababu ya kuhutubia mkutano wa hadhara. Je, Waziri wa TAMISEMI analieleza nini Bunge juu ya tabia ya Wenyeviti wa Halmashauri hasa wanaotokana na Chama cha Mapinduzi kuwasimamisha Madiwani wa Upinzani kuhudhuria vikao vya Halmashauri? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kesi ya Tanga na kesi ya Mbunge wa Viti Maalum upande wa kule Kigoma zote nitazieleza na nitazipa maelezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea kwa upande wa Diwani yule wa Tanga wa *CUF*. Diwani yule alishitakiwa Mahakamani, mashitaka yale yakathibitika akatiwa hatiani. Hakimu kwa busara zake hakumpa adhabu ya moja kwa moja kama ambavyo mara nyingine inatokea, akaamua kumpa kitu kinaitwa *conditional discharge* kwamba katika kipindi cha miezi sita endapo atatenda kosa lingine linalofanana na hilo, basi adhabu hiyo sasa itatimizwa kwa maana ya kwamba kama ni kifungo cha miezi sita basi angefungwa kwa kipindi cha miezi sita. Meya kwa kuamini kwamba huyo mtu ameishatiwa hatiani akachukua hatua ya kumwondoa katika Udiwani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, Meya alitakiwa tu aniletee taarifa kwamba jambo hilo liko hivi na mimi ndiyo ningechukua hatua sasa ya kuiarifu Tume ya Uchaguzi kama ningeridhika kwamba ziko sababu za kutosha.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme kwa kesi ya Tanga, hukumu yake ilikuwa kwamba kama angefanya kosa ingekuwa ni kifungo cha miezi sita. Sheria inataka ufungwe kwa zaidi ya miezi sita ili uweze kupoteza nafasi yako ya Udiwani.

Mheshimiwa Spika, nimekwishachukua hatua za kurekebisha kosa hilo, tumekwishamwandikia barua kumrejesha kwenye nafasi yake ya Udiwani na tumemwelekeza Meya kwamba inapotokea jambo kama hilo ni vizuri akafuata utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mbunge wa Viti Maalum tumeishapokea tuite rufaa au malalamiko. Wanasheria wangu wanalifanyia kazi, liko tofauti kidogo hili kwa sababu hili lilipitia kwenye Kamati ya Maadili ya Madiwani, kwenye Halmashauri inayohusika. Lakini bado tunajiridhisha, tukiridhika litachukua hatua za namna hiyo haraka sana kuweza kurekebisha hiyo kasoro.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini pamoja na majibu hayo sasa tunataka kujua ni lini Diwani huyo atarejeshwa katika nafasi yake. Kwa sababu ni muda mrefu tokea atoe hiyo taarifa, lakini bado hawataki kumrudisha na wanababaisha tu baina ya Mkurugenzi na Meya wa Jiji. Sasa tunataka kujua ni lini atarudishwa, hatutaki tuambiwe tena tuvute subira, subira tumekwishaivuta kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu pamoja na jazba za Mheshimiwa Shoka Juma. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Shoka Juma amelifuatilia jambo hili kwa karibu sana tangu lilipotokea na mimi ninampongeza kwa ujasiri wake wa kuweza kulisukuma jambo hilo kwa nguvu sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Shoka Juma tu kwamba naamini akicheki kama siyo leo au kesho kule Tanga ataambiwa Diwani huyo ameisharejeshwa tayari katika nafasi yake. *(Makofi)*

Na. 116

**Mabaraza ya Ardhi Vijijini**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali katika kuleta Utawala Bora na Maisha Bora kwa kila Mtanzania, Serikali imerekebisha Sheria nyingi ikiwemo na Sheria ya Ardhi, hususan kuanzisha Sheria ya Ardhi ya Vijiji na kuanzisha Mabaraza ya Ardhi Vijijini:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba zipo changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu ya Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji kama vile elimu kwa wajumbe wa Baraza, Vyumba vya kufanyia kazi na vitendea kazi mbalimbali?

(b) Je, Serikali inasema nini kuhusiana na sehemu (a) ya swali hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria iliyoruhusu kuanzisha Mabaraza ya Ardhi ya vijiji ni *the Courts (Land Disputes Settlements) Act* ya mwaka 2002. Majukumu ya Mabaraza hayo ya Ardhi ya Kijiji ni kupokea malalamiko ya wanavijiji yanayohusu Ardhi na kuyapatia ufumbuzi. Kulingana na Sheria hiyo, vijiji vyote vinatakiwa kuunda Mabaraza ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu fika kuwa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yanakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile elimu kwa wajumbe wa Mabaraza, ofisi za kufanyia kazi, vitendea kazi mbalimbali na posho. Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji ni mali ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji na yameundwa na Mamlaka hizo kuanzia mwaka 2004, baada ya kuelekezwa jinsi ya kuunda Mabaraza hayo. Baraza la Ardhi la Kijiji lina Wajumbe Saba (7) ambao ni wanakijiji waliochaguliwa na Halmashauri ya Kijiji na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Kati ya wajumbe 7 wa Kamati, wajumbe wanawake wanatakiwa wasipungue watatu (3).

(b) Mheshimiwa Spika, changamoto zinazokabiliwa na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji zinapaswa kushughulikiwa na Halmashauri ambazo ndizo zinaunda na kumiliki Mabaraza hayo. Napenda kuziagiza Halmashauri zote nchini kuunda Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji kama tulivyoagiza. Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji wapewe mafunzo ili waweze kumudu kazi zao ipasavyo.

Aidha, Halmashauri zitenge Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kulipia gharama mbalimbali za posho, kununua vitendea kazi, kuwapatia ofisi za kufanyia kazi na kuhakikisha Mabaraza hayo yanafanya kazi zao. Halmashauri zitoe ushirikiano wa kutosha kwa Asasi zisizo za Kiserikali ambazo zinashiriki kukabiliana na changamoto hizo. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma Mtandao wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (*DONET*) imesaidia kuanzisha na kutoa elimu kwa vijiji 16 kuhusu elimu mbalimbali ya Mabaraza ya ardhi . Asasi ya *Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)* imetoa Elimu ya Ardhi katika vijiji 18 katika Tarafa ya Mundemu.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimwa Naibu Waziri, ninalo swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa tangu Mabaraza hayo ya Ardhi yalipoundwa kwa Sheria mwaka 2002 kimsingi yalipaswa yahudumiwe na Halmashauri; na kwa kuwa Halmashauri nyingi zimeshindwa kuyahudumia Mabaraza hayo ya Ardhi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatoa maelekezo gani kwa zile Halmashauri ambazo zitashindwa kuendelea kuyahudumia Mabaraza hayo ya Ardhi kwa kuwa ni mali ya Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa karibu na kuzipeleka *NGO* mbalimbali katika Mkoa wa Iringa ili kuendesha semina katika Mabaraza ya Ardhi. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niziagize Halmashauri kwa sababu vyombo hivi tumeviunda Kisheria na viko chini ya Halmashauri husika. Ni jukumu la Halmashauri kuhakikisha kwamba wajumbe hao wanapata elimu na ni jukumu la Halmashauri kuhakikisha kwamba Mabaraza hayo yanafanya kazi kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, niziagize Halmashauri zote kama walivyofanya kwa Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Mufundi, Iringa Vijijini, wametenga Bajeti maalum kwa ajili ya kuhudumia hayo Mabaraza ya Ardhi. Pia kwa ile asilimia 20 ambayo inarudi vijijini ningeviagiza Vijiji vyenyewe vitenge asilimia fulani kwa ajili ya kuhudumia hayo Mabaraza ya Ardhi.

**MHE. CHACHA Z.WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja ndogo la nyongeza. Ningependa kuiuliza Serikali kwamba ina mpango gani wa kuwamilikisha wananchi Watanzania ardhi kwa utaratibu unaoeleweka Kimataifa wa *Title Deeds.* Kwa sababu sasa hivi ardhi ni mali ya Serikali na vijiji ambavyo sasa hivi ni vijiji vya makazi ndivyo vinavyomiliki ardhi wakati ambapo wananchi wenyewe wote Watanzania hawana *Title Deeds* kumiliki ile ardhi. Sasa tunaingia kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki ambapo wenzetu wa Kenya na Uganda wana *Title Deeds* ambazo wanamilikishwa ardhi kwa miaka 90 na wanaweza hiyo ardhi wakawarithisha watoto wao. Lakini sisi hapa Tanzania inaonekana ardhi yetu inakuja kugawiwa kwa wawekezaji. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwamilikisha wananchi wa Tanzania ardhi mtu mmoja mmoja binafsi ili waweze kuithamini na kutumia kwa njia inayofaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu sasa hivi kuna Hatimiliki za Kimila, tangu tuanzishe hayo Mabaraza ya Ardhi imetolewa idhini kwamba watoe Hati za Kimila. Zile Hati zinafahamika kisheria na baadaye zitakuwa zimemilikishwa kihalalia kama zilivyo Hati nyingine ambazo zinatolewa na mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**MHE. JAMES. P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata yameanza kuonyesha kero kubwa kwa maana ya kula rushwa. Je, kuna njia gani za mkato za kuvunjilia mbali Mabaraza yenye kero kama hizo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Spika, hatuwezi kukataa kwamba kwenye Mabaraza ya Ardhi hakuna rushwa moja kwa moja. Lakini hatuwezi vilevile kukubali haraka haraka kwamba huo ndiyo mtindo au mfumo wa uongozi katika Mabaraza hayo. Mimi ninafikiri changamoto ya rushwa Mheshimiwa James Musalika anajua na ndiyo maana juhudi nyingi sana zinafanywa na Serikali katika kila eneo kujaribu kuchukua hatua za kupambana na tatizo hilo kwa upana wake. Mabaraza ya Ardhi ya Vijijini yameundwa kwa utaratibu ambao unatokana na mamlaka ambazo Serikali za Vijiji zimepewa.

Kwa hiyo, wito wangu mimi kwa Serikali zote za Vijiji endapo itabainika mmoja wa wajumbe yeyote ambaye tabia yake haiendani na maadili ya uongozi katika utekelezaji wa majukumu yake, Serikali za Vijiji zina mamlaka ya kumwondoa katika eneo hilo na kutoa nafasi hiyo kwa mtu mwingine. Mimi nafikiri ni vizuri hili likatambulika kwa Serikali zote za Vijiji wao ndiyo wenye mamlaka makubwa sana juu ya jambo hilo. Lakini vilevile kama itabainika waziwazi kwamba jambo hilo limetokea, mimi ninashauri tu hatua za kawaida za kisheria zichukuliwe akamatwe apelekwe Mahakamani, ashitakiwe, akithibitika kwamba ametenda kosa basi hatua za kisheria za kumfunga ziweze kuchukuliwa. Lakini tutaendelea kufanya kazi kwa karibu sana na Halmashauri na kuendelea kuhimiza na kuwashauri wawe karibu sana na vyombo hivyo ili kuhakikisha kwamba vinakuwa vya uadilifu.

Na. 117

**Ujenzi wa Daraja la Mto Lukwamba**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa kuwa, daraja lililopo katika Mto Mkwamba linalounganisha vijiji vya Mburusa na Mpombe na Ndachela kwa upande wa pili lilizolewa na maji miaka kadhaa iliyopita na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wa vijiji hivyo na Kata nzima ya Napacho na wawindaji wanaokwenda kwenye Hifadhi ya Lukwika Wilayani Nanyumbu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, kuchelewa kulijenga daraja hilo kunaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi kwani wanashindwa kwenda hospitali na Makao Makuu ya Wilaya na pia kufanya shughuli za uzalishaji mali?

(b) Je, ni lini sasa Serikali italijenga daraja hilo ili kuwapunguzia kero wananchi wa Kata ya Napacho?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kurekebisha kuwa daraja analoongelea Mheshimiwa Mbunge ni la Mto Lukwamba na sio Mkwamba. Ni kweli kabisa daraja la Mto Lukwamba lililozolewa na mafuriko yaliyotokea mwaka 1990 Mkoani Mtwara liko katika barabara ya ulinzi ya Madimba – Kitaya- Mnongodi – Mbuyuni-Mapili-Mitemaupinde. Barabara hii ni ya ulinzi na inaendelea kukarabatiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara, yaani *TANROADS* Mkoa wa Mtwara. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 – 2006/2007 barabara hii imefanyiwa ukarabati wa jumla ya kilometa 5, usanifu kuanzia kijiji cha Mnongodi – Mapili hadi Mitemaupinde ikiwa ni pamoja na daraja la Lukwamba kwa gharama ya shilingi milioni 130. Daraja hilo litakuwa na urefu wa meta 32 na litajengwa kwa zege. Imekadiriwa kuwa gharama za

ujenzi wa daraja hilo bila usimamizi utafikia jumla ya shilingi milioni 750. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu usumbufu wanaoupata wananchi wa Kata ya Napacho hasa wakati wa masika ndiyo maana maandalizi ya michoro na gharama za ujenzi yamefanywa na Serikali kwa lengo la kujenga daraja hilo ili kuondoa usumbufu huo. Aidha, Wizara yangu kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008 itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili kadri ya Bajeti itakavyoruhusu.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanatia matumaini kwa wananchi wa Kata ya Napacho. Pamoja na ufinyu wa Bajeti ambao ameuelezea Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, daraja hilo linategemea kuanza kujengwa lini na litakamilika lini ili wananchi wa vijiji vya Mpombe na Mburusa waweze sasa kunufaika kulitumia hilo daraja?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, nimesema kwa kweli kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha kulingana na uwezo utakaokuwepo kwa maana ya Bajeti kupitishwa na Bunge hili tutaanza kujenga daraja hilo. Lakini hili litategemea sana uwezo na Bajeti kuweza kupatikana katika mwaka ujao wa fedha. Kama nilivyoeleza Serikali inaelewa sana tatizo hili ndiyo maana juhudi hizi na tumeanza na usanifu na baada ya hapo kwa kweli ni suala la ujenzi kutegemea kama tutapitishiwa Bajeti tutakavyokuwa tumeomba.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika mafuriko makubwa yaliyotokea mwaka 1990 ambayo yaliharibu miundombinu nyingi na hasa madaraja mengi kati ya Mingonyo na Masasi na ningemwelekeza Mheshimiwa Naibu Waziri katika madaraja hasa ya Nanganga na Nangoho na Namakongwa na kadhalika. Wizara itatengeneza lini madaraja hayo ambayo yanatishia usalama wa raia na kadhalika na hasa madaraja mawili ya Nangoho pamoja na lile Nanganga yamekwishaanza kutitia yako karibu na maji. Hata maji ya kawaida yanaweza yakayazoa madaraja hayo. Je, Serikali inasema nini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema kwamba madaraja hayo ya Nanganga na Nangoho na pale Namakongwa yalizolewa na maji ya mvua katika miaka hiyo ya 90. Kwa kweli Serikali imekuwa ikijaribu kuweka Bajeti kuweza kuyatengeneza au kuyarudisha katika hali yake madaraja hayo.

Lakini tatizo ni kwamba ufinyu ni Bajeti umekuwa ni kikwazo. Kwa hiyo, Serikali imezingatia hili na nakumbuka kwa nimeshajibu swali kwamba tutaendelea kujaribu kuweka Bajeti ili kurekebisha angalau daraja moja moja kila tunapokuwa na uwezo ili hatimaye yaweze kurudi katika hali yake.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Swali la Nanyumbu linafanana kabisa na madaraja yaliyoko Kata ya Ngumbo, Jimbo la Mbinga

Magharibi ambayo Serikali mwaka jana imeyajenga na mvua imeyachukua yote na ikizingatia kwamba barabara hiyo ni moja tu inayounganisha Jimbo zima. Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha madaraja hayo haraka?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Komba kwa namna anavyofuatilia kero za wananchi wake hasa kuhusu miundombinu. Ni kweli kwamba mimi na yeye tulipita katika Kata hiyo Ngumbo tukakagua madaraja hayo wakati yakijengwa na tuliamini kwamba baada ya pale kungekuwepo na urahisi sasa wa kupita katika barabara hiyo inayo unganisha Jimbo zima.

Lakini ni kweli kwamba baada ya mvua za hivi karibuni madaraja hayo yamevunjika na tuliyaweka katika mpango wa dharura wa kuweza kujengwa na tuliomba fedha, sasa hivi tunaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha ili madaraja hayo pamoja na maeneo mengine ambayo yaliathirika sana wakati wa mvua hizi zilizopita tuweze kurekebisha pindi tukipata uwezo huo kwa maana ya Bajeti hiyo ambayo tuliiomba kama mnakumbuka zaidi ya bilioni 10, basi tuweze kurekebisha hali hiyo.

Na. 118

**Barabara ya Ipole –Koga- Inyonga**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Ipole-Koga-Inyonga ilitengewa shilingi milioni 600 katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 lakini hali ya barabara hiyo ni mbaya sana:-

(a) Je, Serikali iko tayari kueleza jinsi shilingi milioni 600 zilizotengwa kwa ajili ya barabara hiyo zilivyotumika?

(b) Je, Mikoa ya Tabora na Rukwa inashirikiana vipi ili kuhakikisha kwamba pande zote za barabara hiyo zimetengenezwa kwa kiwango cha kuridhisha?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika Bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha wa 2006/2007 barabara ya Ipole – Koga - Inyonga yenye urefu wa kilometa 135 ilitengewa fedha kiasi cha shilingi milioni 600.

Lengo lilikuwa ni kuifanyia matengenezo barabara hii kwa awamu kutegemea uwezo wa Serikali. Hivyo fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya kipande cha barabara kutoka Ipole hadi Koga kilichopo ndani ya Mkoa wa Tabora chenye urefu wa kilometa 70 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa sehemu mbaya zenye jumla ya urefu wa kilometa 30 ikiwa ni pamoja na kuinua tuta la barabara kwenye mbuga ya Koga.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha utekelezaji wa kazi zilizopangwa, kazi ya matengenezo ya barabara hiyo iligawanywa katika sehemu mbili kama ifutavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza ni kutoka Ipole hadi Iswangala yenye urefu wa kilometa 45. Kazi katika sehemu hii inafanyika kwa kutumia mkarandasi M/s *Anam Road Works* wa Tabora kwa gharama ya shilingi 217,910,000/= na anatakiwa akamilishe kazi hiyo kwa muda wa siku 240 kuanzia tarehe 25/11/2006 hadi 23/07/2007. Hadi sasa kazi ya kusafisha eneo la barabara imekamilika katika urefu wa kilometa 18 na Mkandarasi ameshalipwa shilingi 14,168,000/=.

(ii) Sehemu ya pili ni kutoka Iswangala hadi Koga mtoni yenye urefu wa kilometa 25. Kazi katika sehemu hii pia inafanyika kwa kutumia mkandarasi M/s *Anam Road Works* wa Tabora kwa gharama ya shilingi 373,718,000/= na anatakiwa aikamilishe kwa muda wa siku 240 kuanzia tarehe 25/11/2006 hadi 23/07/2007. Hadi sasa kazi ya kusafisha eneo la barabara lenye urefu wa kilometa 12.8 na kuinua tatua la barabara la kimo cha meta moja lenye urefu wa kilometa 1.3 imekamilika na Mkandarasi amekwishalipwa jumla ya shilingi 47,916,000/= kwa kazi hizo.

Jumla ya thamani ya mikataba hiyo miwili ni shilingi 591,628,000/=. Kwa hiyo inakaribi hili shilingi milioni 600 iliyokuwa imetengwa. Serikali itaendelea kutenga fedha za maendeleo kila mwaka hadi barabara yote ya Ipole – Koga – Inyonga itakapokuwa imekarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika wakati wote.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge ako Tukufu kuwa Mikoa ya Tabora na Rukwa inashirikiana katika kuhakikisha kwamba pande zote za barabara zinatengenezwa kwa kuweka barabara hiyo katika mipango yao ya matengenezo ya kila mwaka. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti inakuwa vigumu kufanya matengenezo ya kuridhisha kwa barabara yote kwa wakati mmoja. Matengenezo muhimu kwa pande zote mbili za mikoa hiyo yataendelea kufanyika kadri fedha zitakavyopatikana.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa. Kwa kuwa wananchi wa Mpanda wako kisiwani na Mheshimiwa Naibu Waziri ameniambia yule Mkandarasi anatengeneza ile barabara ya Ipole – Koga. Barabara ile ni mbaya haifai. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Mpanda pamoja na wananchi wa Sikonge kuhusu barabara hiyo?

Pili, kwa kuwa wananchi wa Mpanda wanahali ngumu ya maisha kutokana na barabara mbaya zimeharibika, nauli zimepanda. Kutoka Sumbawanga mpaka Mpanda nauli imekuwa shilingi 40,000, Kisiwa kutoka Mpanda kwenda Tabora reli haifai. Je. Serikali ina mkakati gani kuhusu masuala ya barabara, vile vile Naibu Waziri yupo tayari mimi na yeye kwa ruksa yako tuondoke naye kwenda Mpanda akaone hali halisi ya wananchi wa Mpanda.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa gari likiharibika njiani huko unakosema itakuwaje? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba usafiri wa barabara katika Wilaya ya Mpanda ni mbaya na ndiyo maana Serikali katika mikakati yake imekuwa ikieleza jinsi ambavyo imedhamiria kupanua usafiri na kuuboresha katika Mkoa wa Rukwa kwa ujumla na Mikoa mingine ya Magharibi na jana tu tumezungumzia jinsi ambavyo Serikali ina mpango wa kujenga barabara ile ya Tunduma –Sumbawanga na baadaye Sumbawanga kwenda Mpanda na Kigoma; na ni kweli kwamba kutoka Mpanda kuja Tabora kwa kupitia Inyonga – Koga – mpaka Ipole barabara ni mbovu na mimi nashuhudia hilo lakini nimeeleza katika majibu yangu kwamba Serikali kwa kutegemea fedha zake ambazo inaweka katika Bajeti yake ya kila mwaka tutandelea kuboresha kama ambavyo tumefanya tumeweka hizo shilingi milioni 600 hazitoshi kwa kweli lakini tunaahidi kwamba kila mwaka tutakuwa tunaweka fedha ili tuweze kwa kweli kurekebisha hali hiyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Rukwa na Tabora Serikali inafahamu tatizo hili na itakuwa inashughulikia kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Sasa ameeleza kwamba hali ni mbaya na akaomba kwamba je, tunaweza tukaandamana mimi na yeye kwenda kule. Sasa ingawa nimetoka Mkoa wa Rukwa hivi karibuni na nimepitia barabara hiyo kuanzia Tunduma – Sumbawanga –Mpanda – Inyonga –Koga –Ipole mpaka Sikonge na nikarudi mpaka Ruangwa lakini kwa maombi yake rasmi nipo tayari kurudi tena tukiambatana naye tuone barabara. (*Kicheko*)

**MHE. SILAJI JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

**SPIKA:** Ni moja tu Mheshimiwa.

**MHE. SILAJI JUMA KABOYONGA:** Ahsante sana swali langu ni kwamba hivi karibuni viongozi wa ngazi za juu wa Serikali walifanya Mkutano na Ma-*RC* na Ma-*DC.* Katika kikao hicho ilitamkwa kwamba Serikali kwa kutambua matatizo ya barabara itatenga fedha za dharura shilingi bilioni 10. Mkoa wa Tabora ulitengewa shilingi 478, milioni. Barabara ya Itigi, Tabora mpaka Urambo ni miongoni mwa barabara zilizoharibika sana wakati wa mvua zilizomalizika hivi karibu. Hakuna senti hata moja katika hizo milioni 478 kwa ajili ya dharura kwa ajili ya barabara hii. Swali ni lini Serikali ita-*release* hizi shilingi milioni 478 ili barabara hii iweze kutengenezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wizara yangu ilikadiria kwamba shilingi bilioni 10.3 zilihitajika kwa dharura kuweza kutengeze barabara zilizokuwa zimeharibika na madaraja wakati wa mvua za hivi karibuni. Maombi hayo yalifikishwa hazina na sasa kinachofanyika kwa kweli ni utaratibu wa kuweza kupata fedha zile ili marekebisho hayo yaweze kufanyika. Lakini tumewaeleza wataalam wetu wa TanRoads pale ambapo kuna uwezo wowote wa kusaidia hasa pale ambapo kwa kweli kumekuwa na matatizo kabisa ya njia kupitika wafanye utaratibu wa kutumia ama fedha walizonazo au utaribu mwingine wa kutumia makandarasi ambao wamewazoea kwa maana ya kufanya nao kazi ili kazi hizo vifanyike wakati tunangojea fedha utaratibu ndani ya Serikali ufanyike kuweza kupata hizo fedha. Tutaendelea kufuatili suala hili tuweze kupata hizo fedha na maeneo kama hayo ambayo kwa kweli yameharibika sana yaweze kurekebishwa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi limeuliza tatizo ya barabra iliyotajwa hapo juu linafanana kabisa na tatizo ya barabara ya Kisesa kwenda mpaka Usagala. Mwaka wa fedha wa 2006/2007 barabara hii ilitengewa fedha na mpaka sasa hakuna matengenezo yanayolingana na fedha zilizotengwa ambayo yamefanyika. Je, Serikali sasa itanieleza nini na mwaka wa fedha unaisha karibuni?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kisesa *by pass* ambayo Serikali iliahidi kuijenga kwa kiwango cha lami ili kuwezesha magari yanayotoka Rwanda, Burundi kupitia Kagera Usagara ambayo hayana sababu ya kuingia mjini Mwanza basi yapitie katika hiyo *by pass* ya Usagara kwenda Kisesa na yale yanayotoka Shinynga ambayo hayana sababu ya kuingia mjini Mwanza yapite huko. Na kama tulivyowahi kujibu katika Bunge hili ni kwamba tulikuwa tunafanya usanifu wa ujenzi wa barabara hiyo lakini kazi kwa maana ya fedha za ujenzi wa barabara hiyo lakini kazi kwa maana ya fedha za ujenzi wa barabara hii ilikuwa imeahidiwa na *European Union* fedha hizo tunaendelea kuzifuatilia kwa sababu si hiyo tu *by pass* lakini ni pamoja na ujenzi wa barabara ya kutoka Nyanguge kuelekea Musoma. Fedha hizi zitakapopatikana barabara hii itajengwa kama ilivyoahidiwa.

Na. 119

**Ubovu wa Barabara – Jimbo la Solwa**

**MHE. AHMED ALLY SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara itokayo *Old Shinyinga* kwenda Pandagichiza, Liselamagazi, Solwa na kuingia Salawe yenye urefu wa kilomita 80 na inayounganisha Mkoa wa Shinyanga na Mwanza katika shughuli za biashara, kilimo na ufugaji ni mbovu sana; na kwa kuwa fedha inayotengwa katika ukarabati wa barabara hiyo ni ndogo sana hali inayosababisha magari kusitisha huduma zake hivyo wananchi kupata usumbufu mkubwa; na kwa kuwa tathimini iliyofanywa na *TanRoads* Shinyanga ilionyesha kuwa ukarabati mzuri wa barabara hiyo unahitaji jumla ya shilingi milioni 700.

(a) Je, kwa nini Serikali isitenge fedha zinazohitajika kiasi cha shilingi milioni 700 ili barabara hiyo ikarabatiwe vizuri na hivyo kwenda sambamba na dhana ya kuwaletea wananchi maisha bora kwa kila Mtanzania?

(b) Kama Serikali inakubaliana na gharama hizo. Je, Serikali itakuwa tayari kuweka fedha hizo katika Bajeti ya 2007/08.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Jimbo la Solwa, napenda kutoa maelezo mafupi kuhusu hali na matengenezo katika barabara tajwa kama ifuatavyo:-

Barabara kutoka Shinyanga mjini kupitia *Old Shinyanga* na kwenda Pandagichiza, Iselamagazi, Solwa hadi Salawe yenye urefu wa kilometa 94 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na wakala wa barabara Mkoa wa Shinyanga. Barabara hiyo inapitika vizuri majira ya kiangazi na kwa matatizo kidogo majira ya masika na wakala wa barabara Mkoa wamekuwa wakiifanyia matengenezo kila mwaka ili iweze kupitika wakati wote. *(Makofi)*

Katika mwaka wa fedha 2006/2007 barabara hiyo imetengewa shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukarabati na shilingi milioni 43.583 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida. Matengenezo hayo ambayo hivi sasa yanaendelea yatasaidia kupunnguza kero kwenye baadhi ya maeneo hususan sehemu korofi katika barabara hiyo.

Aidha tathimini aliyonayo Mheshimiwa Mbunge yenye kuonyesha mahitaji halisi ya shilingi milioni 700 ni sahihi na yanatokana na makadirio ya gharama halisi *(unconstrained budget)*. Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali fedha hizo hazikuweza kupatikana katika mwaka huu wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo hayo mafupi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Jambo la Solwa lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kuwa Bajeti ya Serikali ni finyu, Serikali haiwezi kutenga kiasi hicho cha fedha kwa mwaka 2007/2008. Badala yake Serikali kwa sasa itaendelea kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo ili iendelee kupitika pamoja na barabara zingine Mkoani Shinyanga kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa kila mwaka Bajeti huwa ni finyu na haitoshelezi kabisa katika kukarabati barabara hiyo ya Mkoa au za Halmashauri katika Jimbo la Solwa; na kwa kuwa mvua kubwa iliyonyesha katika jimbo la Solwa iliyosababisha mafuriko na iliyopelekea hata Mheshimiwa Rais kutembelea eneo la ikonda katika Kata ya Samuye hata Mheshimiwa Mizengo Pinda naye alikuwepo iliharibu sana barabara zote za jimbo la Solwa ikiwemo hii ya *Old Shinyanga* Salawe.

Niiombe sasa Wizara ifikirie kwa jicho la huruma kutoa fedha angalau ziweze kutosha kukarabati barabara hii ya Ikonda Masengwa Solwa Didia Imenya Ishinabulandi pamoja na hii ya Ikonda angalau sasa barabara ziweze kupitika na uchumi uweze kurudi katika hali yake katika Jimbo la Solwa?

La pili kwa kuwa maamuzi ya kuona ni tofauti sana na maamuzi ya kuambiwa na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge waliomwomba Mheshimiwa Naibu Waziri na nina imani katika Mkoa wa Shinyanga ni muda mrefu au hajawi kufika kabisa, aje atembelee jimbo la Solwa kuona hizi barabara nilizozitaja ili sasa aweze kufikiria na kutuongezea fedha za kutosha?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nadhani utatangulia kwanza kwenda Mpanda kabla ya kwenda Solwa. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwanza ni mpongeza sana sana Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, kwa namna anavyofuatilia matatizo hasa katika Jimbo lake la Solwa na niseme tu kwamba kwa kweli Solwa safari hii kweli wamepata Mbunge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ni kweli barabara hizo zinahali mbaya lakini uwezo wa Serikali kwa kweli ndiyo unaotukwamisha. Jicho la Serikali kwa kweli ni la huruma katika nchi nzima. Lakini bahati mbaya fedha hazina jicho la huruma sana kwa maana ya Bajeti ya Serikali lakini pale uwezo unapopatikana tutaendelea kuweka fedha ili barabara hizi hasa ile ya *Old Shinyanga* kwenda Salawe tuweze kuikarabati hatua kwa hatua.

Mheshmiwa Spika nimeshafika Mkoa wa Shinyanga lakini ni kweli kabisa kwamba sikuweza kufika katika safari yangu ya kwanza katika Jimbo la Solwa. Kwa hiyo, ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafika Solwa lakini baada ya kwenda Mpanda ili kuweza kuona matatizo ya barabara katika Jimbo hilo. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Naibu Waziri huyu anamsimamo ndiyo uzuri wake hayumbi hovyo. Naona Mama Josephine Ngenzabuke hajauliza siku nyingi. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Matatizo yaliyoko Solwa ni sawa ni matatizo yaliyoko Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma tumekuwa na matatizo ya ukosefu wa barabara kwa muda mrefu na mara nyingi tumekuwa tukitumia reli. Lakini reli yenyewe sasa hivi imechoka ikiwa ni pamoja na treni hatimaye kusababisha ajali za mara kwa mara kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma ambao tegemeo lao limekuwa ni reli.

Je, sasa Serikali sasa haoni umuhimu wa kuweza kututengenezea barabara reli tunayoitumia imkuwa ni chombo cha kutishia maisha ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma na Tabora ili na sisi tuweze kupata njia mbadala badala ya reli? (*Makofi*)

**SPIKA:** Isiwe badala iwe pamoja na reli.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – ( MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nia ya Serikali ni kuboresha njia zote za usafiri kwa maana ya barabara pamoja na reli na ndiyo maana kwa upande wa barabara tumezungumzia sana namna ya kufungua mkoa Kigoma kutokea Sumbawanga kwa maana ya Mkoa wa Rukwa na vile vile kupitia Mkoa wa Tabora.

Ahadi hizo ziko kwenye Ilani na tumekuwa tukielezea ni hatua gani ambazo tumefikia katika kujenga barabara hizo na hata jana tumeelezea hilo. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi kuhusu hilo tutaendelea kutekeleza ahadi hiyo.

Hata kwa upande wa reli kama ambavyo tumeeleza hapa Serikali imeamua kukodisha Shirika la Reli ili kuboresha huduma hiyo ya usafiri wa reli na nina uhakika kwamba baada ya taratibu zote kukamilika na mwekezaji kuingia kwa maana ya kuanza kukodi Shirika hilo basi reli ya kati tutaiboresha ili hali iwe nzuri.

Naomba Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa maeneo hayo Mikoa hiyo ya Magharibi kuwa na subira wakati Serikali ikiendelea na taratibu ya kuboresha hali ya usafiri katika maeneo haya.

Na. 120

**Majambazi wanaowaua Wananchi**

**MHE. AME PANDU AME** aliuliza:-

Kwa kuwa majambazi huwavamia wananchi kwa ajili ya kuwanyang'anya mali zao na wakati mwingine huwaua wananchi hao wasio na hatia; na kwa kuwa kuna wakati wananchi hao hufanikiwa kupambana na majambazi hayo na hata kuwaua kabisa:-

(a) Je, kati ya jambazi na mwananchi ni nani anayevunja haki za binadamu?

(b) Je, ipo haki ya mwananchi yeyote kujifanya jambazi na kuhujumu wenzake?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Nungwi, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria. Vilevile kwa mujibu wa Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake aliyo nayo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni ya adhabu ni kosa la wizi kwa mtu yeyote kuchukua mali ya mtu mwingine pasipo idhini ya mwenye mali na pale mtu huyo anapotumia silaha au nguvu katika wizi huo, mtu huyo atakuwa ametenda kosa la ujambazi. Aidha vifungu 18A, 18B na 18C vya Kanuni ya adhabu vinatambua haki ya mtu kujilinda yeye na mali zake pasipo kuathiri Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame Mbunge wa Nungwi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya Katibu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hati hiyo mtu yeyote atakayetenda ujambazi dhidi ya mtu mwingine atakuwa amevunja sheria za nchi. Aidha hakuna mtu yeyote mwenye haki ya kisheria kujifanya jambazi na kuhujumu maisha na mali ya mtu mwingine.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa jambazi ni mtu anayetumia ukatili sana au ni mtu katili sana. Je, Serikali haini kuwa ipo haja ya kuonge adhabu kubwa sana au hata adhabu ya kifo kwa watu kama wale badala ya adhabu ya miaka 30?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, sheria zilizopo sasa kuhusu adhabu kwa kweli zinakidhi haja la msingi hapa ni lile ambalo Serikali inachukua la kuimarisha ulinzi kupitia Jeshi la Polisi na vikosi vingine vya dola kuhakikisha kwamba tunapambana na ujambazi kwa nguvu zote na kuundoa kabisa katika nchi yetu.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matukio yanayojitokeza katika ujambazi; jambazi anaingia ndani ya nyumba papo hapo ili kumuhujumu mwananchi; ni tukio ambalo halitalajiwi; na mwananchi wakati anamuua jambazi anaingia hatiaji. Je kwa kujinusuru mwananchi ili asiingie hatiani achukue hatua gani ili aepukane na hatia?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba ipo sheria ya mwananchi kujilinda. Lakini lazima kujilinda kwenyewe kulingane na kosa lenyewe. Huwezi kutumia nguvu za ziada katika kujilinda huko. Kwa mfano Kama mwizi amekuja nyumbani kwako anaiba chupa ya chai basi mwizi huyo huwezi kupambana naye kwa risasi. Ni lazima utazame aina ya namna ambavyo anavyokuja na tishio kwa upande wake. Ikiwa emekusudia kuhujumu maisha yako pale unayo haki ya kujitetea na kumwahi yeye mwanzo.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, nina swali dogo la nyongeza. Ametupa majibu kwamba tupime, hivi kweli hali ya majambazi wanavyoingia ndani ya nyumba, kuna nafasi ya *dialogue?* Mimi ninaomba anielimishe vizuri zaidi kwa sababu tulioko hapa wengi tumeishaibiwa na wala hatukupewa taarifa na majambazi. Kwa hiyo, kutueleza hivyo kweli siyo kutupiga chenga? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wako majambazi ambao ni hatari sana kwa maisha ya binadamu ambao huingia ndani ya majumba wakiwa tayari na silaha na kwa nia ya kumuua huyu mtu aliyeko katika nyumba. Kwa msingi huo, unayo haki kabisa ya kujitetea ili kummaliza yeye mwanzo kabla ya kukumaliza wewe. Ninachozungumzia hapa ni kwa wale watu, wezi wa kawaida. Ukikutana na jambazi, maana yake lina silaha, hiyo mnapambana moja kwa moja. Lakini, wale wezi ambao hawafanyi vitendo vya kuwa na silaha na vingine, sasa, moja kwa moja kumpiga risasi ya kichwa, wako wezi unaweza ukapiga risasi ya mguu na kadhalika. Kwa msingi huo Mheshimiwa Balozi Mongella ataangalia hali halisi ilivyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa maana nyingine kwa vibaka, mnaruhusiwa *dialogue*, lakini kwa majambazi ni mapambano. Tunaendelea! *(Kicheko)*

Sasa, tunahamia Wizara ya Fedha. Napenda nitambue uwepo wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ambaye alikuwa Washington *DC* akituwakilisha kwenye mazungumzo na Taasisi tunazowasiliana nazo, *IMF* na *World Bank*. Karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Na. 121

**Msaada wa Kutoka *European Development Fund***

**MHE. KABWE Z. ZITTO (K.n.y. MHE. DR. WILBROD P. SLAA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania kama mwanachama wa Mkataba wa Lome na sasa Mkataba wa Cotonou imekuwa ikinufaika na msaada kutoka *European Development Fund (EDF).*

(a) Je, kupitia *EDF 8* na *EDF 9*, Tanzania ilipangiwa fedha kiasi gani na imepokea fedha kiasi gani hadi sasa kwa kila *EDF* moja kama ilivyotajwa hapo juu?

(b) Je, fedha hizo zimetumika kwenye miradi gani kwa majina na mahali ilipo na miradi mingapi imekamilika kwa kila *EDF* na ni lini miradi hiyo itakamilika au iko katika hatua gani?

(c) Kwa kuwa Kamisheni ya Ulaya *(European Commission)* hivi karibuni ilitenga *Euro 40 bilion* kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya mkataba wa Cotonou kuanzia mwaka 2007. Je, ni masharti gani yanatakiwa kutekelezwa kabla. Tanzania imejiandaa vipi kutekeleza masharti hayo ili inufaike na msaada huo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kupitia *EDF 8*, Tanzania ilipangiwa kupatiwa jumla ya *Euro* 328.7 milioni ambapo hadi sasa, kiasi cha *Euro* 308.0 milioni kimetolewa. Kiasi kilichobaki kilihamishiwa *EDF 9* kufuatia tathimini ya utekelezaji wa muda wa kati wa *EDF 9* mwaka 2004 *(Mid-Term Review)*. Kwa kupitia *EDF 9* awali Tanzania ilipangiwa kupatiwa jumla ya *Euro* 290.0 milioni. Kiasi hiki kiliongezeka na kufikia *Euro* 414.58 milioni kufuatia tathimini ya mwisho *(End of Term Review)*. Hadi sasa kiasi cha *Euro* 214.1 milioni kimetolewa kutokana na *EDF 9*.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi 53 ilipangwa kutekelezwa chini ya *EDF 8*. Kati ya miradi hii, miradi 46 imekamilika na 7 ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha. Kwa upande wa *EDF 9*, jumla ya miradi 20 ilibuniwa ambapo miradi 10 imekamilika na miradi mingine 10 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Orodha kamili ya miradi yote ya *EDF 8* na *EDF 9* kwa majina, mahali ilipo na hatua iliyofikiwa ya utekelezaji ipo. Orodha hiyo ni ndefu, naomba nimpatie mwuliza swali baadaye. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, katika fedha zitakazotolewa na Kamisheni ya Ulaya kwa nchi wanachama wa *ACP*,Tanzania itapatiwa jumla ya *Euro* 540.0 milioni kupitia *EDF 10*. Kati ya fedha hizo upatikanaji wa *Euro* 100.00 milioni utategemea kufikiwa kwa vigezo vya ufanisi vitakavyokubalika na pande zote katika maeneo makuu matatu yanayohusu utawala bora na uwajibikaji.

Maeneo haya ni kudhibiti rushwa nchini *(control of corruption)*, uendeshaji wa uchumi *(economic governance)* na ubora wa mashirikiano *(quality of partnership)*. Kwa kuwa Rasimu ya vigezo hivyo katika maeneo haya matatu ni ndefu, nayo pia nitampatia Mheshimiwa mwuliza swali baadaye.

Majadiliano na sekta husika, Asasi zisizo za Serikali na Jumuiya ya nchi ya Ulaya yanaendelea ili kufikia makubaliano yaliyo na muafaka.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo mazuri sana ambayo ameyatoa alipojibu swali la msingi. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa ili kuweza kupata fedha za *EDF 10*, inatakiwa iandae *Country Strategy Paper* na *National Indicative Programme*. Je, Serikali itakuwa tayari kuzileta hizi Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuziona na kuweza kuchangia kabla ya kuwasilisha kwa *Europian Commission?*

La pili; kwa kupitia fedha ambazo tayari *Europian Union* wamefanya *commitment* kwa Tanzania, jumla ya *Euro* milioni 444 pamoja na hizo *Euro* milioni 100 ambazo zitatokana na mafanikio ambayo naamini kabisa kwamba yatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kwamba itakuwa ni busara kuhakikisha kwamba barabara kwa sababu sehemu kubwa ya hizi pesa zitaenda kwenye *infrastructure*, barabara ya Manyoni – Tabora – Kigoma inaingizwa katika pesa hizi ili tuweze kuhakikisha kwamba tunafungua eneo la Magharibi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwanza, utayarishaji wa *Country Starategy Paper* una muda maalum. *Paper* hiyo imeishatayarishwa na Serikali na imeishawasilishwa *Europian Union* na tutatiliana saini kama kila kitu kitakwenda sawa sawa kati ya mwezi Septemba na mwezi Oktoba. Kuhusu barabara ya Kigoma, pesa zilizopangwa na *Europian Union* zina miradi maalum na miradi hii imeisha kubalika. Kama mradi huu upo katika zile pesa za *EU*, tutahakikisha kwamba zinatumika. Lakini, maradi wa kutoka Itigi – Nzega – Tabora – Malagarasi – Kigoma, Serikali inazungumza na Wafadhili wengine. Majadiliano yako katika hatua nzuri. Namwomba Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto asubiri majadiliano na wafadhili wengine.

**MHE. MUSSA Z. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu imepata fursa nyingi sana ya kusadiwa na nchi mbali mbali hii ikiwa ni pamoja na China. Mheshimiwa Spika. Kamati yangu ya Mambo ya Nchi za Nje ilipata fursa ya kuiona baadhi ya miradi ya *Millenium Challenge Accounts* na miradi ambayo inapendekezwa kwa Serikali ya China katika mpango wa Bilioni 5. Mheshimiwa Spika, lakini katika miradi ile sikuona mapendekezo yoyote ya maboresho au ya matengenezo ya Reli ya Kati. Ninaomba kama muda bado upo, Reli hii iweze kuwa *accommodated* katika mradi huu wa mpango wa bilioni 5 za China. Je, Serikali iko tayari kulifikiria jambo hili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna orodha ya miradi ambayo itafadhiliwa na *Millenium Challenge Account*. Lakini, kama Naibu Waziri wa Miundombinu alivyojibu leo, Reli ya

Kati inakodishwa kwa Mwekezaji kutoka India.  Kwa hivyo ni vema tukamalizana kwanza na huyu Mwekezaji kutoka India kabla hatujaanza kuzungumza na Mwekezaji mwingine.

Na. 122

**Ununuzi wa Miti ya Mitiki**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2003/2004 kampuni ya *Fibreoards 2000 Ltd* ilishinda zabuni Na. 26 ya ununuzi wa mita 40,000 za ujazo wa miti ya mitiki kutoka shamba la Turiani Mtibwa, Mkoani Morogoro kwa *US$ 145* kwa mita za ujazo; na kwa kuwa Julai 15 kampuni ilivuna mita za ujazo 15,000 na kuziuza kwa kampuni ya *Navtar and Co.* ya *Dubai (UAE):*

Kwa kuwa mzigo huo haukuteremshwa Dubai, ulipelekwa moja kwa moja Banglalone India; na kwa kuwa *Fibreboards* iliuza kwa kila mita moja ya ujazo *US$ 455*.  Je, Serikali ilikusanya kodi gani kwa kila mita moja ya ujazo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mnamo mwezi Machi, 2004, kampuni ya *Fibeboards 2000 Ltd*. ilishinda zabuni ya kuuza magogo ya mitiki. Shughuli za uuzaji wa bidhaa hiyo nje zilidumu kwa muda wa miezi 14 kuanzia Mei, 2005 na ziliishia Juni, 2006 ambapo tenda ilitolewa kwa muuzaji mwingine. Aidha, takwimu zinaonyesha kuwa kati ya Mei, 2005 na Juni, 2006 kampuni hiyo iliuza nje bidhaa za magogo kiasi cha mita za ujazo 76,819 katika nchi mbali mbali ikiwemo India na *United Arab Emiretes (UAE)* kama ifuatavyo:-

*UAE*, tuliuza thamani ya shilingi milioni 246.8 kwa kiasi cha mita za uzito ($M^3$) 3,235.
India, tuliuza thamani ya shilingi milioni 5,126.4, kwa kiasi cha mita za ujazo ($M^3$) 40,275.

St. Helena, tuliuza kwa thamani ya shilingi milioni 604.8, uzito kwa mita za ujazo ($M^3$) 36,309.

Mheshimiwa Spika, jumla ya mauzo ilikuwa bilioni 5,978.00, kiasi cha mita za ujazo ($M^3$)) 79,819. Mheshimiwa Spika, pia mnamo Julai,  2005 kampuni ya *Fibreboards Ltd.* Iliuza magogo yenye jumla ya mita za ujazo 1,879 yenye thamani ya

shilingi milioni 526. kati ya hizo, mita za ujazo 1,440 ziliuzwa nchini India na mita za ujazo zilizobakia ziliuzwa St. Helena.

Aidha katika mwezi huo huo, kampuni hiyo ilipokea kutoka nje malipo *(inward remittances)* ya jumla ya dola za Kimarekani 916,966.64, sawa na dola za Kimarekani 488 kwa mita moja ya ujazo. Hata hivyo, si lazima kuwa malipo yaliyopokelewa na kampuni kwa kipindi hicho ni ya mita hizo za ujazo zilizosafirishwa Mwezi Julai. Utaratibu wa malipo hutegemea makubaliano ya muuzaji na mnunuzi na Serikali haihitaji kujua taarifa kama hizi, labda kuwe na sababu maalum.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2004 hadi 2006, kampuni hii ililipa kodi ya jumla ya shilingi 17,200,000/= kama ifuatavyo:-

Mwaka 2004, ililipa shilingi 4,200,000/=, Mwaka 2005, ililipa shilingi 6,400,000/= na Mwaka 2006, ililipa shilingi 6,600,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kodi hiyo ni kwa jumla ya faida yote iliyotokana na biashara kwa kila mwaka, si rahisi kujua ni kiasi gani kampuni ililipa kama kodi kwa kila mita moja ya ujazo ya magogo ya mitiki iliyouzwa na kampuni hiyo huko India kwa mwezi Julai, 2005.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia *TRA*, huwa inaweka vyombo mbali mbali ili kuhakikisha bidhaa zinazoingia nchini zinalipiwa kodi halali. Lakini, Serikali haiweki utaratibu wala vyombo vyovyote vya kuoa rasilimali zetu zinazokwenda nje kama zinapata bei mufaka. Je, kitendo hicho Serikali haionekani inasababisha urari wa biashara uendelee kuwa mbaya kutokana na bidhaa zetu kutokupata bei sahihi kutoka nje? Pili, kwa kuwa Serikali inawabana sana watu wanaoingiza bidhaa kama magari na kadhalika. kwa bei ndogo sana.

Lakini Serikali yetu inawaachia wanaosafirisha nje, kwa mfano wanaosafirisha dhahabu kwa bei ndogo sana kuliko bei hasa iliyoko sokoni, Almasi na kadhalika.. Je, Serikali haioni kwamba kwa utaratibu huu kama ni sera ya makusudi ya kuondosha rasilimali zetu bila kupata mapato sahihi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niseme kwamba si sahihi kusema kwamba Serikali haina utaratibu maalum wa kuweza kujua pale ambapo watu wanasafirisha nje bidhaa mbali mbali. Ni kwamba utaratibu uliopo, kwa mfano kama mtu anasafirisha labda ni korosho nje, basi anaposafirisha nje inajulikana kiasi gani kule kinapatikana na fedha ambazo zinapatikana kama ni *dollars* ama kama ni *Euro* zinaingia moja kwa moja nchini kwenye benki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *TRA* sasa hivi ina utaratibu kutokana na programu maalum ambayo inaitwa *Second Generation Reform Programme* na kuweza kujua kila kitu na ndio maana hata katika hali hii kwa mfano, unaweza kujua ni kiasi gani ambacho mtu ameingiza nchini. Itakuwa kwa kweli si sahihi na si kweli kusema kwamba watu

wanaposafirisha nje basi Serikali haina utaratibu wowote ule wa kujua. Utaratibu upo na namwomba Mheshimiwa Hamad Rashid, kama anataka kujua taarifa zaidi, basi niko tayari mimi kumpeleka kwa Ndugu Kitilya ili aeleweshwe vizuri utaratibu ambao umekuwepo na ambao unaonyesha urari ambao upo kwa upande wa Serikali na ndio maana kila siku tunasema ni kiasi gani ambacho kimepatikana, *otherwise* tusingeweza kupata utaratibu huu. Kwa hivyo, ningependa kusema kwamba suala ambalo Mheshimiwa Hamad Rashid alilolieleza kwamba si sahihi kusema kwamba Serikali haiweki utaratibu. Namwona anatikisa kichwa, lakini utaratibu ndio huo ulivyo.

Na. 123

**Majeshi Yetu Kushiriki Katika Ulinzi wa Amani**
**Chini ya Umoja wa Mataifa na wa Afrika**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni Mwanchama wa Umoja wa Mataifa *(UN)* na Umoja wa Afrika *(AU)*; na kwa kuwa Ulinzi wa Amani katika maeneo hayo ni miongoni mwa majukumu yake muhimu:-

(a) Je, Tanzania inatumia vigezo gani katika kutumia Majeshi yetu ua Ulinzi ana Usalama maeneeo mbali mbali duniani?

(b) Je, ni mara ngapi na wapi majeshi yetu yameshiriki kwa kazi za ulinzi wa Amani chini ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika?

(c) Je, Askari husika pamoja na Tanzania hufaidika vipi kutokana na huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa faida ya Ndugu zangu Wandishi wa Habari, Jina langu ni Omar Yussufu Mzee na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ni mdogo wangu, lakini sidhani kama nafanana naye. Pia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ili nchi iweze kuhusisha Jeshi lake katika shughuli za Ulinzi wa Amani, kwanza, nchi hiyo lazima ionekane na Umoja wa Mataifa kuwa inafaa kwa kazi hiyo na nchi yenyewe kufanya hivyo. Aidha, vigezo ambavyo Umoja wa Mataifa hutumia kuzipata nchi kwa ajili ya kushiriki shughuli za Ulinzi wa Amani. Vigezo hivyo ni kama ifuatavyo:-

Nchi lazima iwe huru na Mwanachama wa Umoja wa Mataifa.
Nchi iwe ya Kidemokrasia na kutambulika Kimataifa.
Nidhamu, imani na uhodari wa Jeshi lake.
Kukubalika na nchi husika.

(b) Mheshimiwa Spika, Jeshi letu lilianza kushiriki shughuli za kulinda amani mwaka 1993 nchini Liberia. Vile vile, kuanzia mwaka 1999, Maafisa wa Jeshi la Ulinzi

wamekuwa wanashiriki katika uangalizi wa amani katika nchi za Siera Leone, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia. Eritrea, Sudan, Ivory Coast na mwaka 2007 Tanzania imepeleka kikundi cha Askari 80 Lebanon, kwa mara ya kwanza nje ya bara la Afrika. Majukumu yote hayo ni ya Umoja wa Mataifa. Bado Tanzania haijaanza kupeleka Maafisa na Askari wake kwa majukumu ya Umoja wa Afrika.

(c) Mheshimiwa Spika, Tanzania inapopeleka Jeshi lake katika kutekeleza ulinzi wa amani, kipaumbele sio kwa Wanajeshi kujinufaisha bali ni kufanikisha jukumu walilopewa katika nchi husika.

Mheshimiwa Spika, Askari hufaidika baada ya kutekeleza jukumu lake. Yapo baadhi ya mambo ambayo nchi yetu Tanzania na Askari hunufaika. Mambo hayo ni:-

(i) Maafisa na Askari kujifunza na kuzoea kufanya kazi mbali mbali katika mazingira tofauti na yale waliyozoea.

(ii) Maafisa na Askari kupata fursa ya kubadilishana uelewa wa mambo ya kijeshi na wenzao wa nchi zingine.

(iii) Yapo malipo yanayotolewa na *UN* kwa Tanzania kwa ajili ya kugharamia vifaa vitakavyotumika katika majukumu ya kulinda amani.

(iv) Yapo malipo ambayo hutolewa na *UN* kupitia Serikali ya Tanzania kama posho ya Maafisa na Askari walioko kwenye Ulinzi wa Amani.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa sababu Tanzania ina wajibu wa kuchangia utulivu wa kisiasa wa nchi zenye matatizo kwa mfano Somalia na Jimbo la Darful kule Sudan. Na hasa kwa sababu machafuko ya kisiasa ya nchi hizo kwa namna moja au nyingine, yanaweza kusababisha hali ya uchumi wetu kijamii na kiuchumi kuwa mbaya. Je, kwa nini Tanzania iliamua kupeleka wanajeshi wake Lebanon nchi ambayo iko mbali na Tanzania badala ya kushughulikia matatizo ya nchi jirani ya Uganda kama vile ambavyo Uganda imefanya katika nchi ya Somalia. Je, hapa kuna siri gani iliyojificha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba: Je, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, lini watatembelea wanajeshi wetu walioko Lebanon ili kuona utekelezaji wa majukumu yao na vile vile kuwafariji? Je, ziara hiyo itakapofanywa, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuwashirikisha baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, akiwemo Waziri Kivuli wa Wizara hiyo Mheshimiwa Sanya?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu nililojibu juzi. Kwa kweli Tanzania tunataka tushiriki ulinzi wa amani katika sehemu zote kwa sababu wanajeshi tunao na wanajeshi wetu wana uwezo mzuri. Lakini hali yetu ya kiuchumi kivifaa hatuwezi tukashiriki katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, kushiriki kwa Lebanon tulikubali mwanzo kwamba tutashiriki Lebanon, baadaye ndiyo yakaja maombi ya Darful na Sudan. Kwa sababu tulikubali kushiriki Lebanon, tulilazimika kwanza kwenda kulingana na hali yetu ya

kivifaa. Mheshimiwa Spika, vifaa vitakapoimarika, basi tutashiriki Darful na Somalia pia. Suala la pili, nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu itakapoona kwamba kuna umuhimu wa kuwatembelea wanajeshi wetu walioko Lebanon na Kamati ya Ulinzi na Usalama itakapoona kwamba wana majukumu na wao kutembelea wanajeshi wetu walioko Lebanon, Wizara haitakuwa na tatizo isipokuwa, nitaiomba Ofisi ya Bunge iwawezeshe siyo Wizara ya Ulinzi. *(Kicheko)*

Na. 124

**Vigezo vya Kitaalam vya Kuweka Idadi ya Walimu – Sekondari za Kutwa**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:-

(a) Je, kwa vigezo vya kitaalam, Sekondari ya Kutwa inatakiwa iwe na walimu wangapi kwa viwango na fani kwa Sekondari zenye mikondo 2, 3 na 4?

(b) Je, kwa vigezo hivyo, hali ya walimu katika Sekondari za Wilaya ya Lushoto inaonyesha picha gani; na ni hatua zipi zinazohitajika ili kufikia uwiano sahihi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Napenda kujibu la Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Idadi ya walimu wanaotakiwa kuwepo katika shule ya Sekondari inapaswa kuzingatia vigezo vya kitaalam ambavyo ni fani za walimu, idadi ya mikondo na idadi ya vipindi 24 ambavyo mwalimu anapaswa kufundisha kwa wiki. Kwa kuzingatia vigezo hivyo, idadi inayohitajika kulingana na masomo ya msingi ambayo ni *Civics*, Kiswahili, *English*, *History*, *Geography, Mathematics, Biology, Physics* na *Chemistry* ni kama ifuatavyo:-

Shule yenye mikondo miwili, inahitaji walimu 3 wa sayansi na walimu saba (7) wa masomo ya sayansi jamii; na

Shule yenye mikondo 3 au 4 inahitaji walimu 6 wa sayansi na walimu 13 wa masomo ya sayansi jamii.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutumia vigezo vya kitaalam, hali inaonyesha kuwa Wilaya ya Lushoto ina upungufu mkubwa wa walimu. Wilaya hiyo yenye jumla ya shule za Sekondari za Serikali 50, inahitaji jumla ya walimu karibu 869 wakiwemo 273 wa masomo ya sayansi na 596 wa masomo ya sayansi jamii. Kwa sasa Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 248 ambapo kati ya hao 79 ni wa masomo ya sayansi na 169 wa masomo ya sayansi jamii.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa walimu Kitaifa uliosababishwa na ongezeko la shule za Sekondari mpya mwaka huu ulikuwa walimu 9,671. Serikali imechukua hatua mbali mbali kukabiliana na upungufu huo kwa kuajiri jumla ya walimu 6,668 na kuwapanga katika Mikoa yote. Mkoa wa Tanga umepatiwa walimu 75 wa Stashahada na 89 wa leseni ambao jumla yake inafika 164. Upungufu uliopo sasa Kitaifa ni walimu 3,003 ambao wanatarajiwa kupatikana kutoka Vyuo vya ualimu mwezi Juni, 2007. Serikali itaendelea kuwapanga walimu katika Mkoa wa Tanga kadri watakavyokuwa wanapatikana.

**MHE. WIILIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuelewa.

Mheshimiwa Spika, shule ya Bumbuli hivi karibuni wameondolewa walimu wanne (4). Shule ya Bumbuli ni moja kati ya shule 10 bora za Mkoa. Je, kuondoa walimu wanne (4) aliyefanya hivyo, nitamwelewaje, anataka iteremke; na ni lini watapelekwa wa kuwabadili?

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri Mkuu anatembelea Wilaya ya Lushoto, alituhurumia sana kwamba tuna wanafunzi 10,000 wanamaliza darasa la saba kwa hiyo kulikuwa na juhudi kubwa sana ambayo ilkuwa inatakiwa katika kujenga madarasa na nyumba za walimu. Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza kwamba tuongezewe madarasa 8 na nyumba za walimu 7. Je, ahadi yake itatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa walimu wengi wamehamishwa katika kipindi hiki kutoka katika shule zile za muda mrefu ili waweze kwenda kusaidia kuwa walimu wakuu katika shule mpya zilizoanzishwa sehemu mbalimbali nchini. Lakini pamoja na kuwaondoa walimu hao wanne kutoka shule ya Bumbuli, wapo walimu wengine wapya tuliowapeleka katika Mkoa wa Tanga. Katika shule hizi zote kama nilivyotaja walimu karibu 164 ambao wanakwenda kuchukua nafasi hizo hizo ambazo tumewaondoa walimu ambao wamekwenda kuchukua nyadhifa za kuwa walimu wakuu katika shule za sekondari mpya zilizoanzishwa. Huu ni utaratibu wa kawaida wa Wizara yetu kwa sababu huwezi ukamchukua mtu anayetoka Chuoni moja kwa moja ukamteua kuwa Mwalimu Mkuu. Si vizuri kwa sababu tunajua hajapata uzoefu. Sasa tunachukua wale wenye uzoefu ndio tunawapatia nafasi ya kuwa walimu wakuu katika shule hizo mpya. Lakini hali hiyo nina uhakika baada ya mwezi Juni, tutapata walimu wengine, natumaini kama nafasi ile itakuwa haijazibwa, itazibwa na hakutakuwa na matatizo.

Kuhusu swali la pili, kuhusu ahadi ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea aliona tatizo, na akasema ni vizuri mkaweza kuongezewa. Hilo lipo ndani ya uwezo wa Wizara, mara Wizara itakapoanza kupata fedha tutatekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niongezee kwa majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, baada ya swali la nyongeza ambalo limeulizwa na Mheshimiwa William Shellukindo. Ningependa hasa kujibu swali

la pili la Mheshimiwa Shellukindo hasa kuhusu msaada maalum kwa ajiil ya Wilaya ya Lushoto. Kwanza, nataka kusema kwamba utaratibu ambao umewekwa sasa hivi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambao kwetu sisi tunaona ni utaratibu mzuri, ni kwamba fedha zote zinazokwenda kwenye Mkoa zinafikishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa, ambaye tuliamini na tunaendelea kuamini kwamba atashirikisha uongozi wa Mkoa wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, katika kuamua jinsi ya kugawa fedha zilizotumwa kwenye Mkoa huo. (*Makofi*)

Wale waliochukua utaratibu huo hatukupata matatizo. Kule ambako tumepata matatizo ni Katibu Tawala wa Mkoa kukaa peke yake au kwa utaratibu ambao haukushirikisha viongozi wa Mkoa na kwa hiyo, kusababisha malalamiko mengi. Sitaki kutaja Mikoa iliyohusika na utaratibu huo. Lakini mimi ningependa kutoa wito kwa uongozi wa Mikoa yote kwamba fedha zinavyotumwa kwenye Mikoa ni vizuri ukaitwa uongozi wa Wilaya na Halmashauri, utaratibu ambao utashirikisha na Waheshimiwa Wabunge, kuangalia jinsi ambavyo wanaweza kugawa zile fedha ili vipaumbele vizingatiwe. Kama alivyosema Mheshimiwa Mshangama huenda Lushoto ina mahitaji makubwa zaidi kuliko Wilaya zingine, basi huo ndiyo wakati muafaka wa kukubaliana kwamba fedha hizi tulizopata kipindi hiki tuweke mkazo zaidi wapi na nadhani utaratibu huo ni mzuri Wizara ya Elimu, ingawa moja kwa moja. Lakini pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema kwamba kweli kutokana na mgao ulivyozingatiwa kwa Mkoa wa Tanga, ni vizuri sharti hilo likaangaliwa na kweli tuliahidi kwamba tutasaidia madarasa mawili na nyumba moja ya mwalimu. Sasa kama lilitekelezwa au halikutekelezwa ni suala ambalo tutalifuatilia lakini tulikubali kwa utaratibu huo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ndio mnaongezeka sasa. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo sijakusikia siku nyingi. Hebu tumsikilize Mheshimiwa Shellukindo.

**MHE. BEATRICE SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, nitajaribu kuongea kwa sauti ndogo maana yake mara nyingi sieleweki nikiongea kwa sauti yangu ya kawaida.

Pamoja na jitihada za wananchi wa Kilindi kujenga shule za sekondari ambako tungeweza kuchukua wanafunzi asilimia 100 na shule nyingine kubaki bila kupata wanafunzi; na kwa sababu Naibu Waziri amejibu kwamba walimu wamepangwa Mkoa wa Tanga, nadhani sabini na kitu; je, Waziri atatuambiaje Wilaya ya Kilindi kupatiwa mwalimu mmoja tu naye ambaye mpaka nakuja Bungeni aliyekuwa hajaripoti? Waziri atatuambiaje na atatusaidiaje wananchi wa Kilindi? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunapitiliza kidogo, mtakumbuka tulianza na matatizo matangazo kwa hiyo, naruhusu muda wa ziada wa maswali ili tumalize.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa Wizara yetu ili kuweza kurahisisha ugawaji wa walimu katika Mkoa, wanachuo wanapomaliza katika vyuo Wizara tunawapanga kimkoa. Mkoa wa Tanga ulipangiwa walimu 164. Sasa ni suala la Mkoa wa Tanga wenyewe, Afisa Elimu wa Mkoa pamoja na Maafisa waliopo katika Wilaya wanaeleza matatizo yalipo katika shule zao ili walimu wale wanaopelekwa katika Mkoa waweze kupangwa katika shule hiyo yenye matatizo. Kwa sababu siyo

rahisi sisi kufahamu moja kwa moja matatizo ya kila shule. Lakini Afisa Elimu wa Mkoa, pamoja na Maafisa waliopo kule wanafahamu matatizo hayo ndiyo maana tunawapelekea idadi ya walimu wao ndiyo wawagawe katika maeneo yale ambayo yana mahitaji.

Lakini tatizo lake ambalo inaonekana mwalimu hajafika katika shule hii, mimi naahidi nitafuatilia ili kuweza kuelewa Afisa Elimu wa Mkoa, amefanya nini na tuhakikishe kwamba mwalimu anafika katika shule hii mara moja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Pamoja na hatua nzuri za Serikali zilizochukuliwa kuajiri walimu lakini bado kuna tatizo kubwa sana la walimu wa sayansi; Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa walimu hao wanapatikana ili wanafunzi waweze kupata vipindi hivyo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Kiwelu, kama ifuatavyo:-

Kuhusu uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi tumeliona tatizo hilo na kama mmefuatilia tulitoa taarifa kwa vyombo vya habari kwamba tutaanza kuchukua wahitimu wa kidato cha sita waliofaulu katika kiwango cha *principal pass* moja na *subsdiary* moja. Uamuzi huo umetokana na kwamba wale wanaokuwa wamefaulu katika *principal pass* mbili mara nyingi wanakuwa ni masomo ambayo si ya sayansi , yaani sayansi ya jamii. Tumechukua hatua hiyo kwa makusudi ili tuweze kupata walimu waliofaulu *principal pass* za masomo ya sayansi kwa sababu wale wanaopata *principal pass* moja na *subsidiary* moja ndiyo hawa ambao wenye masomo ya sayansi. Kwa hiyo, tumeshusha kwa makusudi ili tuweze kupata wahitimu wenye masomo ya sayansi. Naamini kabisa mwezi Juni wale walimu ambao watapatikana miongoni mwao wengi watakuwa wenye masomo ya sayansi. (*Makofi*)

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ingawa swali langu limefanana kidogo na Mheshimiwa Grace Kiwelu. Pamoja na upungufu wa walimu kwenye sekondari, lakini tuna tatizo moja la walimu wa hesabu lakini lingine amesema Mheshimiwa Grace na kigezo kikubwa cha wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne kwa ajili ya kujiunga na kidato cha tano na kozi zingine, imekuwa ni kufanya mitihani ya majaribio ya hesabu na Kingereza. Sasa kutokana na tatizo hilo la kutokuwa na walimu wa hesabu, nataka kujua Wizara imefanya tathmini gani kuhakikisha kwamba tunapata walimu wenye vipaji vya hesabu katika shule zote za Sekondari? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tumegundua kwamba somo la hisabati lina matatizo hasa katika ufundishaji. Kwanza, tuna uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati kama nilivyosema hapo awali lakini pia hata jinsi njia za ufundishaji wenyewe, tumeona zina matatizo. Kwa hiyo, suala hili tumeshalizungumzia katika Mkutano wetu wa elimu tuliofanya Arusha hapo majuzi na kwa msingi huo tumeunda Kamati inayoshughulikia jinsi ya kuboresha ufundishaji wa somo la hisabati. Lakini wakati huo huo pia tumewasiliana na wenzetu wa Kenya ili na sisi tuanze kupeleka walimu Kenya kwa sababu kuna kituo maalum cha ufundishaji wa somo la Hisabati ambalo linaendeshwa kwa msaada wa *JAICA*. Kwa hiyo,

na sisi kuanzia mwaka huu tutaanza kupeleka makundi ya walimu kujifunza njia bora za ufundishaji lakini wakati huo huo na sisi wenyewe kuna *task force* ambayo inaangalia jinsi ya kuboresha ufundishaji wa somo la hisabati mashuleni. (*Makofi*)

Na. 125

**Wafugaji wa Kuku Singida**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. MARTHA M. MLATA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wafugaji wa kuku Mkoani Singida licha ya kukosa zana na mbinu za kisasa za ufugaji, wanakuwa wakilisha Dar es Salaam, Dodoma, Pwani, Morogoro na sehemu zingine kwa biashara ya kuku kwa miaka mingi:-

(a)Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwasogezea karibu watalaamu wa ufugaji wa kuku ili kuongeza ubora wa kuku?

(b) Je, Serikali inaweza kuwahimiza wawekezaji wa nje na ndani ili kuanzisha kiwanda cha *sausages* za kuku Mkoa Singida?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum Singida, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Singida ni kati ya mikoa yenye kuku wengi hapa nchini. Mkoa wa Singida una kuku wa kienyeji milioni 1.6. Baadhi ya kuku hao huuzwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro na Pwani.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida una watalaamu wa ugani 211 wakiwemo watalaamu wa mifugo 127 ambapo wenye shahada ni 7, stashahada 76 na astashahada 44. Watalaam hawa wamepangwa katika vijiji na kata za Wilaya zote za Mkoa wa Singida kama ifuatavyo: Halmashauri ya Manispaa 23, Wilaya ya Singida Vijiji 73, Iramba 67 na Manyoni 48. Wataalamu hao hutoa mafunzo ya ufugaji bora ikiwa ni pamoja na ule wa kuku kwa kutumia mbinu shirikishi. Hata hivyo, idadi hiyo ya watalaamu ni ndogo ikilinganishwa na jumla ya vijiji 360 vilivyopo Mkoani. Kwa hali hiyo, Wizara yangu itaendelea kujenga uwezo wa watalaamu hao kwa kuwapatia mafunzo na kuzihamasisha Halmashauri ziongeze idadi yao kwa kuajiri wengine kulingana na mahitaji pamoja na uwezo wa Serikali.

(b) Mheshimia Spika, vile vile nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba ni vyema kuwahimiza wawekezaji wa nje na ndani ili kuanzisha viwanda vya kusindika nyama ikiwamo ya kuku kwa kuwekeza katika mikoa mbalimbali ukiwemo Mkoa wa Singida. Sera ya Taifa ya uwekezaji inasisitiza kuhusu suala la kuwekeza vijijini na mijini.

Wizara yangu imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na kuku kwa kushirikiana na kituo cha uwekezaji (*TIC*) pamoja na balozi zetu zilizo nje ya nchi. Hata hivyo, kwa vile suala la uwekezaji linategemea matakwa na mwelekeo wa mwekezaji mwenyewe baada ya kujiridhisha na malighafi zilizopo, mtaji wake na soko, ujenzi wa kiwanda cha *sausages* Mkoani Singida utategemea aina ya mwekezaji atakayejitokeza.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kweli Mkoa wa Singida unaongoza kwa ufugaji wa kuku na kwa kuwa Mkoa wa Singida umekuwa ukitoa kuku kwa kwenda mikoa mbalimbali kama ilivyotajwa kwenye swali la msingi, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atanieleza ni kuku wangapi ambao kwa sababu wamekuwa na takwimu hasa kwa kipindi hiki cha *rift valley fever* kwa sababu kuna ugonjwa ambao umeingia na sasa watu wanahitaji sana mboga na mboga mbadala imekuwa ni kuku.

(a) Je, ni kuku wangapi wametolewa kwa Mkoa wa Singida katika kipindi hiki?

(b) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na vile nilivyosema, kwa sababu kuna magonjwa na ili watu tuwe na mboga mbadala imeonekana ni kuku zaidi; sasa anasemaje namna ya kuwahami kuku ambao wanasumbuliwa na magonjwa mengi kama vile kideli na mafua ya ndege. Je, wapo tayari kutoa chanjo ya kudumu kwa Mkoa wa Singida? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui hii idadi ya kuku lakini nakuachia tu uweze kuangalia utakavyojibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nifanye masahihisho kidogo kwa kile alichosema Mheshimiwa Killimbah kwamba Mkoa wa Singida unaongoza kwa ufugaji wa kuku. Kulingana na takwimu zilizopo Mkoa unaoongoza kwa kuku wa kienyeji ni Mkoa wa Shinyanga wenye kuku milioni tano. Mkoa wa pili ni Mkoa wa Mwanza. Ningeweza kuendelea kueleza mengine ila kulingana na muda hautoshi. Sasa naomba kujibu maswali yake kwamba hivi sasa Wizara inafuatilia biashara ya kuku wa kienyeji hasa kufuatia kuongezeka kwa ulaji wa kuku hasa wa kienyeji kutokana na kuwepo kwa bonde la ufa ambalo hata hivyo Serikali haijazuia wananchi kula nyama ya ng'ombe ilimradi iwe imepikwa vizuri kutokana na ng'ombe walio salama. (*Makofi*)

Kuhusu magonjwa ya kuku hususan wa kienyeji, ugonjwa mkubwa unaoathiri kuku wa kienyeji ni ugonjwa wa Kideli. Kuna chanjo za kideli, zipo za aina mbili, chanjo baridi, ambayo inabidi chanjo iwekwe kwenye jakofu kabla ya kutumiwa, na chanjo isiyohitaji kuwekwa kwenye jokofu. Chanjo hizi zinapatikana, Wizara inamwahidi Mheshimiwa Killimbah na wananchi wote wa Tanzania na kutoa wito kuwa tuwalinde wafugaji wetu wa kuku, chanjo ipo, ni rahisi hata kwa bei ili kusudi tuweze kuboresha ufugaji wa kuku wa kienyeji. Kuku 1000 wanaweza wakatumia shilingi 4000 tu kuweza kuipata chanjo hiyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. YONO. S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa biashara ya kuku inafanana kabisa na biashara ya nyama ya ng'ombe, je, Serikali inaweza ikatueleza ni

viwanda vingapi ambavyo vipo kwa ajili ya kusindika nyama ya ng'ombe kwani kuna mikakati mingi ambayo inafanywa lakini tunaona huwa haitekelezeki? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, viwanda vya nyama vilivyopo vya sasa nikijumuisha na machinjio ya kisasa ni pamoja na machinjio ya kisasa ya Dodoma yaliyopo hapa hapa. Kuna kiwanda cha mwekezaji kipo Mvomero, kinaitwa *daily investment*, kuna kiwanda cha nyama Sumbawanga kinaitwa Safi na kuna viwanda vingine vidogo vidogo vilivyopo Dar es Salaam vya usindikaji wa nyama ndogo ndogo *biltoms*. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali ulishapita na maswali yamekwisha. Matangazo tukianza na wageni. Naomba kwa heshima tutambue kuwepo pale kwenye *speaker's galley,* Mheshimiwa Balozi wa Poland nchini Bwana **Rwizad Malick.** *Welcome to Parliament your Excellence, we are very happy to see you coming from the friendly country of Poland welcome! (Makofi)*

Bado wageni wetu wale wa Chama cha Matibabu ya Asilia kutoka Tanzania na Kenya wapo pia na leo. Wamependa kukutana na Kamati ya Huduma za Jamii, kwa hiyo, nadhani utaratibu utakuwa umefanywa ili waweze kuonana na wajumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Janet Masubiri ameomba nitangaze kuwepo kwa wageni ambao ni watoto wake, naomba wasimame pale walipo, Juliana, Jacqueline, Monica, Angelina na Albetina. Mheshimiwa Huyu amejaliwa sana uzao wa watoto wa kike, kwa hiyo, wale Waheshimiwa Wabunge wenye watoto wavulana basi wachangamke. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Killimbah ameniomba nitangaze kuwepo kwa mgeni wake Mheshimiwa Omar Kami Kinota, Diwani wa Kata ya Shelui. Karibu sana Mheshimiwa Diwani. Natumaini kuna maendeleo mazuri ya ujenzi wa barabara ya kwenda Igunda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Genzabuke ameniomba nitangaze kuwepo kwa mgeni wake kutoka Wilaya ya Kigoma Kijiji anaitwa Pili Mvunye ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya UWT Kigoma Vijijini. Mheshimiwa Pili Mvunye karibu sana na pole na safari ndefu.

Matangazo ya Kamati. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda anawatangaziwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ikutane katika Ukumbi namba 432 saa 8.00 Mchana leo. Waheshimiwa Wabunge wote ambao hawakupata mikoba iliyohusishwa na semina *ya HIV aids* ya *USAID* wanaomba kuchukua mikoba hiyo sehemu ya mapokezi katika jengo hili hili pale sehemu ya mapokezi mikoba kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge ambao pengine hawaikupata siku ya *USAID* semina.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara anaomba wajumbe wakutane hivi punde saa tano, ukumbi namba 219 ghorofa ya pili. Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi

anaomba wajumbe wake wawe na kikao kifupi kesho saa tatu asubuhi katika ukumbi namba 428.

Waheshimiwa Wabunge ninayo maelezo yafuatayo kuhusu *Order Paper*. Kwanza niseme tu mtaona kwenye *Order Paper* ya jana kuna tofauti na leo. Tulitazamia tupokee taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi. Lakini tumejifunza kutokana na tukio la jana ambalo Kamati ya Huduma za Jamii ilipewa muda mfupi mno na Wabunge wengi wakajisikia vibaya. Sasa ofisi yangu ina utaratibu wa kuweza kujua zile taarifa ambazo zinahitaji muda mrefu zaidi. Kwa hiyo, tumejirekebisha na tukaona kwamba kutokana na utashi wa kutaka kuchangia taarifa za kamati ya fedha na uchumi na uwekezaji na biashara pamoja na maendeleo ya jamii zitakazokuja, Maliasili na Miundombinu tutaziweka katika orodha ya shughuli za Mkutano wa Nane ambapo tutashirikiana na Serikali kuweza kupata kupata muda wa kutosha ili taarifa hizi zisiwe tu ziliwekwa mezani lakini zipate nafasi nzuri ya mjadala. (*Makofi*)

Kuhusu tena *Order Paper* naomba nifanye mabadiliko kwa mpangilio kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge mbaki ndani ya ukumbi ili tufanye uchaguzi wa *University of Dar es Salaam Council* kwa sababu naelewa tukianza na Kamati wengi mnaweza mkatoka kwenda kunywa chai. Kwa hiyo, hata tukipiga kengele itakuwa siyo haki. Nadhani kwa kuwa bado na uchaguzi huu hauchukui muda kwa sababu upande mmoja kuna mgombea amejitoa, kwa hiyo, hakuna hata uchaguzi , kwa kweli kwa upande huo wa wanaume. Ni wanawake ndiyo sijui nitumie neno ving'ang'anizi lakini hapana naliondoa neno hilo, wanatumia haki yao ya kidemokrasia. Kwa hiyo, uchaguzi utakuwa kwa kweli ni mmoja tu, hivyo hatutachukua muda mrefu. Baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge ndiyo tutaendelea na mpangilio wa mtiririko wa Kamati ya Kilimo na Ardhi halafu tutamalizia na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mwisho kabisa Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Rais, kuhusu hatua yake ya kuiita Serikali ambalo ni tukio la mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu ili kujadili taarifa ya *CAG*. (*Makofi*)

Azimio hilo litawasilishwa kwetu na Mheshimiwa Balozi Dkt. Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe. Baada ya matangazo hayo sasa namwomba Katibu atuingize katika hatua inayofuata.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, shughuli inayofuata ni uchaguzi wa Wajumbe kwenye Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Naomba kutoa maelezo.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyokuwa imetangazwa siku ya Jumanne tarehe 17 Aprili, 2007, leo tarehe 20 baada ya kipindi cha maswali kama *Order Paper* ilivyosahihishwa, hivi sasa kutakuwa na uchaguzi wa Waheshimiwa Wabunge watakaowakilisha Bunge katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Muda wa mwisho wa kurudisha fomu za kuomba uteuzi ilikuwa ni Jumatano, tarehe 18 Aprili, 2007 saa 10.00 jioni. Muda huo ulipofika Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamejitokeza na kuchukua na kurejesha fomu ni 4 kama ifuatavyo:-

Kundi la wanawake: Katika kundi hili anatakiwa Mheshimiwa Mbunge mmoja, waliorudisha fomu ni wagombea wawili ambao ni Mheshimiwa Suzan A. Lyimo na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Hivyo basi katika kundi hili Waheshimiwa Wabunge

watapiga kura kumchagua Mgombea mmoja kwa kuweka alama ya *V* mbele ya jina la mgombea wanayemtaka kuwasilisha katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kundi B Wabunge wanaume. Katika kundi hili pia anatakiwa Mheshimiwa Mbunge mmoja, waliorudisha fomu ni wafuatao:-

Profesa Banyikwa ambaye ametangaza sasa hivi kwamba amejitoa, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mbunge. *(Makofi)*

Kwa utaratibu napenda athibitishe kauli yake hii mbele ya wapiga kura. Hivyo basi , katika kundi hili utaratibu utakaotumika kama atathibitisha hivyo ni kupita bila kupingwa. Uchaguzi huu unaendeshwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 9(a) na nyongeza ya pili ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, ambazo zinafafanua kuwa uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine ambavyo kwa mujibu wa Sheria zilizounda vyombo hivyo kwa mfano Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vitatakiwa viwe na uwakilishi wa Bunge utakaofanywa kwa kuzingatia kwa kadri iwezekanavyo uwiano wa idadi ya Wabunge wa vyama mbalimbali vya siasa vinavyowakilishwa Bungeni. Uwakilishi wa jinsia na uwakilishi wa pande zote za Muungano.

Kutokana na maelezo hayo mafupi na kwa mujibu wa kifungu cha 3(ii)(a) cha nyongeza ya pili ya Kanuni za Bunge kila mgombea atatakiwa afike mbele ya Waheshimiwa Wabunge yaani wapiga kura kujieleza kwa dakika zisizozidi tatu na kujibu maswali yao kama yatakuwapo. Baada ya kujieleza karatasi za kupiga kura zitatolewa, karatasi ya kupiga kura itakuwa ni moja kwa kila kundi na Waheshimiwa Wabunge watatakiwa kupiga kura moja katika kila kundi ili kupata Wabunge wawili watakaowakilisha Bunge katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo mwisho wa maelezo. Ahsante.

**SPIKA:** Mambo mawili tu, kwanza kuna kuweza kumsikia aliyejitoa mgombea Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ambaye nitampa nafasi na pili uchaguzi kwa kweli ni mmoja tu. Kwa sababu ikiwa kweli Mheshimiwa Profesa Mwalyosi kajitoa ina maana tutapigia tu kundi la wanawake kwa majina yale mawili. Ndiyo hivyo, ingawa pia nitatoa nafasi kwa Mheshimiwa Profesa Banyikwa, kusimama baadaye ili aweze kushukuru.

Sasa kabla hatujaingia kwenye zoezi hilo kuna matangazo muhimu ya Semina na Mikutano kwa ajili ya kesho na keshokutwa. Waheshimiwa Wabunge kesho saa 4 Tume ya Rais inayokusanya maoni kuhusu kuharakisha Shirikisho la Afrika Mashariki itakutana saa 4 katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Nakuombeni muhudhurie na kutoa maoni kwa sababu sisi ni wadau muhimu sana katika zoezi zima na niseme tu kwamba stahili za kawaida na hii ni zaidi hata ya kawaida zimeandaliwa kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Hii ni Afrika Mashariki sasa. Kwa hiyo, mambo yake tofauti kidogo. Jumapili tarehe 22 tutapokea taarifa za viongozi wa misafara ya mafunzo iliyofanyika na Waheshimiwa Wabunge mwaka jana hadi mwaka huu ili kujifunza mambo muhimu ambayo wameyakuta huko ambayo yanaweza kutusaidia katika kuboresha shughuli na huduma za Bunge letu. Hii nayo ni muhimu na Ofisi imeandaa utaratibu wa kawaida wa kuwaweka vizuri Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Sasa turudi kwenye uchaguzi wa Baraza la Chuo Kikuu, ningeomba sasa Mheshimiwa Profesa Mwalyosi aseme anayotaka kusema.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza naomba kuwashukuru sana kwa kunipa ridhaa ya kuwawakilisha katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kipindi cha takriban mwaka mmoja uliopita. Naamini kwamba nilifanya kazi hiyo vizuri na ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Kwa vile tunaogombea wote wawili, ni maprofesa na tuna uwezo sisi wote wa kuliwakilisha vizuri tu Bunge katika Baraza lile na kutokana na kwamba mimi nimepata bahati ya kuwa kwenye Bodi nyingi niliona si vema kung'ang'ania kuchukua nafasi nyingi ambazo zitanichukulia muda wangu wa kufanya kazi kwa umahiri na vizuri kwenye Bodi ambazo nipo na kuwawakilisha wananchi wangu wa Ludewa vizuri. *(Makofi)*

Pamoja na hilo sisi wote wagombea wanaume, ni wanachama wazuri na waumini wa CCM, niliona si vizuri wanachama sisi wa CCM tukawa tunang'ang'ania kitu ambacho sisi wote tuna uwezo na mimi ninaweza kufanya kazi nyingine. Kutokana na maelezo hayo nimeona afadhali mimi nimwachie mwenzangu aendelee kutuwakilisha kwenye Baraza la Chuo cha Dar es Salaam. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Profesa kwa moyo huo. Si viongozi wengi wana moyo kama huo wa kuachia achia mambo. Nakushukuru sana kwa mfano mzuri huo. Tunaingia kwenye zoezi la kuwasikiliza kundi la wanawake. Ningewasihi Waheshimiwa hii ya kushangilia kwa huyu aliyejitoa sawa. Lakini kwa hawa wawili nadhani tuwatendee haki tu, tuwasikilize. Kutakuwa na fursa ya kuuliza maswali yasiyozidi matatu, baada ya maelezo hayo ya dakika tatu. Baada ya hapo kura ziseme, lakini ushangiliaji na makofi inakuwa hautendi haki. Naomba hilo tulikubali. Ahsante sana.

Kwa hiyo, Katibu basi utusaidie kuwaweka, kuwapanga kadri ambavyo wamepangwa ili waweze kuja kujieleza. Sijui umefuata alfabeti au umefuata kitu gani?

**NDG. DAMIAN S.L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nimefuata alfabeti, nikianza na jina la mwisho alfabeti inayohusika na kuendelea. Kwa ajili hiyo tulikuwa tumemtanguliza Suzan A. J. Lyimo. Halafu atafuatiwa na Ruth B. Msafiri. Kiutaratibu wakati fulani tulikuwa tunapenda kwamba wakati mmoja anapokuwa anajieleza mwingine anakuwa nje. Kwa ajili hii tutamwomba sasa Mheshimiwa Ruth awe nje halafu nafasi hii tunaitoa kwa Mheshimiwa Lyimo. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Katibu unazo CV zao kabla hawajajieleza?

**NDG. DAMIAN S.L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, CV tunazo. Nadhani ni wakati muafaka labda tugawe kwa kila Mbunge au nisom?

**SPIKA:** Ili wasipoteze muda wao wagombea kwa muhtasari tu usome sifa zao kabla mtu hajaingia. Ni utaratibu wa kura maana yake akija hapa mtu akianza kusema

alizaliwa lini inachukua muda. Sasa kwa kifupi tufanye hivyo ili tumalize. Karatasi za kura zimegawiwa? Basi kama mmegawiwa, wagombea hawana haja ya kujieleza kirefu sana. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Suzan Lyimo.

Karibu Mheshimiwa Suzan Lyimo, unazo dakika tatu za kutoa maelezo mafupi ya kutuomba kura, na baadaye tutatoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge waulize maswali yasiyozidi matatu. Karibu!

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Ahsante Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge. Natumaini wote mnanifahamu, *asalaam aleikhum*! Waheshimiwa Wabunge awali ya yote kwanza napenda niwashukuru sana kwa ridhaa yenu mliyonipa mwaka jana nikaweza kwenda kuwawakilisha katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kazi ambayo nimeifanya kwa ufanisi mkubwa nikishirikiana na Profesa Mwalyosi na Profesa Banyikwa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli mtakavyoelewa ni kwamba tumeifanya ile kazi kwa muda mfupi lakini ni kwamba *Act* ya Chuo Kikuu imebadilika kwamba sasa anatakiwa mwanamke mmoja na wanaume wawili. Kwa hiyo, basi ninaamini kwamba Waheshimiwa Wabunge hasa wa Bunge hili Tukufu mmekuwa na busara sana, na hii imethibitika wakati tunapitisha Miswada hapa Bungeni na ni kwa mantiki hiyo pia mliamua kunipitisha mwaka jana. Ninaamini kabisa mtanipitisha katika kipindi hiki ili niweze kumalizia muda wangu.

Waheshimiwa Wabunge ninawaomba wakati mnapopiga kura mjiulize sisi ambao ni washauri tuna maneno mawili hasa *emphasis* na *sympathy.* Naomba mtumie zaidi *emphasis,* siyo huruma. Kwamba ingekuwa ni wewe umechaguliwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, umeteuliwa juzi inatakiwa ufanye kipindi chako cha miaka mitano, lakini leo mtu anakuambia uondoke, anakustaafisha, hivyo nawaomba, hata Misahafu yetu ya dini inasema umtendee mwenzako kile ambacho wewe ungependa kutendewa.

Kwa hiyo, wakati mnapiga kura mlitambue hilo mjiulize kweli ingekuwa ni mimi sijamaliza kipindi changu cha Uwaziri, Rais akanitoa ningejisikiaje? Kwa hayo machache Mheshimiwa Spika, nakushukuru nawaombeni kura zenu zote mnipe ili niweze kumaliza kipindi changu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Maswali, Mheshimiwa Kajege!

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Hivi karibuni kumetokea mgomo Chuo Kikuu na mgomo huo umekuja baada ya baadhi ya viongozi wako wamekutana na wanafunzi; Je, wewe ulikuwa na *role* gani na wanafunzi katika kuwashauri kuhusiana na mgomo huo?

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, nashukuru kwa swali zuri sana. Naomba ieleweke kwamba Wajumbe wa Baraza la Chuo tulishaondolewa kabla ya mgomo ule, tulishaagwa rasmi tarehe 28 Machi, kwa hiyo kwa njia moja au nyingine hatuhusiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo, sasa itabidi utoke nje. Anabaki? Basi vizuri, tumwite sasa mgombea Mheshimiwa Ruth Msafiri. Karibu sana

Mheshimiwa Msafiri, Wabunge wapo tayari kupiga kura, lakini kwanza utajieleza mbele yao kwa dakika zisizozidi tatu, na baada ya hapo wamepewa fursa ya kuuliza maswali yasiyozidi matatu. Karibu!

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge Mabibi na Mabwana, *asalaam aleykhu!*. Bwana Yesu Asifiwe!

Mheshimiwa Spika, jina langu ninaitwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, tangu mwaka 2000. Nimekuja mbele ya Bunge lako tukufu kuomba mnichague niwe mmoja wa wajumbe wa Baraza jipya la Chuo Kikuu ambalo linaundwa kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya mwaka 70 na sasa linaundwa kwa mujibu wa Sheria mpya ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa na uzoefu wa kipindi kirefu ndani ya masuala ya uongozi na vile vile nimekuwa na uzoefu na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa sababu nilisoma pale digrii ya kwanza, digrii ya pili na hata diploma katika Uzamili wa Sheria na hata wakati Bunge lilipokuwa linamaliza kipindi chake katika kipindi kilichopita, nilipata bahati ya kuchaguliwa mwishoni mwishoni. Lakini yalipotokea mabadiliko kwamba tulianza Bunge jipya sikupata nafasi hiyo tena.

Mheshimiwa Spika, ninao uzoefu wa kutosha na nina hakika kabisa nitawakilisha kwa uaminifu na uadilifu, si rahisi kusahau nilipotoka. Mimi ni Chama Cha Mapinduzi, kwa hiyo, nitawawakilisha kwa uaminifu na uadilifu na kuhakikisha kwamba tunasimamia taratibu za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa heshima na taadhima kubwa naomba kura zenu zote. Ahsanteni sana.

**SPIKA:** *Order please!* Utatatakiwa zaidi uwakilishe Bunge siyo Chama. Kwa hiyo, sasa maswali kama yapo. Hamna maswali Mheshimiwa Ruth. Ahsante sana. Kuna swali?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa mgombea, ni mambo gani ambayo unategemea kuyapa uzito wakati unaliwakilisha Bunge kule Chuo Kikuu?

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Baraza hili ni jipya, tutakapofika kwanza baada ya uteuzi kama nitakuwa mmojawao, tutaletewa miongozo ya mambo gani ambayo tutakuwa tunafuata. Na mimi nitausoma na kuuzingatia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ruth ahsante. Kakae kwenye kiti chako. Naomba Katibu sasa agawe karatasi za kura. Tuonyesheni kwanza masanduku hayana kitu hayo? Waheshimiwa masanduku hayo hayana kitu chochote. Sasa tuyaweke wapi Katibu kwa urahisi wa kupiga kura. Nadhani yakae hapa karibu na rungu.

**NDG. DAMIAN S.L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Lakini Utawala ulichofanya ni kwamba kwanza sasa tutapita kuwa hesabu Waheshimiwa Wabunge ambao wapo ndani.

**SPIKA:** Tutulie ili tupate hesabu ya idadi ya Waheshimiwa

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Utaratibu Mheshimiwa Spika!

**SPIKA:** Utaratibu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu na kanuni za Bunge mtu yeyote ambaye si Mbunge na alipotaka kuingia katika Ukumbi huu lazima tupate kauli za Wabunge na ridhaa ya Bunge hili ili aweze kuingia katika ukumbi huu wa Bunge. Sasa kuna watu ambao si Wabunge ambao si wafanyakazi wa kawaida wa Bunge hili wamo katika Ukumbi huu. Naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Ni yupi huyo unayemwona siyo wa kawaida?

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Nimemwona Zainab hapa anapita? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa watumishi wa Bunge hawaingizwi katika kanuni hiyo. Maana yake wao wanatuhudumia. Kwa hiyo, hakuna mgeni ambaye yuko humu. *(Makofi)*

Wewe Mheshimiwa umemwona Zainab tu basi? *(Makofi/Kicheko)*

Haya Katibu tuendelee! Hesabu za Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa sote tumepata karatasi za kupigia kura? Bado, wakati hesabu zinaendelea vijana mgawe karatasi za kupigia kura. Kuna Waheshimiwa ambao bado hawajapata karatasi? Vijana pale kwa Mheshimiwa Kimaro, Lembeli pote, pale Masoud, hata huku. Walio bado kupata karatasi Waheshimiwa wanyooshe mikono ili vijana waone pale, kwa Mheshimiwa Kendesya, Waheshimiwa wote tumepata karatasi. Namwomba sasa Katibu atangaze idadi ya wapiga kura.

**NDG. DAMIAN S.L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge hesabu ambayo imepatikana ya Waheshimiwa waliomo ndani ingawa kunaonekana kuna watu wengine wanazidi kuingia ni 215.

**SPIKA:** Ahsante sana vijana mkusanye sasa karatasi. Sote tumekwishapiga kura? Bado? Tayari basi mkusanye hizo mstari kwa mstari.Waheshimiwa zote zimekusanywa sasa? Wapi bado wanyooshe mkono ili vijana wawaone. Sasa Waheshimiwa kama ilivyo kawaida kwa uchaguzi wowote pengine wagombea watapenda kuwa mashahidi kabla kura hazijapelekwa *Speaker's Lounge* kwa ajili ya kuhesabiwa. Nitamwita kwanza Mheshimiwa Suzan Lyimo awe na mwakilishi wake.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Halima Mdee anisimamie.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, mimi naiamini Meza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kura zote zimekusanywa? Ahsante sana. Vijana pelekeni sehemu ya kuhesabu. Anayesimamia kuhesabu ni Ndugu Sagasii na Vijana waliopangwa. Zinahesabiwa hapa hapa *Speaker's Lounge* tutapata matokeo kabla ya kusitisha shughuli

za Bunge pale saa 7. Naomba tu niongezee matangazo mafupi tu. Nilipotamka kuhusu mkutano wa Jumapili wa kupokea taarifa za viongozi wa misafara waliokwenda nje ya nchi yetu sikutamka muda, ni saa 5 asubuhi siku hiyo ya Jumapili tarehe 22. Naomba pia mkutano mfupi sana wa Kamati ya Uongozi Ofisini kwangu saa 7.30 mchana huu utafutiatiwa na Mkutano wa Kamati ya Kanuni saa 8 kamili katika Ukumbi ule ule, Ukumbi wa Spika wa Mikutano. Wananikumbusha kweli Mheshimiwa Banyikwa nikupe dakika moja na nusu au ni wakati wa matangazo, kweli ili tuwe na mtiririko na mshindi mwanamke pia aseme wakati huo huo. Ahsante sana kwa kunikumbusha hilo.

**MHE. GIDEON A. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMAT YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(11), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kufanya hivyo naomba kutumia nafasi hii kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu Dr. Aaron Chiduo, kwa Mheshimiwa Bakar Mwapachu na familia yake kwa kufiwa na mama yake mzazi, kwa Mheshimiwa Prof. Msolwa na familia yake, kwa kifo cha ndugu yao na kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopata misiba katika kipindi hiki, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi Amen!

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ambao waliteuliwa mwezi Januari, 2006 ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Kidawa H. Saleh, Mb - M/Mkt.
Mhe. Maida H. Abdallah, Mb - Mjumbe
Mhe. Kheri K. Ameir, Mb - Mjumbe
Mhe. Iddi Azzan, Mb - Mjumbe
Mhe. Mwadini A. Jecha, Mb - Mjumbe
Mhe. Salim H. Khamis, Mb - Mjumbe
Mhe. Castor R. Ligallama, Mb - Mjumbe
Mhe. Joyce Machimu, Mb - Mjumbe
Mhe. Dr.Samson Mpanda, Mb - Mjumbe
Mhe. Fred Mpendazoe, Mb - Mjumbe
Mhe. Manju S. Msambya, Mb- Mjumbe
Mhe. Cynthia H. Ngoye, Mb - Mjumbe
Mhe. Said Nkumba, Mb - Mjumbe
Mhe. Juma S.Omari, Mb - Mjumbe
Mhe. Shally J. Raymond, Mb - Mjumbe
Mhe. Jacob B. Shibiliti, Mb - Mjumbe
Mhe. Martha Umbulla, Mb - Mjumbe
Mhe. Chacha Z. Wangwe, Mb - Mjumbe na mimi Gideon Cheyo ambaye ndiyo Mwenyekiti wa Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Kilimo na Ardhi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia na kujadili Bajeti za Wizara inazozisimamia.

(ii) Kupitia na kujadili Miswada ya Sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(iii) Kupitia na kujadili taarifa za kila mwaka za Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa na Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanywa na Kamati katika kipindi cha Januari - Desemba, 2006, ni:-

Kujadili na kuwasilisha Bungeni maoni ya Kamati kuhusu Bajeti za Wizara inazozisimamia.

Kuchambua Muswada wa Sheria ya Nyama wa mwaka 2006.

Kufanya ziara katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mbeya, Iringa, Tanga, Pwani, Dar es Salaam, pamoja na Morogoro na Dodoma ili kukagua utekelezaji wa miradi katika sekta za maji, kilimo, ardhi na mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Kamati ilipelekewa na kuutafakari Muswada wa Sheria ya Nyama wa mwaka 2006*, (The Meat Industry Bill, 2006)* na kuwasilisha maoni na ushauri wake Bungeni. Hatimaye Bunge lilipitisha Mswada huo na sasa ni Sheria Na. 10 ya Mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilifanya ziara ya kutembelea miradi ya kilimo katika mikoa ya Mbeya na Iringa, Morogoro, Dar es Salaam na Tanga. Kamati ilipata taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali na kuelezwa mafanikio, changamoto na matarajio ya baadaye. Kamati ilitoa ushauri na maoni kila ilipowezekana kama ilivyoelezwa katika aya ya 4.1 ukurasa 5 hadi 12 wa taarifa yetu ambayo imegawiwa. Kuhusu sekta ya Maji, ilifanya ziara ya kutembelea miradi ya maji katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Mwanza na Shinyanga na kupata taarifa za utekelezaji zikionyesha mafanikio changamoto na matarajio ya baadaye. Kamati ilitoa ushauri na maoni kwa lengo la kuboresha utekelezaji kama ilivyoelezwa katika aya ya 4.2, ukurasa wa 12 hadi 14 katika taarifa ya Kamati yetu**.**

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya ardhi, Kamati ilifanya ziara katika mkoa wa Dar es Salaam tu. Kamati ilitembelea mradi wa kupima viwanja 20,000 jijini Dar es Salaam na ujenzi wa nyumba za kuuza za shirika la nyumba la taifa eneo la Boko. Kamati ilipata taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo ikionyesha mafanikio na changamoto. Kamati ilitoa ushauri na maoni kama ilivyoelezwa katika aya ya 4.3 ukurasa wa 14 hadi 16 katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi ya sekta ya mifugo, katika mikoa ya pwani, Dodoma na Tanga. Kamati ilipata taarifa ya utekelezaji

ikionyesha mafanikio na changamoto kadhaa. Kamati ilitoa maoni na ushauri kama ilivyoelezwa katika aya ya 4.4 ukurasa wa 16 hadi 19 katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia ilipitia makadirio ya Wizara ambazo tunazisimamia. Kamati ilipitia mapendekezo ya Makadirio na Mapato ya matumizi ya Wizara za Maji, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maendeleo na Mifugo, na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Maoni ya Kamati hii kuhusu mapendekezo hayo yaliwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ya utangulizi sasa naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka 2006 kama ifuatavyo:-

Maoniya Kamati wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

i. Serikali ifuatilie umiliki halali wa shamba la Tukuyu *Tea Estates* lililotelekezwa na Bwana Shamji, ambalo kwa sasa lipo chini ya uangalizi wa Mohamed *Enterprises Ltd*.

ii. Bodi za mazao ziwe na wataalamu wa kutosha wa kushughulikia mazao yake ikiwa ni pamoja na kuajiri maafisa ugani wa kushughulikia mazao hayo.

iii. Serikali iwasaidie wakulima wadogo wa Tukuyu na wa Dabaga waungane ili wapate nguvu ya kumiliki mashamba ya chai.

iv. Serikali isimamie kwa makini utekelezaji wa mipango mkakati ya kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula hasa sehemu zenye uhaba wa mvua.

v. Mabwawa yachimbwe maeneo yote yanayowezekana ili uvunaji wa maji ya mvua uweze kufanywa na yatumike kwa kilimo cha umwagiliaji.

vi. Maji ya ardhini *(ground water),* yatumiwe ipasavyo hususan kwa kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na tatizo la ukame.

vii. Serikali ihakikishe kuwa mbolea ya ruzuku inasambazwa kwa wakati na mawakala wa usambazaji wawe wale wanaokubalika ili wakulima wapate mbolea kwa wakati muafaka na kwa bei nafuu.

viii. Wafanyabiashara walioruhusiwa na Serikali kuagiza chakula ili kukabiliana na tatizo la njaa watakiwe kuuza kwa bei nafuu kwa wananchi kwa kuwa wamesamehewa kodi. Aidha, vyakula vinavyoagizwa lazima viwe na viwango vilivyokubalika. Hatua kali zichukuliwe kwa wanaokiuka utaratibu.

ix. Uongozi wa soko la Tandale uboreshe mazingira ya soko, barabara, mifereji ya maji taka na kuzoa takataka ili kuepuka magonjwa ya mlipuko

kama vile kipindupindu. Aidha, umeme uwekwe maeneo ya soko na ujenzi holela ukomeshwe ili soko liwe na hadhi ya kitaifa na kimataifa.

x. Serikali iimarishe miundombinu katika maeneo ya Dakawa *Estate*, Turiani na vijiji vya Lukenge, Songambele ili kurahisisha usafirishaji wa miwa kupelekwa viwandani.

xi. Serikali ihamasishe hatua kwa hatua wakulima kulima mazao mbadala badala ya tumbaku. Kabla ya hatua hizo utafiti wa kina ufanyike ili kutoathiri hali za maisha ya wakulima wa Tumbaku. Serikali ihakikishe mikoa inayolima tumbaku inakuwa na mipango madhubuti ya uhifadhi wa mazingira.

Maoni ya Kamati kwa Wizara ya Maji

i. Serikali itafute ufumbuzi wa suala la upatikanaji umeme ili kuweza kufanikisha kwa haraka umalizaji wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama.

ii. Ulinzi wa kutosha uwepo hususan sehemu zilizojengwa matanki ili kudhibiti wizi na uharibifu wa vifaa. Hii ni pamoja na kuwashirikisha wakazi katika eneo la mradi waone mradi ni wao, wauthamini, waulinde na kutunza vifaa.

iii. Suala la upatikanaji wa mabomba ya mradi kwa haraka litafutiwe ufumbuzi ili kufanikisha hatua za kumalizika kwa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyapeleka Shinyanga, na Wilaya ya Kahama.

iv. Serikali ihakikishe kuwa Mifugo inadhibitiwa katika maeneo yote yenye vyanzo muhimu vya maji na maeneo mengine.

v. Serikali itafute ufumbuzi wa kudumu kwa tatizo la maji kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam, na walengwa wawe wakifahamishwa mara kwa mara hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali.

Maoni ya Kamati kwa Wizara ya Mifugo

Serikali iendelee na jitihada za kuwahamasisha watu binafsi kuzalisha malisho ya mifugo ili kutosheleza mahitaji hasa kwa wafugaji wadogo wadogo.
Serikali iendelee na jitihada za kuwapatia wafugaji malambo na miundombinu mingine ili mifugo isipate shida ya maji na malisho na kupunguza tatizo la Wafugaji kuhamahama.

Wafanyabiashara na wakazi wa Dodoma wahamasishwe ili kuona umuhimu wa kuchinjia mifugo yao kwenye machinjio ya kisasa hususan ya Mjini Dodoma.

Serikali iandae utaratibu wa kuwafundisha wauza nyama kwenye mabucha ya mitaani wahifadhi na kukata nyama kitaalamu kupitia chuo cha kukata nyama cha Dodoma.

Serikali isaidie kukuza soko la kuuza malisho ili shamba la malisho Vikuge mkoani Pwani liweze kuuza malisho ya mifugo ndani na nje ya nchi ili shamba liweze kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

Uzalishaji na ubora wa bidhaa za Tanga *Fresh* uongezeke ili kushindana na wazalishaji wengine kutoka nje na ndani ya nchi.

Aidha, Tanga Freshi wapatiwe ardhi ya hekta 500 na kupewa hati- miliki kama kiwanda kilivyoomba kwa ajili ya ufugaji na ujenzi wa kiwanda.

Wizara itenge fedha kwa ajili ya ruzuku ya Madawa ya Mifugo

Serikali iandae na kusimamia kwa makini zoezi la kuhamisha mifugo kwenda kwenye mikoa ya Kusini na Pwani.

Maoni ya Kamati kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

(i) Katika kuunga mkono jitihada za Serikali za kupima viwanja vingi mijini na kubuni miradi ya ujenzi wa nyumba za kuuza, Kamati inahimiza Serikali kuharakisha uanzishwaji wa chombo au utaratibu wa kuwawezesha wananchi walio wengi kupata mikopo kwa mashari nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na ununuzi wa nyumba katika maeneo husika.

(ii) Serikali iangalie uwezekanao wa kuwasaidia wachimba kokoto kupatiwa maeneo mengine nje ya maeneo ya mradi wa nyumba na viwanja au iwasaidie kupata shughuli nyingine ya kuwaletea kipato ambayo ni mbadala na uchimbaji wa kokoto ambao huchangia uharibifu wa mazingira kwa kiwango kikubwa sana.

(iii) Serikali iendelee kuimarisha mbinu za kupambana na vitendo vya rushwa kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

(iv) Viongozi na watendaji wawajibishwe kwa mujibu wa sheria kwa vitendo vinavyokiuka maadili ya uongozi na utendaji.

(v) Wizara ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ziimarishe udhibiti na kuondoa migongano.

(vi) Mamlaka za Serikali zinazohusika na miundombinu, nishati na maji zishirikiane kufikisha huduma zao katika maeneo ya miradi ya upimaji viwanja na ujenzi wa nyumba ili maeneo hayo yafikiwe na kukalika.

(vii) Sheria, kanuni na taratibu za mikopo ya nyumba zizingatiwe ili kuhakikisha kuwa wateja wanalipa madeni yao kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, Bunge lako Tukufu ndicho chombo pekee kilichopewa mamlaka kwa niaba ya wananchi kuisimamia Serikali na namna mojawapo

ya kutekeleza wajibu huo ni kupitia katika Kamati za Bunge, ikiwemo Kamati ya Kilimo na Ardhi.

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi hiki Kamati hii imepata fursa ya kuisimamia Serikali, kwa niaba ya Bunge zima kwa Kuchambua Mswada wa Sheria ya Nyama, kufanya ziara katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Mwanza, Shinyanga, Dar es Salaam Dodoma, Pwani, na Tanga pamoja na kutoa ushauri katika sekta husika.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu na kufanikisha shughuli za Kamati kwa kipindi hiki. Aidha, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha Taarifa ya Kamati kwa 2006. Pia napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati yangu katika kipindi hiki chote. Aidha, nampongeza Katibu wa Bunge na Katibu wa Kamati hii ndugu Frank K. Mbumi, maafisa mbalimbali wa Wizara, Idara na Mashirika ya Umma, Bodi za mazao ya biashara na Wadau waliosaidia Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika**,** naomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja. (*Makofi*)

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuongea machache kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi. Kilimo kipo nyuma, mgongoni kama kinavyoitwa uti wa mgongo. Mgongo una matatizo makubwa, hata kama unawashwa mgongoni kujikuna inakuwa tabu, ndivyo kilimo ambavyo kimewekwa mgongoni, wakulima wa Tanzania wana tabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitaka kutafuta fukara wa mwisho katika nchi hii anatoka kwa wakulima, mkulima akiugua hana *E.D.* Mkulima akizeeka kama ninavyoelekea, hana pensheni, mkulima hana upendeleo wa aina yoyote. Hata anapopanda kwenye basi, kama basi limejaa yeye ndiye anayeshindiliwa na ngumi "sogea!" Mkulima katika nchi yetu ana matatizo, lakini kwanini mkulima awe na matatizo wakati kwa kweli ni mtu muhimu, ni mtu muhimu kwa sababu ndiye anayetoa chakula tunachokula. Bila mkulima kwa kweli nadhani hatuwezi kuishi, si hivyo tu, mkulima pamoja na kuwa mnyonge, ni wakulima wachache wanaokula mara mbili, wengi wanakula mara moja, lakini mkulima pia ndiye anayekabiliwa na kazi kubwa ya kujenga taifa hili.

Nenda vijijini tunapokuwa tunafanya kazi ya kujitolea, ambayo kwenye Katiba yetu inasema kwamba hata kama ni shuruti, ilimradi ni ya kujenga nchi isiitwe ya shuruti, lakini ndiyo wanaobeba mawe kichwani ya kujenga shule, kujenga zahanati, ndiyo wanaobeba mchanga kichwani, ndiyo wanaofanya kila aina ya kujenga taifa hili, wakati huo nguvu hawana, kwa sababu ya lishe.

Mheshimiwa Spika, kwa nini hawa wawe na hali ya namna hiyo, wamesahaulika? Mfanyakazi kila siku anaomba mshahara uongezwe marupurupu, lakini mkulima hata mbolea ni hadithi. Naambiwa watapata mbolea lakini mpaka leo kilimo kimekwisha hakuna mbolea iliyokwisha kwenda, madawa kwa mazao yao, hayapatikani.

Mkulima anasaidia sana pesa za kigeni katika nchi hii, ukiangalia pamba tumbaku hii inayopigwa vita, kahawa, korosho, katani yote hayo anayalima kwa jasho lake, hapewi hata mundu wala jembe. Lakini pesa ya kigeni inayopatikana kwa mazao hayo, huyo mkulima hapati wala haioni, lakini hasaidiwi.

Mheshimiwa Spika, mkulima amebaki anadanganywa danganywa tu, na wakati mwingine anababaishwa. Leo hii sera ya nchi yetu ni umwagiliaji lakini sisi tuna umwagiliaji wa jadi, tuna mabonde yanayoitwa matingatinga, huyu mkulima anababaishwa kwamba ni vyanzo vya maji, hawezi akaambiwa bwana kwamba chanzo cha maji, na haya ni mapitio ya maji. Hakuna sheria inayomwonyesha mkulima kwamba maji chanzo ni hapa maji yanapotokea, ikitokea tu bonde lina maji basi anaambiwa bonde hilo asiguse ni vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kujua hivi maji yanafumuka hata kila mahali, haya maji yanatoroka yametoka kwenye chanzo yanatoroka hata kuyatenga tu, tukayatumia shambani tunaambiwa hapana, acha yaende, mkulima anababaishwa. Siku moja tukiwa tunasoma, kuna wanafunzi wa chuo walisema: Heri ya mkoloni!" wengine wakafukuzwa, mpaka wakaomba radhi na kuambiwa wajute wapige magoti. Sasa mimi naweza nikasema, hebu angalieni yale malambo ambayo yamechimbwa na mkoloni, mkoloni ambaye si ndugu, si shangazi yetu hatuna ujamaa naye, akatuchimbia malambo, leo hii hayo yamefutika, mchanga umejaa *acid*, yamekwisha!

Mheshimiwa Spika, halafu inasikitisha, huko Zanzibar kulikuwa na hoteli nzuri tu Bwawani, kulikuwa na Bwawa zuri, juzi nimekwenda nikakuta lile bwawa limefutika, limekuwa pori. Huyu katutengenezea kusaidia wakulima waweze kumwagilia, waweze kunywesha mifugo yao, lakini Watanzania sisi ndugu zake na huyu mkulima tumeacha vitu vyake vimeharibika.

Sasa tunasema: "tunafufua kilimo cha umwagiliaji", kwa vipi? Nimejaribu kupita hapa Dodoma, nawaambia Wagogo, Mwenyezi Mungu aliwanyima maji ya juu, akawapa maji ya chini, ukifukua kidogo maji hapa Dodoma yapo, lakini hawayatumii, wangechimbiwa visima hapa wangefanya kilimo cha kumwangilia. Nguvu yao inapotea, nguvu za Watanzania. Ndugu zangu sisi Mwenyezi Mungu tunampa kazi nzito, tunamwambia tulinde lakini bado tunamwambia hata mvua atuletee, wakati katuwekea maji chini na mengine yako juu. Sasa hawa Wagogo wana maji ya chini nani awasaidie kuyatumia.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kuona kwamba nchi yetu ni maskini wakati ardhi ni mali, lakini pamoja na kwamba ardhi ni mali, ni mali ya nani? Angalieni Katiba, inasema ardhi ni mali ya umma, hivi mimi nimemiliki ardhi, nianze kuiendeleza kwa gharama kubwa kubwa wakati ni mali ya umma, umma maana yake nini? Ni kwamba yeyote anayeweza akataka kutumia hiyo anaruhusiwa na Serikali. Leo hii

dhahabu ikitoka kwenye shamba la Kabuye, nadhani hata mikataba ya kupanga wachimbe kwenye shamba langu sitaambulia.

Lazima tuangalie hawa wenye nchi, nchi yao mali ya nani? Kipaumbele, mkulima hana, tangu wapime vijiji hata robo ya vijiji vya Tanzania haijaisha. Kwa sababu tunaona si jambo la lazima, lakini tungepimiwa tukapata milikiinayoeleweka, sio hii ya kudanganya danganya kwamba kijiji kinatoa miliki, kwa miaka mingapi? Tufanye vitu vya kumsaidia mkulima iwe ni mali yake naye aweze kuitumia kupata mkopo, na tumsaidie kuiendeleza. Mali ya mkulima mara nyingi haiangaliwi.

Mheshimiwa Spika, jana na leo kuna kumpongeza Mtukufu Rais, kwa sababu ya kuita Serikali ijadili taarifa, lakini vyama vya wakulima vimepotea, vimefilisika na vingine vimedhohofika, Rais ameita nani, kuuliza kwanini SHIRECU imekufa, Rais ameita nani kuuliza kwanini NYANZA imekufa? Rais ameita nani kuuliza vyama vyote vikubwa?

Hivi kitu kinapotea tu si kuna mtu ameingiza mkono, kinapotea tu vyama vyote nchini vimefutika, mkulima amebaki hivi hivi, hakuna waliokula hizo pesa wakaulizwa? Hakuna waliokuwa viongozi lakini leo kwa kuwa pesa ya Serikali, Mtukufu Rais ameacha kazi zote, na Serikali yote imekaa pale kujadili lakini mali ya mkulima imeteketea hakuna anayeulizwa, watu wamejenga majumba, watu wamefurahia mkulima anateketea, hakuna anayeuliza, lakini bayana zaidi, mkulima ameachwa, hata kile anachobahatisha kupata, bei mbaya.

Samahani, Mheshimiwa Spika, leo nasema Wagogo ni kwa sababu nipo hapa, wameivisha karanga nyingi, lakini wataishiwa kulanguliwa. Hakuna mpango kwamba jamani, tufanyeje? Kuna nchi jirani na ndani ya nchi ambao hawana karanga, hao wangefanyiwa mpango wakatafutiwa masoko, hao wakulima wangefaidika, sisi huko maharange Karagwe, Biharamulo, hayana mpango, mtu tu mlanguzi anakuja analangua, hebu uwe mlanguzi unapeleka wapi? Na kwanini watu tusiwasaidie kule wanakopeleka walanguzi, wakulima wetu wakapeleka wakapata bei nzuri lakini nani anayewahangaikia.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kabisa kuwa Serikali inaelewa kabisa wakulima ni hoi ndiyo maana wakasema hata karo ya shule zao za msingi hawawezi wakasamehewa, kodi hawawezi wakasamehewa, sekondari *school* zikapunguka sana sana. Lakini shule ya msingi mtoto wa mkulima hana hela, sekondari *school,* mtoto wa mkulima hana lakini akishakwenda Chuo Kikuu anaambiwa ana hela achangie asilimia 40 ambayo ni sawasawa na laki tano shilingi 500,000/=. Mtu aliyeshindwa shilingi 40,000/= za sekondari akishaingiza mtoto Chuo Kikuu basi ametarajika, sijui anauza hiyo sielewi!

Mheshimiwa Spika, naomba muone kwamba sisi ni fukara mahali popote, lakini tusaidiwe kuondokana na huo ufakara miaka hamsini, wewe unasema tutaondoa umaskini, miaka mingapi unataka? Basi tuinue mikono kwamba ufukara umetushinda, miaka hamsini tunajitawala, sisi wenyewe tunawala shangazi zetu, watoto wetu lakini hakuna kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukiona mtendaji wa kijiji na kata amekuja kwako, kama upo kwenye ua usitoke! Hana nia nzuri! Haji kukuuliza mbona huna chakula? Mbona nyumba imebomoka? Mbona pa kuanika vyombo huna? Hapana! Anatafuta mchango. Kaa huko huko aende, uwaambie watoto wamwambie sipo, kikombe kipite. *(Kicheko)*

Sasa watu wetu haujakwenda kuwauliza kwa nini ardhi imekuwa hivi? Wewe unakuwa Mbunge, Diwani, Rais kipindi kikiisha unamshukuru Mwenyezi Mungu, unakwenda, yule mkulima unamwacha vile vile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawaombeni sana, Taifa letu limuangalie mkulima kwani ana hali mbaya na nyie mnaogopa. Leo hii mtu akimaliza Ubunge haendi kulima, utamsikia anafanya biashara. Nenda kaonje joto ya jiwe ukaone! Hatuendi huko ndio maana hatuwasaidii wakulima kwa sababu *we dont belong to them,* ndio maana hatu-*feel* hilo joto la jiwe wanalopata.

Mheshimiwa Spika, ninawaombeni sana, hawa wakulima tuwasaidie kwani ni ndugu zetu, ni watoto wetu, kwa kweli tukivaa njuga, hili Taifa letu linaweza likaondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema hayo tu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi.

Kwanza, napenda nimpongeza Mwenyekiti, niimpongeze Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa kazi nzuri na taarifa na ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze na hii sekta ya maji na ninapenda ndugu zangu wamwelewe Mheshimiwa Phares Kabuye kwamba hawasemi Wagogo isipokuwa anawatetea waweze kupata huduma ya maji. Siyo kwamba alikuwa anawasema, isipokuwa tuna tatizo kubwa sana la maji katika Mkoa wetu wa Dodoma. Napenda niishukuru Serikali, na Shirika la Msaada la Uingereza *(British Water Aid)* na Benki ya Dunia, ndio wanaofanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba tunapata huduma ya maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai, maji ni maendeleo na maji ndio uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu miradi ya maji katika maeneo yetu, nianze na mradi wa maji wa kuboresha huduma ya maji katika miji tisa ambayo sasa imebaki mitano katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni wa muda mrefu, *feasibility study* ilishafanyika, Mji wa Mpwapwa una matatizo makubwa sana ya maji. Hivi sasa tulikuwa tunatarajia utekelezaji ungeanza, tumeeleza kwamba wanataka kufanya *feasibility study* kwa ajili ya kuanza kutekeleza huo mradi wa maji katika Mji wa Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, maji ni uhai, Mji wa Mpwapwa ni mji wa siku nyingi tangu mwaka 1905 na wakati huo Wananchi walikuwa ni wachache, yaani

wakazi walikuwa ni wachache katika mji huo na huduma ya maji vyanzo walivyokuwa wanategemea ni vile vile. Chanzo cha maji cha Mayawile ambayo ni maji ya mtitiriko, visima viwili viko pale Kikombo, kwa hiyo, maji hayo hayatoshi, huduma ya maji katika Mji wa Mpwapwa hivi sasa ni tatizo kubwa sana na akina mama wanapata shida sana ya maji hasa katika maeneo ya Vihawe, Mpwapwa Mjini pamoja vitongoji vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda niishukuru sana Serikali kwamba wamejitahidi angalau sasa Wilaya ya Mpwapwa tunapata maji zaidi ya asilimia 70. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji au Naibu Waziri wa Maji atembelee Mji wa Mpwapwa na kuona jinsi Wananchi wanavyopata shida ya maji.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu sekta ya mifugo. Nchi yetu ina ng'ombe zaidi ya milioni 18 na mifugo hii inaipatia mapato Taifa letu na tuna vituo vya utafiti wa mifugo katika nchi yetu ikiwemo Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Mapwapwa.

Hivi sasa tumekumbwa na tatizo hili la ugonjwa wa *Rift Valley Fever* na ugonjwa huu unaweza ukazuilika kama Wananchi tutafuata masharti ya wataalam wa afya na tumeweka kwenye kundi la *Communicable Disease.* Kwa hiyo, *Communicable Dieses* ni ugonjwa unaoweza kuwa *transmitted* kutoka kwa mnyama na kwenda kwa binadamu, lakini ugonjwa huu unaweza ukazuilika kwa chanjo pamoja na tiba.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri mambo yafuatayo: kwanza tuna machinjio ya kisasa hapa Dodoma ambayo ni *slaughter house.* Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba, ni vizuri wananchi wazingatie masharti ili kujikinga na ugonjwa huu, wasichinje mifugo ovyo katika maeneo yao na hata machinjio ambayo yamethibitishwa na Serikali kwamba yametimiza masharti ya afya, lazima zile *procedure* zote za *meat inspection* zifanyike, ile *postmortem inspection* kwamba tuhakikishe mnyama asichinjwe siku hiyo hiyo, lazima apelekwe kwenye machinjio alale pale kusudi waweze kuona kama ana dalili ya ugonjwa halafu siku ya pili ndio wanamchinja na kufanya *postmortem inspection* ili kuhakikisha kwamba mnyama huyo haleti madhara kwa walaji.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunaambiwa tuchemshe nyama, ni kweli na tuchemshe maziwa sana ili kusudi kuuwa wale *virus* kwa sababu *it's a viral dieses.* Kwa hiyo tukichemsha sana nyama na tukichemsha maziwa tunaweza tukazuia. Chanjo ni muhimu sana kwa sababu katika suala zima la kupambana na ugonjwa huu kwanza tuna tiba na chanjo, lakini haturidhiki na idadi au *doze* za madawa ambayo yanaagizwa, ni kidogo sana kulingana na mifugo tuliyonayo. Hivi karibuni Mpwapwa tulipata *doze* 16,000 sasa *doze* 16,000 na sisi tuna zaidi ya mifugo 300,000 na ng'ombe karibu 5,000 ndio waliochanjwa, lakini idadi kubwa ya ng'ombe bado hawajachanjwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naishauri Serikali kwamba iweke mikakati, tuagize madawa ya kutosha kwa ajili ya chanjo ya mifugo, tusielimishe wananchi kwamba sasa mchemshe nyama sana, mchemshe maziwa, lakini kwa kweli ni vizuri tuhakikishe kwamba fedha zinatengwa za kutosha za kununua madawa ili tuweze kuchanja mifugo wote na kuzuia ugonjwa huo ambao ni hatari na kwa kweli unapoteza maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili la kula nyama, nakumbuka Mheshimiwa mmoja hapa alizungumza kwamba, ukitaka kula nyama kwanza nenda hospitali

ukawaone wagonjwa na ukirudi utaamua wewe mwenyewe ule au usile, lakini lazima tuchemshe ili tuweze kuuwa wale *virus* ambao wanaleta ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Kamati zetu zinafanya kazi nzuri, Kamati zote za Bunge zinafanya ziara katika Mikoa, lakini tatizo letu kubwa ni ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, nilikuwa naomba katika bajeti ijayo Kamati zipate fedha ya kutosha ili tuweze kutembelea miradi. Tunapotembelea miradi katika Mikoa, tunajifunza mambo mengi sana. Badala ya kujadili na kusomewa taarifa na Waheshimiwa Mawaziri lakini tunapoona miradi *physically,* kwa kweli tunajifunza mambo mengi na tunaweza kuishauri Serikali vizuri zaidi kuliko kusomewa taarifa tu kwamba visima vingapi vya maji vimechimbwa, mifugo mingapi imechanjwa na imepata tiba.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba, katika bajeti ijayo Kamati za Kudumu za Bunge zipate fedha za kutosha ili tuweze kutembelea miradi katika Mikoa na hii inasaidia tunapofika katika mikoa tunatia msukumo kusudi miradi hiyo iweze kutekelezwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kuchimba malambo ni muhimu katika maeneo yote ambayo kuna ukame kwa sababu kuna maeneo mengine kuna ukame na hakuna uwezekano wa kuchimba kisima kirefu, kwa hiyo, bwawa *holes* au visima vifupi, vitasaidia sana kwa kuwa hakuna maji ya mtitiriko.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba ni vizuri sasa na wakati umefika maeneo hayo ambayo ni makame tuchimbiwe mabwawa ambayo yatasaidia sana wananchi kupata huduma ya maji pamoja na mifugo yao. Lakini madawa ya kusafishia maji ni muhimu sana, hivi sasa kuna baadhi ya maeneo wanachimba visima ambavyo tunaita *unprotected holes,* sasa maji kama yale ni hatari sana hasa kwa magonjwa kama ya homa za matumbo.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kipindupindu hauwezi kutoka nchi hii kwa sababu sasa ni *endemic.* Ni ugonjwa ambao upo siku zote kwa sababu wananchi hawazingatii masharti.

Kuna taratibu za kusafisha maji tunaita *water treatment and process,* kwa mfano unapochimba kisima cha maji au maji ya *gravity scheme* lazima yasafishwe, lazima *process* ya *treatment* ifanyike, kuna suala la *segmentation* lazima lifanyike, *storage, filtration* lazima ifanyike. Lakini sasa hivi wananchi wanachimba visima wanachota maji wanakunywa . Ni hatari sana kwa kupata magonjwa haya hasa homa ya matumbo na kipindupindu.

Mheshimiwa Spika, magonjwa haya hayataisha kama hatutazingatia na tunaiomba Wizara inayohusika lazima tupate madawa ya kutosha kwa ajili ya kusafishia maji kwa sababu maji yanasaidia sana binadamu, kilimo, lakini maji kama yanachafuliwa na vijidudu ile *water contamination* inaweza kuleta *water bone dieses* kwa mfano magonjwa haya ya kuharisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba sekta inayohusika na maji itusaidie tupate madawa ya kutosha ili tusafishe haya maji yawe salama na wananchi waweze kuyatumia na kuhakikisha kwamba hayaleti magonjwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi na huo ndio mchango wangu na ninaunga mkono taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwamba kweli kazi imefanyika na wamefanya ziara lakini nasisitiza suala la Kamati zetu za kudumu zipate fedha za kutosha ili tuweze kutembelea miradi hii.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie.

Kwanza nianze kwa kuipongeza sana Kamati hii ya Kilimo kwani imefanya kazi kubwa sana, imetembelea maeneo mengi na kwa kweli imetuletea mambo ambayo Serikali sasa ni lazima iyachukulie hatua. Wamekwenda kwa wakulima wa chai, wamekwenda kwa wafugaji, wamekwenda kwenye upimaji wa ardhi, nami nirudie kuwapongeza na niunge mkono hoja hii moja kwa moja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitakuwa na machache ya kuzungumzia. Kwanza nikianza na kilimo, wenzangu wameshasema wote wawili waliozungumza mbele yangu, wamegusia juu ya kilimo cha hapa kwetu Tanzania, bado tuna matatizo makubwa sana. Wakulima wetu bado wamesahauliwa, Serikali sasa hivi ni lazima ilete mapinduzi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna wakulima wetu bado wanalima kwa jembe la mkono na hii nimejifunza sana nilipokuwa na Kamati yetu ya *LAAC* tulipotembelea Wilaya mbalimbali. Kwa kweli Serikali ni lazima ilete mapinduzi kwa wale ambao bado wanatumia jembe la mkono, walete majembe ya kukokotwa na wanyama kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifika Mkoa wa Ruvuma - Jimbo la Peramiho kule bado wakulima wanatumia jembe la mkono. Sasa hivi tuko kwenye Dunia ya Maendeleo, lakini wananchi bado wanatumia jembe la mkono na ni maeneo mengi, sio Peromiho tu, lakini kwa sababu nilikwenda Peramiho naomba niseme kwamba Serikali ni lazima ijitahidi kuwapelekea wananchi wa Peramiho, Namtumbo na maeneo mengine majembe ya kukokotwa na wanyama kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale kuna kituo cha kufundishia wanyama kazi, nami naomba Serikali isaidie, uongozi wa Peramiho na Mbunge wao wanataka kuja kutembelea Iramba ambapo sisi kwa kilimo cha wanyama kazi tupo zaidi ya asilimia 85. Lakini kwa nini wasipelekewe hizi nyenzo kule waanze kuzitumia? Ninaikumbusha Serikali kwamba iwasaidie wakulima wote ambao bado hawajafikia hata ngazi ya kutumia wanyama kazi waweze kuendelea na kwa maeneo mengine niseme kwamba Serikali ni lazima ianzishe utaratibu mpya, itafute fedha ya kutafuta matrekta madogo madogo ambayo wakulima wetu wanaweza kuyatumia kuleta maendeleo kwenye kilimo chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna fedha ambazo zimetolewa na Rais wetu, mimi napongeza sana. Sasa hizi fedha ndio zingetumia matrekta madogo madogo, yangesogezwa kila Wilaya ili wananchi wetu waweze kununua. Kwa kweli bila kufanya hivyo, tutaendelea kupata taabu na wakulima wetu wataendelea kutunyooshea vidole kwamba hatuwasaidii. Sasa hivi bajeti haijapangwa na mimi naomba hili jambo la kuwaendeleza wakulima wadogo wadogo kwa kupeleka matrekta madogo madogo

ambayo wanaweza kununua kwa fedha zao na fedha ambazo Rais ametoa wakopeshwe liwekwe na lipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na mvua kubwa mwaka huu. Hizi mvua zimeharibu *scheme* nyingi za umwagiliaji, zilikuwepo *scheme* za Mwangeza, Msingi ambazo ziko Iramba Mashariki na anajua na kwingine kote zipo. Sasa kwa sababu hizi *scheme* zilikuwa zinafanya kazi na sasa hivi zimeharibiwa na mvua, tunaomba bajeti ijayo zitengewe fedha ili zifufuliwe, wananchi wetu waendelee kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, nilipata bahati ya kutembelea Mkoa wa Tabora na nilitembelea Wilaya karibu zote, lakini tatizo hili nililikuta zaidi katika Wilaya ya Urambo na Skonge juu ya wakulima wa tumbaku. Sasa hivi wale matajiri wanaonunua tumbaku ndio wanaowakopesha wakulima. Kwa hiyo, mkulima nusu ya mapato yake yanaishia kulipa mazao kwa matajiri wanaowakopesha. Mimi ningeshauri Serikali kwamba kwa sababu Skonge kuna Benki, Nzega kuna Benki, Urambo kuna Benki hii ni mikopo, ipite Benki na kama siyo Benki, basi ipite kwenye *SACCOS* ambazo kote zipo na ni nchi nzima ziko kwa kweli tutakuwa tumewasaidia wakulima wetu wa tumbaku. Mimi nimekuta kazi wanawafanyia matajiri wanaonunua. Kwa hiyo, naomba sana hili lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, juzi tulikuwa na wenzangu wa *CRDB,* walituletea semina hapa na wakatueleza na wakasema jinsi ya kupata mikopo kutoka kwao, lakini kitu ambacho nilikishikilia zaidi ni kwamba wao wanasema kazi ya kufundisha hizi *SACCOS* ili ziweze kupata mikopo ni kazi ya Serikali. Sasa ninaishauri Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa mwaka unaokuja ili Wilaya zetu kwa kutumia Maafisa Ushirika waweze kutoa elimu kwa *SACCOS* zetu iwe rahisi kupata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo juu ya upande wa mifugo. Kwanza, niipongeze sana Serikali kwa kujenga machinjio ya kisasa hapa Dodoma. Lakini ukienda mazizini Ukonga Dar es Salaam kwa kweli hutatamani kula nyama inayochinjwa kule. Pale mahali ni pachafu, wanyama wanapata mateso badala ya kuchinjwa na kwa kweli inawezekana kabisa kwamba mara nyingine wananchi wetu wanalishwa vibudu.

Mheshimiwa Spika, mimi na Kamati yangu tulitembelea kule na tulikuta mnyama aliyekufa pale machinjioni na wanyama wanateremka wanarusha kutoka kwenye *lorry* kwenda chini, kwa kweli ni mateso makubwa. Ninaomba hii Kamati ya Kilimo na Ardhi itembelee hayo machinjio mapema iwezekanavyo na tunaomba machinjio haya ya kisasa yajengwe maeneo mengi hapa kwetu Tanzania kwani wote tunataka kula nyama safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nikirudi upande wa wafugaji wetu, bado tuna matatizo na dawa, bado tuna matatizo na majosho, bado wafugaji wetu wana matatizo makubwa sana, tuwasaidie, tuwape elimu ya kutosha. Nina imani kabisa tukishawapa elimu ya kutosha, hata hili tatizo la kuhamahama halitakuwepo, litatoweka. Sasa hivi wafugaji wetu wengi wamehamia Lindi na kule matayarisho hayakufanywa ya kutosha. Naomba sana Serikali iwathamini wafugaji wetu kwa sababu wao wana haki ya kuishi Tanzania kama watu wengine na wana haki ya kupata huduma ili waongeze kipato cha Taifa. Kwa hiyo, nawaomba sana wafugaji wote hapa nchini wakiwepo wa Iramba Mashariki wasaidiwe ili ufugaji wao uwe mzuri.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa bei ya mazao. Sasa hivi karibu wananchi wataanza kuvuna na kipindi kilichopita tumeona wakulima wetu wa korosho walivyoteseka korosho yao haikupata bei nzuri, korosho yao nyingine bado ipo kwenye majumba, sisi tunaomba Serikali inapoamua kitu iamue. Kwani mwanzo Serikali ilipanga bei ya korosho, baadaye ikalegalega lakini tunashukuru ikarudi na msimamo ule.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida Wilaya zote tunalima alizeti na sasa hivi msimu wa alizeti unakuja na sasa hivi walanguzi wameshaanza. Serikali tunaomba mtuhurumie sisi wakulima, tuwahurumie hawa wakulima wetu. Soko huria ni zuri pale ambapo vyama vyetu vya ushirika vilikuwa bado vinafanya kazi, lakini sasa hivi kwa kweli wakulima wetu wanapata taabu sana, wakulima wote wa mazao hasa haya mazao ambayo hayana Bodi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iingilie na iliahidi kujenga masoko ya kisasa; iliahidi kujenga soko pale Iguguno la kisasa lakini mpaka sasa sijaona ikoje na mimi naomba wakati wakifanya majumuisho nisikie juu ya hilo soko.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, lakini tuwakumbuke wakulima wetu na wafugaji wetu wa Tanzania. Narudia kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Kamati ya Kilimo na Ardhi. Kwanza, nianze kwa kuzipa pole familia zote zilizopoteza jamaa zao hivi karibuni, Mungu azilaze roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru wewe mwenyewe kwa kuiwezesha Kamati yetu ya Kilimo na Ardhi kutembelea mikoa mbalimbali. Kwa jumla tumetembelea mikoa sita tukianzia Morogoro, Iringa, Mbeya, Mwanza, Shinyanga na Tanga. Tumejifunza mengi, tumeona matatizo mengi na tumekuja na mapendekezo kwa Serikali ili iyafanyie kazi na tuna imani kwamba ziara yetu hiyo na gharama hizo zilizopotea hazitapotea bure ila mapendekezo yetu yatatiliwa umuhimu na kufanyiwa kazi. Lakini vile vile nataka niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu wa Wizara zote nne ambazo tunashirikiana nazo Wizara ya Kilimo, Wziara ya Mifugo, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maji kwa ushirikiano wao mzuri kwa sababu kule ambako tulikwenda au tulikuwa na Waziri mwenyewe, au Naibu Waziri, au Katibu Mkuu au wawili katika hao. Kwa hiyo, ilifanya ziara yetu kuwa na uzito mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ni *reflection* ya mwaka 2006, kwa hiyo, ni mambo ambayo pengine yakiongelewa sasa hivi yataonekana yamepitwa na wakati, lakini kwa bahati mbaya kabisa mambo ambayo tumeya-*record* katika mwaka 2006 kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe jana katika *briefying* inaonesha kwamba hakujakuwa na maendeleo makubwa zaidi ambayo tumeyaona.

Kwa hiyo, mimi napata wasiwasi katika mchakato huu wa kufanya mapinduzi ya kilimo na mpango huu madhubuti wa *ASDP* kuwa utafanikiwa kama ulivyokusudiwa.

Hata hivyo, muda upo, huu ni mwezi wa Nne, labda katika miezi iliyobaki tunaweza kuona mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, katika Wizara zote nne kuna tatizo moja ambalo ningependa kulizungumzia, nalo ni tatizo la uajiri wa wafanyakazi wa Wizara hizo katika TAMISEMI, kuna lugha ya pamoja ambayo wafanyakazi wa Wizara hizo ambazo wako chini ya TAMISEMI wamekuwa hawana uwezo nao wa kuwadhibiti kwa maana ya kwamba hawana meno hata ya plastiki. Nafikiri hapa kuna tatizo la sera, au la kiutendaji vyovyote itakavyokuwa, lakini hapa kuna tatizo. Kwa kwa sababu Wizara zote inaongelewa suala hilo hilo. Naomba Serikali iangalie: Je, ufanisi wake ukoje kwa kila Wizara? Inasema kwamba wafanyakazi wa TAMISEMI uwajibikiaji wao siyo mzuri na kwa sababu wao hawana uwezo wa kuwashughulikia, hali inabaki hivyo hivyo. Sasa itabaki hivyo hivyo mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba imejitokeza kuwa kuna baadhi ya mambo ambayo yanaweza kufanywa kwa ushirikiano kati ya Wizara mbili au tatu, lakini kinachoonekana ni kwamba kila Wizara inafanya peke yake. Sasa kuna maeneo ya ushirikiano, nafikiri sio vibaya nikatoa mfano mmoja tu. Kwa mfano, katika ujenzi wa mabwawa, Wizara ya Kilimo inahitaji maji, Wizara ya Mifugo inahitaji maji, kwa hiyo kama kungekuwa na ushiriano katika baadhi ya maeneo, nafikiri tungeweza kuokoa fedha nyingi za wananchi walipa kodi. Kwa hiyo, nafikiri kuna haja Wizara husika kukaa pamoja kuangalia ni katika maeneo gani wanaweza kufanya miradi yao ya pamoja ili kunusuru fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii michango yangu na mapendekezo yangu nimeyatoa katika Kamati nitakuwa na machache tu ya kugusia gusia yale ambayo labda hayakujitokeza vizuri katika maelezo yetu.

Mheshimiwa Spika, matatizo ambayo Mheshimiwa Waziri jana aliyaeleza kwa mfano matatizo ya ugani, mbolea, mbegu na madawa ndiyo yaleyale ambayo sisi tuliyakuta na tukatoa mapendekezo yafanyiwe kazi lakini ndiyo kana nilivyosema kwa bahati mbaya hadi sasa kwa maelezo ya Waziri hadi hapo jana ni kwambo bado imebaki kuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tumeona kwamba Maafisa Ugani hawapo ni wachache lakini vilevile hawafikishi ile taaluma ya kilimo kwa wakulima husika kwa hiyo hata hao wachache waliopo *efficiency* yao haijaonekana vizuri. Lakini kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba tunategemea labda katika kipindi kijacho suala la Ugani linafanyiwa kazi na litarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, tumekuta vilevile watu wamepanda lakini mbolea haijafika bado na mbolea imefika tayari watu wameshapanda. Lakini kuna wengi wanaolalamika juu ya kukosa mbolea hii ya ruzuku, nafikiri hili vilevile limeelezwa vizuri na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atalifanyia kazi kama alivyoahidi na madawa ni hivyohivyo kwamba madawa hayapatikani, madawa hayana ruzuku na wakulima wanalima bila madawa.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni tatizo la soko ambalo nasi vilevile tumeliainisha katika *report* yetu na inasema kwamba hili ni tatizo kwa kweli ni kubwa

kwa sababu linawaongezea wakulima umaskini badala ya kuwaondolea umaskini. Kilimo bila soko maana yake ni kuongeza umaskini kwa wakulima. Kwa hiyo dhana ya MKUKUTA hapa itakuwa haifanyi kazi ikiwa Wizara husika hazikajakaa kitako na kutatua tatizo la masoko kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo cha mkataba, kilimo hiki ni kizuri kwa sababu kina soko la uhakika, lakini uzwa yake ni kwamba matatizo haya ya kufanya *cartel* kwa makampuni ya kununua mazao ya wakulima yanawanyonya wakulima wetu na lazima suala hili liangaliwe vizuri. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri jana kwamba wanatumia Vyama vya Ushirika kuondoa hiyo *problem,* lakini sijui ushirika wenyewe naona bado haujakuwa wa kutegemea.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie habari ya Viwanda vya Sukari. Tanzania tumebahatika kuwa na viwanda vikubwa vya sukari vitatu na bila shaka uzalishaji wa sukari kwa nchi yetu ni mkubwa sana. Nataka niseme kwamba viwanda vya sukari vina utajiri mkubwa kwa nchi yetu kwa sababu muwa kama *raw material* ya sukari, una matumizi ya asilimia 100. Majani yake ni lishe kwa mifugo, makapi yanatumiwa na baadhi ya nchi kutengeneza fenicha, lakini vilevile kuna *molasses* ambayo viwanda vyetu vingi huwa inamwagwa bure katika barabara na chache ndiyo inauzwa. Hii inaweza kutengenezwa *ethanol* baada ya kujengwa *Plant* au kiwanda.

Mifano mingi ipo, kwani kuna nchi kama Brazil wana kiwanda kikubwa cha *ethanol* ambacho kinasaidia katika kuendesha magari yao. Lakini vilevile sukari ambayo ni zao kubwa ambalo ndiyo *main product* bado inaonesha kwamba kuna upungufu kidogo wa sukari kwa sababu kuna uagizwaji wa sukari kutoka nje ya nchi. Kwa hiyo, kuna haja ya kutilia mkazo vilevile kulitosheleza zao la sukari.

Mheshimiwa Spika, katika miwa, ningependa kuzungumzia suala moja la msingi la uzalishaji wa umeme. Viwanda vya sukari huwa vinajitosheleza kwa umeme, vinazalisha umeme wa kutosha kwa ajili ya matumizi yao, lakini vilevile vina uwezo wa kuuza baadhi ya umeme ambao wanauzalisha kwa Taifa na hili tumeliona tulipotembelea Kilombero. Wao walikuwa tayari kuuza zaida kwenye *Grid* ya Taifa. Nafikiri suala hili likishughulikiwa, linaweza kulipunguzia Taifa letu mzigo mkubwa wa suala la umeme ambao sasa hivi limekuwa ni zito kitaifa kwa sababu viwanda ni vingi. Tuna Kilombero, Mtibwa na Kagera. Nafikiri tafiti zikifanywa, suala la umeme linaweza likatatuliwa kidogo kwa kupitia Viwanda vya Sukari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la mkonge. Tulipotembelea Tanga tulishtuka kuona kwamba kuna mashamba makubwa ya mkonge ambayo yamekuwa ni pori sasa hivi na watu wa Tanga wanasema kwamba bila ya mkonge wananchi wa Tanga wako katika hali ya umaskini. Zao hili kwa bahati nzuri halihitaji mbolea wala haliathiriwi na ukame, lakini maeneo makubwa ya Mkoa wa Tanga hayana kitu, ni pori tu.

Tafiti zimefanywa kwa matumizi mengine ya Mkonge mbali na singa ambayo ni 2% kuna 98% ya Mkonge amabayo hupotezwa bure. Fedha nyingi zimetumika kwa *research* na wao vilevile wanaweza kuzalisha gesi ambayo itasaidia katika kupunguza matumizi ya nishati nchini. Kwa hiyo, nafikiri utafiti huu uliofanywa kule katika kiwanda cha Utafiti cha Tanga, Mkonge ni bora ukufuatiliwa vizuri ili matokeo yake yaweze kulisaidia Taifa.

Mheshimiwa Spika, nigusie kidogo Wizara ya Mifugo. Wizara ya Mifugo ilikuwa ni Wizara mpya. Kwa hiyo, kwa muda mrefu walikuwa wanajipanga vizuri, wanaandaa sera na kweli nafikiri mipango yao ni mizuri.

Katika mifugo, ningependa kuzungumza Kituo cha Ufiti cha Ndorobo kule Tanga. Kituo hiki ni muhimu sana na kina watalaam wengi sana, lakini cha kusikitisha ni kwamba wataalamu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu. Kuna sehemu ambayo wale ndorobo huwa wanapigwa miozi na mionzi hiyo ina hatari kubwa kwa wanadamu.

Kwa hiyo, unapoingia kwenye chumba hicho cha kutibu au kuwageuza hao madume wa ndorobo ili wasiweze kuzaa ni cha chumba cha hatari na hutakiwi kukaa kwa muda mrefu. Sasa wafanyakazi wetu wa kule wanafanya kazi katika mazingira hayo na walikuwa wanadai kitu kinachoitwa *Hardship Allowance,* kwa bahati mbaya Serikali ilikuwa imeondoa *Hardship Allowance.*

Mheshimiwa Spika, lakini Kamati yangu iliridhika kwamba walikuwa na kila sababu ya kuomba kutokana na mazingira yao. Majengo yao kwa kweli yamezeeka kabisa na wanafanya kazi katika mahali ambapo hutegemei wataalamu kama wale wangefanya kazi katika maeneo hayo.

Vilevile katika Wizara ya Mifugo, nizungumzie kuhusu viwanda vinavyotengeneza maziwa kama *Tanga Fresh.* Tumetembelea hapo na tumeona juhudi kubwa zinazofanywa na kwa kweli sisi tungependelea kuona *Tanga Fresh* nyingi katika nchi hii. Kuna *Tanga Fresh, Iringa Fresh*, *Dodoma Fresh* na hata *Mbeya Fresh* katika maeneo yote ambayo mifugo inapatikana kwa wingi tuzalishe maziwa ya aina hiyo kwa sababu kama tunavyosema, ni kwamba Watanzania hawana mazoea ya kunywa maziwa, lakini pengine hawayapati maziwa pale wanapoyahitaji. Sasa tukitengeneza maziwa… *(Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa kuzungumza umekwisha)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tutajitahidi tumalize kabla tuseme tukifika ile saa saba. Kwa hiyo, nimearifiwa na upande wa Serikali kwamba hoja zote pamoja na maelezo mafupi watakayoyatoa Waheshimiwa Mawaziri, hoja zote watazitolea majibu ya maandishi na hususan wenzetu wa ardhi ambao wako Nairobi sasa hivi kwenye Mkutano, kuna hoja zimegusiwa za ardhi hapa tutazipata kwa majibu ya maandishi.

Kwa sasa hivi nitawaomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo dakika saba, Mheshimiwa Naibu Waziri Maendeleo ya Mifugo dakika saba halafu nitamwita Mheshimiwa Mtoa hoja. Mheshimiwa Waziri wa kilimo karibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa dakika saba ili niweze kutoa maelezo mafupi sana.

Ningependa kusema kwamba tunaunga mkono hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi.

Pili ningependa niseme kwamba mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati hii katika Ukurasa wa 20 tumeyapokea na tunayashughulikia na baadhi ya mapendekezo ambayo yametolewa kusema kweli tulishawahi kuanza kuzungumza na Kamati yenyewe.

Kwa mfano, mambo yanayohusiana na *Estate* ya Tukuyu tulishazungumza, mambo ya Dabaga tulishazungumza, mambo yanayohusu Ugani nimeyaeleza vizuri zaidi jana wakati nilipokuwa natoa *briefing,* nisingependa kuyarudia kwa sababu ni sisi hawahawa tuliokuwa katika Kamati ile jana. Kwa hiyo, tutayarudia vizuri zaidi wakati wa bajeti wakati tutakapokuwa tunayaoanisha na utekelezaji pamoja na fedha tutakazoomba kwa ajili ya kazi hii.

Labda jambo moja tu ambalo ningependa niseme hapa, ni juu ya kauli ya Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye. Rafiki yangu Mheshimiwa Kabuye yeye ni *orator* mzuri, akiamua kusema anasema mambo ambayo yanatoa changamoto, lakini wakati mwingine anaeleza lakini yeye mwenyewe hatusaidii kusema tufanye nini.

Sasa amezungumzia juu ya hali ya wakulima, lakini kwa kweli siyo jambo jipya kwa sababu sisi wote tunatoka kwa wakulima kwani kama hukai huko, basi umezaliwa huko. Kwa hiyo, tunajua hali ya wakulima ndiyo maana katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imeelezwa waziwazi kwamba kilimo chetu ni duni, wakulima wetu hawatumii Kanuni za Kilimo Bora na Wakulima wetu wanalima kwa jembe la mkono. Sasa ukitumia nusu saa kueleza hayo mambo utakuwa huelezi jambo jipya kwa sababu hivyo ndivyo hali ilivyo.

Tunachosema sisi, ni hatua gani tunazichukua kubadilisha hali hii? Hiyo ndiyo habari. Tunachukua hatua gani katika kubadilisha hali hiyo habari? Sasa habari ni kwamba, tunachukua hatua, tunataka kubadilisha kilimo chetu kwa sababu kwa hali ilivyo sasa hali ya kilimo hicho ina uhusiano wa moja kwa moja na umaskini wa watu wetu.

Kwa hiyo, hatuwezi kuondoa umaskini wa watu wetu bila kubadilisha kilimo chao, tuna-*address issue* ya *technology* inayotumika kwa wakulima kwani wakulima wetu hawatumii maarifa ya kisasa katika hiki kilimo. Kwa hiyo, kuanzia sasa kupitia Mpango wa *SDP* tuta-*address issue* ya kufikisha maarifa kwa Wakulima ili tuhakikishe kwamba wanatumia maarifa hayo kubadilisha kilimo chao.

Waheshimiwa Wabunge, tumezungumza habari ya kulima kwa jembe la mkono, ni kweli. Lakini ni lazima tuanze sasa kutoka kwenye jembe la mkono, lakini tunajua kwamba huwezi kutoka kwenye jembe la mkono ukaenda kwenye trekta kwa sababu wakulima wetu walio wengi hawana uwezo wa kununua trekta. Kwa hiyo, naungana mkono, na wale wote wanaosema tutumie wanyamakazi na sisi tuna *program* maalumu ya kufundisha kama ile aliyoisema Mheshimiwa George M. Lubeleje kwamba tunafundisha matumizi ya wanyamakazi ili tuanze hatua kwa hatua kutoka kwenye jembe la mkono kwenda kwenye wanyamakazi.

Lakini vilevile tunakopesha matrekta, kwa sababu hatuwezi kusema kwamba sisi ni *free from tractors* ni lazima tutumie *animal power and motor power.* Tunafanya yote hayo ila kwa sababu ya uwezo wetu mdogo matrekta yataingia hatua kwa hatua na tunaomba Sekta Binafsi kwa uwezo mdogo tulionao waendelee kukopa yale matrekta na kuyatumia katika kilimo, siyo kuyakopa halafu yanakuwa lori la kubeba mchanga na

mawe wakati kilimo hakina majembe. Kwa hiyo, kuna masuala hayo. Sasa nadhani nikilisema hivyo, nitakuwa nimejibu sehemu kubwa ya yale yaliyosemwa.

Rafiki yangu Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye yeye amezungumza juu ya ubadhilifu katika Vyama vya Ushirika. Anasema kwamba Rais wetu amezumguzia mambo ya ukaguzi, lakini hakuzungumza ushirika. Rais alishasema ushirika sana alipokuwa Mwanza, amekemea sana juu ya masuala ya ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika. Lakini ni lazima tuseme Vyama vya Ushirika ni vya Wanachama na sisi kama Wabunge tunaweza tukawa wanachama wa Ushirika na tukavisaidia Vyama vile ili viweze kufufuka na sisi upande wa Serikali tunafanya kazi hiyo. Tunataka kufufua Vyama na tuna *program* mwaka huu ya kufufua Vyama vya Pamba na Vyama vya Korosho ili vi-*address problem* ya masoko kwa ajili ya kuleta ushindani wa haki kwa mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ni kwamba maswali mengine tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yaliyo fasaha kabisa. Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo kwa masuala yale yanayohusu mifugo kwa dakika zisizozidi saba. Karibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naanza kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi.

Mheshimiwa Spika, naongea kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Salim aliyeweza kusema ukweli kwamba Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ni Wizara mpya na kwa hiyo, pamoja na mambo mengine, ina kazi kubwa ya kujipanga vizuri ili kusudi kutimiza ipasavyo maelezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa mujibu wa Kifungu Na. 32.

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Kamati yetu ambayo kusema kweli imetusaidia sana sisi katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mambo mbalimbali ambayo imetoa muhtasari wake hapa na kusema kweli mambo mengine mengi waliyoyazungumza yatajionesha kwenye bajeti yetu ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, niruhusu niweze kusema machache kuhusu maoni ya Kamati suala mojawapo likiwa ni la Serikali kuwapatia wafugaji maji, malambo na miundombinu mingine na kuwawezesha kupata malisho ili kuondoa tatizo la kuhamahama.

Mheshimiwa Spika, hili linazingatiwa kwa namna mbalimbali na tumekuwa tukilitolea maelezo hata kwenye maswali mbalimbali yanayojitokeza, yaani maswali ya msingi na ya nyongeza.

Pia, nimezungumzia vilivyo kuinua machinjio ya kisasa ya Dodoma na hili linazingatiwa kwa kikamilifu. Sambamba na hilo, limezungumziwa suala la ukataji wa nyama kitaalamu kwamba uimarishwe.

Machinjio ya Kisasa ya Dodoma ilianza kujengwa mwaka 2004 na kukamilika mwaka 2004 sambamba na Chuo cha Mafunzo ya Ukataji Nyama kilichopo pia hapa hapa Dodoma na wiki iliyopita Wizara yangu ilikabidhi Chuo hicho cha Ukataji Nyama kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi chini ya *VETA* ili waweze kukindesha kwani wao ndiyo wanastahili kabisa ili Watanzania wengi waweze kujifunza taaluma hii ya ukataji nyama ili hatimaye Watanzania tuweze kupata nyama iliyokatwa kwa viwango.

Mheshimiwa Spika, limezungumziwa suala la ruzuku ya madawa ya mifugo na hili tumekuwa tukilitolea maelezo na kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha jumla ya dola bilioni 2 zilitolewa kwa ajili ya ruzuku ya madawa ya mifugo ambayo imegusa Mikoa 18, Mikoa mitatu iliyobaki itajumuishwa kwenye ruzuku katika mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, pia nilibahatika kupata michango ya Waheshimiwa Wabunge watatu wakiwemo Mheshimiwa George M. Lubeleje ambaye naomba nikubaliane naye kwamba Tanzania ni kweli kama tunavyofahamu ina mifugo mingi ni ya tatu Afrika, ikiwa na ng'ombe 18,500,000.

Mheshimiwa George M. Lubeleje alizungumzia uwepo wa Homa ya Bonde la Ufa, lakini nimpongeze sana kwa kuungana nasi katika kuwakumbusha na kuwaelimisha wananchi kuhusu namna ya kujikinga na Homa hii ya Bonge la Ufa ambayo kimsingi kama tungekubali kuzingatia masharti yote ya kujikinga na ugonjwa huu tungeweza kuwa kwenye nafasi nzuri.

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilirudia Kauli ya Serikali ya kusema haijazuia Wananchi kula nyama, ilimradi itokane na wanyama safi waliokaguliwa na nyama iliyochinjwa vizuri ikakaguliwa na ikapikwa vizuri tayari kwa kuliwa. Mheshimiwa George Malima Lubeleje aliliongelea vizuri sana katika hili na ninapenda kumpongeza sana.

Mheshimiwa Spika, suala la chanjo lilizungumzwa, pia alizungumza suala la kuchimba malambo ambalo nimekwisha litolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mgana I. Msindai kwanza alipongeza juhudi za Serikali kwa ujenzi wa Machinjio ya Kisasa sambamba na Ujenzi wa Chuo cha Ukataji Nyama. Mheshimiwa Mgana I. Msindai tunakushukuru sana na kwa taarifa tu ni kwamba hii ni machinjio ya kwanza ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, kuna machinjio nyingine, nilisema asubuhi hapa kwamba ipo Mvomero inaendeshwa na Sekta Binafsi, Mkoa wa Rukwa pia inaendeshwa na Sekta Binafsi ikiongozwa na Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya Mbunge. Zote hizi ni machinjio za kisasa, viwanda na machinjio nyingine za kisasa zinajengwa nchi nzima ili kusudi tuweze kupata nyama safi kwa soko la ndani na kwa ajili ya soko la nje ili kuinua mchango wa Sekta ya Mifugo katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mgana I. Msindai alionyesha kusikitishwa kwake na hali ya machinjio kule Ukonga. Wizara imelisikia na itafuatilia pia licha ya wito wake alioutoa,

lakini pia Wizara ina wajibu wa kufuatilia kuona hali ilivyo ili kusudi kama hali ni mbaya kiasi hiki, iweze kusahihishwa bila kuchelewesha.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo yalikuwa mambo ya msingi. Suala la Mheshimiwa Salum nimekwishaeleza alivyoeleza. Ningependa kumalizia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Kama nilivyotangulia kusema hoja nyingine zote kwa kikamilifu zitajibiwa kwa maandishi na Wizara husika. Kwa utaratibu, sasa nimwite Mtoa hoja, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi na kwa kuzingatia kwamba Serikali imeunga mkono mapendekezo, nadhani hana mengi sana ya kusema. Mwenyekiti karibu.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI - MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kweli kazi yangu itakuwa kwanza kuwatambua waliochangia kwa kuzungumza humu ndani na kwa maandishi. Nianze kwa kuwatambua waliochangia kwa kauli.

Kwanza ni Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Salim, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira na Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana wote ambao wamechangia katika taarifa yetu na kimsingi, wote wameunga mkono taarifa ya Kamati, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao wamechangia na kwa kuwa baadhi ya haya tumekwishazungumza nao kwenye Kamati, naamini kwamba tutaendelea kushauriana nao ili tuweze kupata taarifa na majibu kwa hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa katika mchango wa leo.

Kwa hiyo, ningependa tu kwa kumalizia niseme kwamba sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuyakubali mapendekezo yaliyomo katika Taarifa ya Kilimo na Ardhi kwa mwaka 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo na Ardhi yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu ni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi ikiomba kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hiyo. Hoja hiyo imetolewa na Mwenyekiti na imeungwa mkono.

Kwa kuwa bado tuna dakika chake, naomba tusiweke tu shauku miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge, namwomba Katibu sasa asome matokeo ya kura tulizopiga kuhusu Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**NDG. DAMIAN S. L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kama ifuatavyo:

Nilikuwa nimetangaza kwamba waliokuwepo katika Ukumbi huu walikuwa ni 215, lakini wakati huohuo nikawa nimetoa tahadhari kwamba naona kama kuna wapigakura wanaingia na kumbe kweli wameingia 15 zaidi. Kwa hiyo, wakawa waliopiga kura sasa ni 230.

Mheshimiwa Spika, kura zilizopigwa ni 230, idadi ya kura zilizoharibika ni tano na matokeo ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo kapata kura 61, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri kapata kura 164.

Kwa mujibu wa matokeo haya, aliyechaguliwa ni Mheshimiwa Ruth B. Msafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo matokeo ambayo ndiyo yamesimamiwa au alikuwepo shahidi wa Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo ambaye ni Mheshimiwa Halima James Mdee naye ameyakubali matokeo hayo.

Mheshimiwa Spika naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tutapata nafasi ya kuwasikiliza kwa muda mfupi sana wakati wa shughuli za jioni.

Kwa sasa hivi niseme tu kwamba, saa 11.00 tutaanza na Taarifa ya Mwenyekiti wa Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, itafutiwa na Azimio la Bunge na mwisho nitamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hoja ya kuahirisha Bunge.

Nikumbushe tu kwamba, saa 07:30 mchana tuna Mkutano mfupi wa Kamati ya Uongozi, yaani Wenyeviti wote na Saa 08: 00 mchana tutakuwa na Mkutano mfupi pia wa Kamati ya Kanuni kuzingatia utaratibu mpya wa Kanuni ambazo zimeandaliwa.

Baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11:00 jioni.

*(Saa 07.00 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**HOJA ZA KAMATI**

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO (k.n.y. MHE. JUMA S. NH'UNGA) - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na kwa niaba ya Wanakamati wa Kamati hiyo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kuwasilisha Taarifa ya Kamati hiyo pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hiyo, na kwamba ni mategemeo yangu hapo mwishoni kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu waikubali pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kamati yangu, napenda kutumia fursa hii kutoa salamu za rambirambi kwako wewe Mheshimiwa Spika, Serikali, familia, ndugu na wananchi wa Jimbo la Tunduru, kutokana na kifo cha Marehemu Juma Jamaldin Akukweti, aliyefariki nchini Afrika Kusini mwezi Januari, 2007.

Aidha, napenda kutoa pole kwa ndugu na jamaa wa Marehemu Dr. Aaron Chiduo, aliyekuwa Mbunge wa siku nyingi na Waziri wa Afya. Vilevile napenda kutoa rambirambi za Kamati yangu kwa Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu na ndugu zake kwa kifo cha mama yao mpendwa.

Mwisho, napenda kutoa salamu za rambirambi za Kamati yangu kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Arusha kwa vifo vya wananchi kwenye ajali ya basi la Buffalo vilivyotokea siku chache zilizopita. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amin!

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa ndugu yetu Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Tunduru kuwa Mbunge wao mpya kwa kura nyingi. Pongezi hizo vilevile ziende kwa Chama cha Mapinduzi kilichomsimamisha Mheshimiwa Mtutura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ya Mwaka 2006, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(11), Kanuni za Bunge za Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda nikuarifu kwamba wajumbe wa Kamati hii uliwateua mwezi Januari, 2006 na uteuzi huo ulifanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 87. Napenda kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga - Mwenyekiti, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo - anayesoma taarifa hii, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo - alikuwa mjumbe lakini baadaye akajiuzulu na Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa William M. Ngeleja - Mjumbe ambaye baadaye aliteuliwa kuwa Naibu Waziri na Kamati inampongeza sana kwa uteuzi huo na mwisho Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa historia fupi ya Kamati. Kabla ya mwaka 1999, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilijulikana kama Kamati ya Haki za Bunge na ilikuwa na majukumu mawili:- (i) Kushughulikia masuala yote yahusuyo Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge; na (ii) kufikiria jambo lingine lolote litakalopelekwa kwenye Kamati hiyo na Spika.

Hata hivyo, kwa kutambua kuwa hakukuwa na chombo kilichokuwa kikishughulikia maadili ya Wabunge, mwaka 1999, Kamati ya Haki za Bunge ilipendekeza Bungeni iongezewe jukumu hilo na Bunge lilipitisha na kukubali pendekezo hilo. Tangu wakati huo Kamati hii sasa ilijulikana kwa jina la Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, yameainishwa katika Kanuni ya 99 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, kama ifuatavyo:-

- Kuchunguza masuala yote yahusuyo Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge yanayopelekwa kwake na Spika;

- Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge; na

- Kufikiria jambo lingine lolote litakalopelekwa kwake na Spika

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanywa na Kamati ni moja, Semina na mafunzo. Mara tu baada ya kuwateua Wajumbe wa Kamati hii, Ofisi yako iliandaa semina ya Wabunge wote iliyofanyika mwishoni mwa mwezi Januari, 2006 katika jengo la Ubungo Plaza, Dar es Salaam. Katika semina hiyo mada kadhaa zilitolewa zikiwa na lengo la kuwaelimisha Waheshimiwa Wabunge juu ya kazi mbalimbali za Bunge, stahili zao, kazi zao, na kadhalika.

Aidha, mara baada ya semina hiyo, tarehe 2 Februari, 2006, Kamati iliwachagua viongozi wake katika Kikao kilichofanyika Ofisi ya Bunge, Dar es Salaam, ambapo Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mbunge wa Jimbo la Dole alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, tarehe 10 – 13/4/2006 Kamati ilishiriki katika semina iliyoandaliwa na Ofisi ya Bunge, kwa ajili ya kuongeza ufahamu wa Kamati juu ya maeneo mbalimbali yanayohusiana na majukumu yake. Katika semina hii jumla ya mada saba zilitolewa kama ifuatavyo:-

(1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge: Uzoefu hadi 2005 ambayo ilitolewa na Ofisi ya Katibu wa Bunge;

(2) Sheria ya Haki, Madaraka na Kinga ya Bunge, 1988 ambayo ilitolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(3) Mchakato wa Kutunga Sheria nchini Tanzania ambayo ilitolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(4) Haki za Binadamu na nafasi ya Bunge katika utekelezaji wake ambayo ilitolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu;

(5) Namna Sekta ya Utumishi wa Umma inavyodhibiti nidhamu za watumishi wake na hii ilitolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

(6) Mambo muhimu ya kuzingatiwa na chombo cha utoaji Haki na hii ilitolewa na Msajili wa Mahakama ya Rufaa; na mwisho

(7) Jinsi Mahakama inavyodhibiti nidhamu za Majaji/Mahakimu pia ilitolewa na Msajili wa Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Kamati hii ni chombo kinachojihusisha na utoaji haki, mada hizi zililenga kuwaelimisha Wajumbe misingi ya utoaji haki, haki za binadamu na nafasi ya Bunge katika kuzilinda haki hizo, jinsi Sheria ya Haki, Madaraka na Kinga ya Bunge 1988 inavyotumika, historia ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, na taratibu zilizokuwa zikitumika katika kusikiliza mashauri yaliyopelekwa kwenye Kamati. Pia Kamati ilipata fursa ya kusikiliza jinsi maadili ya Majaji/Mahakama na watumishi wa umma yanavyodhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, semina hii ilikuwa ya manufaa kwa Kamati yangu kwani Wajumbe walikiri na hadi leo wanaendelea kukiri kuwa walijifunza mambo muhimu na kwamba iliwajengea uwezo mzuri wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya haki. Katika tathmini ya jumla, Kamati iliona kuwa kulikuwa na umuhimu mkubwa kwa Bunge kuwa na Kanuni za Maadili ya Wabunge ili pawe na mwongozo kwa maadili yatakayofuatwa na Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, yaliyojitokeza katika semina, kwa muhtasari Kamati ilijifunza kuwa chombo chochote kinachojihusisha na utoaji haki hakina budi kumpa haki za msingi mtuhumiwa yeyote anayeitwa mbele ya chombo hicho. Hizi ni haki za kikatiba na zipo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 hasa Ibara 13(6). Haki hizo ni pamoja na haki ya kusikilizwa, haki ya kuwakilishwa na kadhalika. Aidha, Kamati ilijifunza kuwa Taasisi kama Mahakama imeweka utaratibu wake wa kuwadhibiti Majaji na Mahakimu wanapokiuka taratibu zao za kazi. Halikadhalika, Kamati ilijielimisha jinsi sekta ya utumishi wa umma inavyodhibiti nidhamu za watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu lilofanywa ni uchambuzi wa kanuni za maadili ya Wabunge. Tarehe 15 – 19/5/2006 na 5 – 6/6/2006, Kamati ilikutana Dar es Salaam, kwa ajili ya kuandaa Kanuni za Maadili ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa, kazi ya kuandaa Kanuni za Maadili haikuanza na Kamati hii. Kazi hii ilianza tangu Kamati hii ilipojulikana kama Kamati ya Haki za Bunge. Hata hivyo, hadi 2005 kazi hiyo haikuwahi kukamilika. Hivyo basi, katika kipindi hiki Kamati ilifanya uchambuzi wa Kanuni za Maadili ya Wabunge kwa kuangalia Kanuni za Maadili za Bunge la Uingereza, Uganda, Australia na kadhalika. Hatimaye, Kamati iliandaa Rasimu ya Kanuni za Maadili ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na kuwasilisha kwako ili zifanyiwe kazi. Tazama Kiambatisho ambacho kipo pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya Bwana Reginald A. Mengi – Mwenyekiti Mtendaji wa *IPP* na Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima - Mbunge wa Mkuranga. Tarehe 21 Agosti, 2006, uliipatia kazi Kamati hii kuchunguza malalamiko ya Bwana Reginald Mengi aliyowasilisha kwako kwa barua yake Kumb. Na. *ITV*/C/BUNGE/06/2006 ya 6 Agosti, 2006 yenye kichwa cha habari: "Shutuma za Mheshimiwa Adam K. Malima dhidi ya *ITV* Bungeni na malalamiko ya Mheshimiwa Adam K. Malima, Mbunge, dhidi ya Taarifa ya Bwana Reginald Mengi, Mwenyekiti Mtendaji wa *IPP*", aliyoitoa kwa vyombo vya habari, yaliyowasilishwa kwako pia.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi hii, Kamati ilitoa fursa kwa walalamikaji kuwaleta mashahidi wao. Vilevile iliwaita wataalamu kadhaa kama mashahidi kadhaa wakiwemo Wahariri wa Vyombo vya Habari na watu binafsi. Pia Kamati ilipitia vielelezo kadha vya kanda za video na magazeti vilivyoletwa na walalamikaji. Aidha, ilipata maoni ya kitaalamu kuhusu Katiba na Sheria, Sekta ya Habari na Mawasiliano kutoka Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, vilevile kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

Kamati inapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, Mbunge, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu - Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Johnson Mwanyika - Mbunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wao kwa kuisaidia Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ikishughulikia malalamiko ya Bwana Reginald A. Mengi, Mwenyekiti Mtendaji wa *IPP* na Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Mbunge, pia uliipelekea kazi Kamati kushughulikia suala la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto - Mbunge wa Kigoma Kaskazini, ajieleze kutokana na kauli yake aliyoitoa kwa Waandishi wa Habari tarehe 2 Novemba, 2006 baada ya uchaguzi wa Wagombea Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki uliofanyika katika Mkutano wa Tano wa Bunge. Kauli yake ilinukuliwa kwenye vyombo vya habari yakiwemo magazeti ya Nipashe na Tanzania Daima ya tarehe 3 Novemba, 2006 yaliyomnukuu akihoji pamoja na mambo mengine, uelewa wa Spika juu ya Kanuni za Bunge kuendesha uchaguzi huo, kwamba ama hazijui au anazijua, lakini aliamua kuzipindisha kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Novemba, 2006 ndani ya Bunge hili, ulimtaka Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, akuombe radhi ndani ya siku tano, kwa kauli yake nje ya Bunge, iliyoonesha dharau na utovu wa nidhamu kwa Spika binafsi na kwa nafasi ya Spika kama Kiongozi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili lilihusu maadili ya Mbunge hususan, “kuonyesha dharau kwa Spika na kutotiii maelekezo yake”, uliona ni vyema, kwa mujibu wa mamlaka uliyopewa chini ya kifungu cha 12(2) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988, ulipeleke mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata mapendekezo ya Kamati hii tarehe 1 Februari, 2007 ulitoa maamuzi yako Bungeni kuhusu suala hili na kumsamehe Mheshimiwa Kabwe, ukizingatia pamoja na mambo mengine jitihada alizofanya kukutafuta kukuomba radhi na kuzingatia kuwa alikuwa ametenda makosa ya kuonesha dharau kwako, kinyume cha kifungu cha 24(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988, makosa ambayo ulisema kwamba huenda alitenda kutokana na ugeni wake kuhusu taratibu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kazi zote hizi tatu, nikianza na Malalamiko ya Bwana Reginald A. Mengi - Mwenyekiti Mtendaji wa *IPP*, Mheshimiwa Adam Kighoma A. Malima, Mbunge wa Mkuranga yaliyowasilishwa kwenye Kamati kwa barua yako ya tarehe 21 Agosti, 2006 na suala la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, yaliyowasilishwa

mwezi Desemba, 2006, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, uliipatia Kamati kazi ya kuchunguza masuala hayo na kisha ikushauri.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilichunguza kwa makini mashauri yote matatu na kuwasilisha taarifa kwako na kukupa ushauri ambao uliufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Moja, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Bunge iwe na chumba mahsusi kitakachokuwa na nyenzo mahsusi kwa ajili ya vikao vya Kamati hii na nyinginezo zinaposhughulikia masuala nyeti. Aidha, kuwe na chumba maalumu *(strong room)* kwa ajili ya kuhifadhi vielelezo vya ushahidi vitakavyotumiwa na Bunge na Kamati zake.

Pili, Ofisi ya Bunge iandae ziara fupi za mafunzo kwa ajili ya Kamati kuwawezesha Wajumbe kujifunza uzoefu wa Mabunge mengine jinsi yanavyoshughulikia masuala ya Kinga, Haki na Maadili ya Bunge ili Bunge na Kamati zake ziende na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, kutokana na utafiti ambao Kamati hii imeufanya juu ya kuwepo kwa Kanuni za Maadili ya Wabunge katika nchi kadhaa za Jumuiya ya Madola, Kamati hii imewasilisha kwako Mheshimiwa Spika Rasimu ya Kanuni za Maadili ya Wabunge ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo tunashauri ifanyiwe kazi pamoja na mapendekezo ya Kanuni mpya za Bunge yaliyowasilishwa kwako.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza hapo mwanzo, kwenye mwisho wa taarifa hii tumeweka Kiambatisho Na.1 ya Rasimu ya Kanuni hizo.

Nne, kutokana na majukumu yake ya kushughulikia masuala yote yanayohusu Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, pia Kamati hii imekuwa ikishughulikia suala la Ofisi za Wabunge Mikoani na Wilayani ili kuona kama zinalingana na hadhi na nafasi ya Mbunge. Kamati inatarajia kuanza kuzikagua Ofisi hizo hivi karibuni kwenye Majimbo ya Wabunge.

Tano, kwa kuwa Kamati hii hufanya kazi kwa kutumia taratibu zinazofanana na Mahakama kwa kiwango fulani ingawa yenyewe sio Mahakama, Kamati inahitaji kupata semina za mara kwa mara za mafunzo hususan kupata uzoefu juu ya uendeshaji wa mashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nichukue fursa hii kukupongeza kwa kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu kwa kipindi chote hiki. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kutekeleza vema majukumu yao wakati wote ulipowaachia majukumu. *(Makofi)*

Napenda nitumie fursa hii pia kuwashukuru Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Kamati katika kipindi chote hiki.

Napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano na ushauri wao waliokuwa wakiutoa Kamati hii mara kwa mara.

Kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kama nilivyowatajwa hapo mwanzo, kwa ushirikiano mkubwa waliompa Mwenyekiti wetu katika kipindi hiki bila kumsahau Katibu wa Bunge, Bwana Damian Foka na watumishi wote wa Bunge wakiwemo Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Nenelwa Mwihambi na Charles Mloka kwa kufanikisha shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 106, Kanuni za Bunge, nilizokwishazitaja, naomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali. Kwa heshima na taadhima, naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JUMA K. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Mwakilishi wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, Mezani kwangu nina wachangiaji watatu na sina hakika kama kuna Waziri atakayeongea. Lakini basi, ninao hawa wafuatao: Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Tutaanza na Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja iliyo mbele yetu inayohusu Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya familia yangu na pia kwa niaba ya ndugu zangu wote nataka kutoa salamu za rambirambi kwa Mheshimiwa Harith Mwapachu ambaye amefiwa na mama yake. Natumai mazishi yamekwisha. Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ni ya maana sana kwa sababu inazungumzia juu ya madaraka ya Bunge letu na madaraka ya Bunge letu yapo katika Ibara ya 63 ya Katiba ambayo napenda kuyanukuu. Yanasema:

"Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utendaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunayosema ndani ya Bunge na tunayopitisha kama Maazimio au kama mapendekezo ya Bunge hili ni vizuri basi Serikali ikajua tunafanya hivyo kwa niaba ya wananchi wa Tanzania, na hivyo kuyapa hayo mapendekezo umuhimu unaostahili na kujibu basi Bunge.

Mheshimiwa Spika, juzi hapa tulipokuwa kama Kamati ya Hesabu za Serikali tulitoa mapendekezo mengi sana na mengine yalihusu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na mengine yalihusu Wizara ya Fedha, mengine yalihusu Wizara ya Miundombinu na pia Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, tulichotegemea katika Bunge hili ni kuletewa majibu na Serikali. Lakini mpaka leo tunafunga Bunge lako Tukufu, hakuna majibu ya Serikali. Nina hakika ni hivyo hivyo kwa baadhi ya Kamati nyingine za Bunge. Nasi tunatumia fedha nyingi sana katika Kamati za Bunge kuweza kuangalia mambo mbalimbali ya nchi yetu na fedha nyingine umeshazitamka wewe mwenyewe mpaka Shilingi milioni 100 kuangalia baadhi ya mambo ambayo yanahusu uendeshaji wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikerwa sana. Badala ya kuweka umuhimu kwa mfano, kwa upande wa madini, juu ya uhakiki wa madini, Waziri alisimama hapa akasema watafanya hiyo kazi wao wenyewe. Waziri alipuuza kabisa mapendekezo ambayo yamo katika taarifa ya Bunge na yalikuwa mapendekezo kwa Wizara yake zaidi ya mapendekezo nane. Moja, lilihusu pawepo na hali ya utulivu katika sekta ya Madini, lingine lilihusu pawepo na mjadala juu ya kurekebisha sheria kwa mfano, kuondoa *fifteen percent additional allowance* kwa ajili ya madini.

Lingine lilikuwa linahimiza kwamba *TRA* iangalie baadhi ya hasara ambazo zimezungumzwa katika taarifa mbalimbali ambazo tulikuwa tumeletewa kama Kamati. Lingine lilikuwa linasema tuangalie sasa hivi bei ya uhakiki ili iwe nafuu. Lakini zaidi pawepo na *a transaction period* ambayo inahakikisha kwamba kweli tuko tayari kuchukua kazi hiyo muhimu ambayo ni ya uhakiki wa madini yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa Mheshimiwa Waziri kusimama mbele yetu hapa Waheshimiwa Wabunge na kusema wataanza kufanya hiyo kazi wao wenyewe, kwanza, ni kukiuka sheria. Kwa sababu sheria haikubali kwamba ujikague wewe mwenyewe. Ni lazima uwe na *External Evaluator* nje ya *operations.* Angetuambia kwamba tunataka *Controller and Auditor General* afanye hiyo kazi, labda ningeondoka kidogo nimeridhika au kwamba linafanyiwa kazi. Angetuthibitishia kwamba mapendekezo yote yanayosemwa na Kamati za Bunge yanaangaliwa, hapo ningeondoka kidogo nimefarijika. Lakini Wizara ya Nishati na Madini ni sugu kwa matatizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Cheyo, taarifa iliyopo hapo ni Taarifa ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Naona kama umejisahau unazungumza kama Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Sasa sogea kidogo kwenye upande wa taarifa ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Ninajua mambo haya ni vigumu kuyatenganisha.

**MHE. JOHN M.CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nasogea kidogo kwenye taarifa husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kaa kwanza. Vipi bwana, mbona tunabishana tena. Sogea kwenye upande wa taarifa kama ilivyosomwa kuhusu taratibu za Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wewe. Nilichokuwa nataka ku-*conclude* ni kwamba Kamati kama yetu ni sawasawa na Kamati nyingine zilizopo hapa. Natoa taarifa za Kamati za Bunge na hapa hoja ninayoijenga, yale tunayosema ambayo ndiyo madaraka ya Bunge kwa umuhimu ambao unastahili. *This is a point which I am trying to lead.* Wala sitaki kujikita zaidi huko na sitaki kubishana na wewe.

Nilichokuwa nataka kueleza ni kwamba hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na yeye ametoa maneno hayo hayo. Katika kukiangalia hata siku hizi tuna taarifa ambayo ni ya kiswahili na yeye ananung'unika juu ya *carat* zaidi ya 400 ambazo hazina udhibiti na ana-*conclude* kwamba hakuna uwezo ndani ya Wizara ambao unaweza kuangalia mambo haya ya madini. Repoti ya *CAG*.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema, kama sisi tumefanya kazi hapa na tukatoa *recommendations* nyingi, tunataka Wizara mbalimbali Serikali iyachukue maneno kuwa ni muhimu na kama inasomwa hapa halafu inapigiwa kura sio tena mapendekezo ya Kamati ni mapendekezo ya Bunge zima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kutoyawekea utaratibu ambao unaweza ukajibu unakiuka au unadhoofisha madaraka ya Bunge letu. Hicho ndicho kitu ambacho nilitaka kujikita.

Nikiondoka kwenye sekta hiyo, nakwenda upande mwingine. Juzi hapa tulipokuwa tunaangalia maswali ya Bunge ambayo leo nafurahi sana kusema kwamba Bunge limeanza kuwa mfano mzuri wa kuleta mahesabu yasiyokuwa na dosari. Safi kabisa! Lakini tumegundua kitu kimoja kwamba Madaraka yetu ya kuweza kuidhibiti Serikali hayawezekani kama Bunge halina Bajeti ambayo inajitegemea. *(Makofi)*

Pamekuwa na baadhi ya Kamati imebidi kwenda kwa mtu wanayemkagua. Kwa mfano Wizara inaongozwa na Waziri Mkuu na kuomba fedha mpaka kiasi cha Shilingi milioni 65 ili waende wakakague utekelezaji wa shughuli za Serikali, fedha hizo kwa upande wa Bunge hazipo.

Kwa hiyo, kama Serikali haiitengei Bunge fedha kufuatana na Sheria ambayo Sheria inasema bayana kabisa kwamba *there shall be a National Assembly Fund* na hii tumethibitisha juzi tulipokuwa kwenye Kikao cha *PAC*, sheria hiyo ipo na *CAG office* inaifahamu, sasa kama Serikali inabishana na ina-*deal* kuweza kuitengea bajeti nzuri tena ya makubaliano *percent* kadhaa iende kwenye Bunge, Bunge hili litakuwa lina Katiba nzuri ambayo inani-*support* kwamba Bunge ndiyo lenye madaraka. Lakini Bunge linakaa likigandamizwa na Serikali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi ambayo tunaweza hapa na kwa hili ninataka kusifu, tunamaliza Bunge hili bila kuwa na kesi yoyote ya kuweza kutukanana hapa au kufanyiana fujo na wewe vikesi vidogo vidogo kama kwa Mheshimiwa Chacha Wangwe umeyamaliza vizuri, tunaondoka wote tuna-*smile,* natumai na baadaye tunapata hotuba hapa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya lala salama. *(Kicheko)*

Lakini bila kuliwezesha Bunge hili kuweza kufanya kazi yake haya mambo mengine madogo madogo tunayofanya hapa ni kulishana pipi tu. Tunataka Bunge lenye nguvu, lenye madaraka kama vile Katiba inavyosema. Njia ya kupata madaraka ni

kuhakikisha kwamba Bunge linasikilizwa na Serikali. Ni kuhakikisha kwamba Bunge linapotaka kutenda mambo yake linafanya kwa sababu lina uwezo. Wananchi wote waelewe mambo ambayo tunayafanya hapa.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa naiangalia Serikali, Wizara ya Fedha imeweka pale programu ya kueleza kazi ya Serikali ua Idara ya Fedha. Vipeperushi vipo na programu ya televisheni, sijui imewa-*cost* shilingi ngapi, lakini ipo. Je, Bunge ni programu gani iliyopo ambayo inaeleza wananchi kwamba madaraka yetu kama Bunge ni hivi. Tuna uwezo huu, tuna mipaka hii na wananchi hawana mipaka kwa sababu wao ndiyo wametuweka hapa. *(Makofi)*

Hilo ndiyo tunapaswa kuzungumza juu ya maadili na madaraka ya Bunge, watu wajue wana madaraka hapa, na Serikali hii ni Serikali ya Bunge hili. Tena mimi nashangaa, kwanza Bunge hili Serikali inatokana na Wabunge wenyewe na wengi wakishapata Uwaziri wanafikiri kwamba ndiyo wameula, basi. *(Kicheko)*

Kuna siku ya kuwa Mbunge na kuna siku ya kuwa Waziri. Mimi sina hiyo *hope* ya kuwa Waziri na kuna siku ya kurudi nyuma na waliorudi nyuma wapo wengi tu na wengi wao ni watu wazuri tu wapo upande huu. *They are good back benchers*. Kwa hiyo, tunapozungumzia madaraka ya Bunge si *confrontation* kati ya Bunge na Serikali. Tungependa kuona kwamba Serikali na Bunge tunakwenda pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini ni mara ngapi hata wewe najua huwezi kusema haya. Ni mara ngapi tumekaa katika Kamati ya Uongozi tunaisubiri Serikali ije? Mara ngapi? Kama kweli Serikali ingekuwa inaona kwamba wenye madaraka ni Bunge, tuki-*fix* kwamba saa 4.00 tuna Mkutano na Spika kila mmoja awe pale *exactly ten o'clock* Spika anakaa tunaanza Kikao. *(Makofi)*

Sisi katika Kamati tunawaandikia Maafisa Wahasibu waweze kuja kwenye Kamati, unapata *excuses*; na unaambiwa kwamba mimi nina Mkutano na Waziri Mkuu Dodoma. Kamati yetu tumesema sisi ndiyo wenye madaraka, Waziri Mkuu atasubiri unakuja hapa. *(Makofi)*

Nimeona nitumie nafasi hii ku-*lead* hili kwa sababu halieleweki. Tunaonekana tunaendesha hapa kama vile tuna Vyama viwili. Chama kimoja Serikali na mambo yake, Chama kingine Bunge la Tanzania na sisi tunagandamizwa tu. Mara utaambiwa leo tutamaliza Bunge, mara hapana, kesho tutamaliza, kesho hapana! Tunataka Mheshimiwa Spika aendeshe Bunge hili na sio mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, Madaraka ya Bunge yahimizwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ulipomwelekeza Mheshimiwa Cheyo kwenda kwenye hoja iliyoko hapa naona hakutii na badala yake ameendeleza mfululizo wa lawama na kujenga picha ya kana kwamba Serikali hii ni Serikali ambayo haiheshimu Bunge, haiheshimu Kamati za Bunge ambalo sio kweli.

Mheshimiwa Spika tena yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Uongozi, nilifikiri atakuwa ameelezwa kwenye Kamati ya Uongozi kwamba *general fund* ya Bunge ipo kwa mujibu wa Sheria toka mwaka 1997 na kwamba tumekubaliana kuanzia sasa Bunge

litakuwa *Independent* katika matumizi yake kwa kufuata Sheria hii ya toka mwaka 1997. *(Makofi)*

Sasa tukishakubaliana hivi, nilifikiri Mheshimiwa Cheyo angekuwa Muungwana zaidi kwa kuiheshimu Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Hilo nathibitisha ni kweli kabisa na hatua za kuweza kurekebisha ni kushirikiana na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na zinaendelea hivi sasa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Sasa nadhani nihamie kwa Wabunge wa CCM ili wapinzani wasipangane pamoja, maana yake nikimwita Mheshimiwa Kabwe Zitto itakuwa ni mtiririko ule ule. Sasa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo halafu tutamalizia Mheshimiwa Zitto.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi nina machache sana nadhani nitatumia nusu ya muda ulionipa. Lakini awali ya yote nianze kwa kuipongeza sana Kamati hii ambayo kwa kifupi ukiangalia utafikiri ina kazi chache sana. Lakini ukweli wenyewe ina kazi za muhimu sana na nzito sana kwa ajili ya Bunge letu. Aidha, napenda kuipongeza Kamati hii kwa kushughulikia masuala ambayo wametuambia bila upendeleo. Mimi binafsi nilifarijika sana. Hongereni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nina machache, *point* kama tatu. Ya kwanza, niseme kwamba nimefarijika sana, moja ya kazi ya Kamati hii ni kupitia na kufanya ukaguzi katika Ofisi za Wabunge Mikoani na Wilayani. Niseme Kilindi pamoja na matatizo yake lakini kwa kweli Ofisi ya Mbunge ni ya Mfano. Nina Ofisi Kubwa ambayo imewekewa pia na *furniture* na Serikali. Kwa hiyo, kwa hapo nawapongeza na ninawashukuru.

Mheshimiwa Spika, ila tu niseme kwamba ninaomba basi hilo liende na kwa wenzangu. Nitoe rai kwamba pale ambapo tunakuwa na Ofisi za Wabunge, sisi ni wawakilishi wa watu, ziwe karibu na wananchi. Kwa sababu pale zinapowekwa kwa mfano kwenye Maboma ha hizi Wilaya mpya, mara nyingi ni nje ya mji kabisa. Kwa hiyo, unakuwa kidogo mbali sana na wapiga kura wako.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninashauri labda kwa sehemu nyingine basi, Ofisi hizi ziweze kuwa karibu kidogo na wananchi hata kama ni mjini katikati.

Mheshimiwa Spika, la pili ninataka kulizungumzia, tukisema haki za Bunge kwa tafsiri yangu mimi naweza pia nikakoselewa, lakini naomba niseme tu yale ambayo nayafikiria. Bunge kama muhimili mmojawapo wa Serikali, mimi nadhani tuna haja kabisa na haki kabisa ya kuzungumzia pia haki ya kiongozi wa muhimili huu. Kwa mfano kwenye Bunge ni Spika na nakusudia kuongelea haki za Spika na pengine sijui kama ndiyo Kamati hii hata kama siyo hii ila nadhani naweza nikasema mahali hapa.

Mheshimiwa Spika, wakati mwengine inasikitisha sana, unakuta kuna msafara wa kwenda sehemu fulani, gari ya Spika ikiwa inapeperushwa Bendera imesimama kwenye foleni inasubiri. Tatizo anakuwa hana *escort*. *(Makofi)*

Mimi nadhani Spika ana kila haki kama kiongozi wa muhimu na yeye kupata *escort* sio tu kwenda kwenye misafara mikuu, lakini nadhani kama viongozi wa mihimili mingine wanavyopata, basi na yeye aweze kupatiwa *escort* hiyo na pale anapo-Kaimu Naibu Spika pia na yeye aweze kupatiwa.

Lakini lingine, pia nilibahatika kipindi kimoja kusafiri na Mheshimiwa Spika. Niwe muwazi tu maana yake huwa napenda kusema kitu cha uhakika. Tukaenda Abuja kwenye Mkutano wa *CPA*. Maspika wengine waliokuja walivyokuwa wanapokelewa utashangaa. Spika wetu ilikuwa inabidi nimwambie Mzee, wewe kaa tu. Anakaa kwenye yale Mabenchi ya Chuma tunapanga naye foleni. Nadhani kuna haja itifaki ya huu muhimili wa Bunge iweze kuangaliwa pengine na Kamati hii au na wengine.

Lakini haki hiyo kwa kweli inakiukwa. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vyema kabisa tuangalie itifaki hiyo na sio hapo tu. Nitoe mfano wa karibuni ambao ni hai sana ambao wengi ulituumiza katika Kikao hiki. Hivi majuzi tulivyokwenda kwenye Hitima ya Marehemu Mpendwa wetu Mheshimiwa Akukweti, wakati wa kuchukua chakula, viongozi wengine walipokelewa sahani, lakini ilisikitisha kuona Spika kabeba sahani yake mwenyewe mpaka sehemu ya kukaa. Wote waliokuwepo walitizama chini. Sisemi nataka kumpa utukufu lakini nadhani ni stahili yake kama kiongozi wa muhimili.

Lingine pia ambalo nataka kulisemea, nadhani mtashangaa kwanini nang'ang'ania kwenye hili, lakini kwa kweli tunaposafiri ninaona hili mara nyingi. Sijui kama wenzangu mmepata bahati ya kukaribishwa nyumbani kwa Spika Dar es Salaam au Dodoma, kama kiongozi wa muhimili, kwa kweli mimi nilikuwa nasema, haki hapa haijatendeka. Naomba kabisa haki hii iweze kutendeka ili Spika awe na nyumba kwa sababu pia anakuwa na wageni wa nje, anakuwa na dhifa mbalimbali ambapo na sisi kama Bunge tuweze kujivunia. Kwa hiyo, hilo suala la nyumba nilikuwa naomba sana liangaliwe. Kwa wale ambao hamjafika, jaribuni hata kumtembelea hata hapa Dodoma halafu mtaelewa ninachokisema.

Lakini lingine la mwisho ni kuhusu Kiongozi huyu wa muhimili huu wa tatu. Spika anapokuwa Jimboni havui Uspika, bado anakuwa ni Spika. Je, tuliwahi kuwaza Ofisi yake kule Jimboni inafananaje? Wanapokuja wageni wakalazimika wakasema lazima tukamwone Spika inabidi tumwone wanakwenda kule, Ofisi yake inaeleweka? Maana yake nyumbani anaweza asiwapeleke, hiyo ni juu yake, lakini nadhani ni haki kabisa Ofisi yake kwenye Jimbo nayo iangaliwe iwe na hadhi. Ili hata sisi tunapokwenda pale tujue kwa kweli inastahili.

Ninakumbuka kuna kipindi fulani tulikuwa na masuala ya haraka akabidi afanye kazi ya Uspika akiwa kule kule Jimboni. Sasa ndugu zangu fikirieni, una kazi, una ofisi ya chumba kidogo na kadhalika. Kwa hiyo, yote haya nimeona katika Kamati hii pengine mkaelewa kwamba pamoja na haki za Bunge ni pamoja na haki za Spika kama Kiongozi wa Wabunge.

Mheshimjiwa Spika, lakini la mwisho kabisa nilikuwa nataka kusemea itifaki kwenye Wilaya zetu. Kwa kweli panakuwa na utata sana panapofika nafasi ya Mbunge katika Wilaya yake hasa panapokuja ugeni. Kwa kweli mara nyingi unakuwa huelewi itifaki imekaakaa vipi. Mimi siku hizi kwangu nimeamua kukaa nyuma kabisa, kwa sababu kwa kweli hatuelewi inakwendaje. Nadhani hili ni suala la muhimu kama haki

yetu sisi Wabunge tunapokuwa kule hatusemi kwamba tupewe labda utukufu fulani tupelekwe hapa. Tunachotaka kusema tu, ieleweke nafasi yako ni ipi ndani ya Jimbo, unatakiwa ufanye nini kwa wakati gani na kwa ugeni wa aina gani.

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee tena kupongeza sana Kamati hii na kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi na nilitaka kusema haya kwa sababu nilidhani hutakuwa kwenye Kiti leo, ndiyo maana nimesema haya kwa sababu nilikuwa nimeshaleta karatasi ya kuchangia, basi imebidi niyaseme mbele yako. Nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ahsante sana na hakika umezungumzia Ofisi, kwa sababu Ofisi ya Spika inadumu, imo kwenye Katiba. Ahsante sana.

Sasa namwita msemaji wa mwisho, Mheshimiwa Kabwe Zitto karibu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia taarifa hii ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ya mwaka 2006 kufuatana na kazi ambazo Kamati hii imezifanya mwaka 2006; na kwa kweli nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu kujikita sana katika Taarifa ya Kamati yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ina *instrument* kuu tatu za kufanyia kazi. *Instrument* ya kwanza ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya nane ambayo inaelezea kwamba Serikali yote inapata Mamlaka kutoka kwa wananchi. Ibara ya 100 ambayo inaelezea Kinga ya Bunge kwamba ni Taasisi huru na Ibara ya 62 na vipengele vyake vidogo ambayo inaelezea majukumu gani ambayo Bunge inayafanya.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa tatu wa hii taarifa nimeona majukumu ambayo wamepewa kama jinsi ambavyo Mwenyekiti kwamba wamepewa na Kanuni za Bunge kwanza kuchunguza masuala yote yanayohusu haki, kinga na madaraka ya Bunge yanayopelekwa kwake na Spika.

Pili, kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge. Tatu, kufikiria jambo lingine lolote litakalopelekwa kwake na Spika. Pamoja na kwamba haya ndiyo majukumu ambayo Kamati hii imepewa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, lakini kwa kweli haya majukumu ni dhaifu mno kwa sababu Kamati hii lengo lake hasa ni kusimamia *independence* ya Bunge. Matokeo yake Kamati hii kwa kiasi kikubwa na hata ukiangalia taarifa yake imekuwa kama Mahakama fulani hivi ndogo ya Bunge kitu ambacho naamini kabisa kinapunguza umuhimu wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, tukipiga kura za maoni leo kuuliza wananchi ni Kamati gani ya Bunge ambayo ni *the most hated* itakuwa ni Kamati hii. Kwa sababu inaonekana ni Kamati ambayo imekaa kikesi kesi. Hata ukisoma taarifa yake wanajisema kabisa kwamba wao ni kama Mahakama ingawa sio Mahakama kitu ambacho nakiona kwamba sio sahihi.

Lakini kazi kubwa sana ya Kamati hii ni kusimamia uhuru wa Bunge, kusimamia Sheria namba tatu ambayo ndiyo inaelezea suala zima la uhuru Bunge na kusimamia

utekelezaji wa Kanuni za Bunge na wala sio Kamati ya kusubiri kupelekewa kazi na Spika, ni Kamati ya kuweza kuangalia kwamba ni jinsi gani ambavyo Bunge linakuwa huru. Sasa hayo nitakuja kuelezea kwa mifano moja baada moja.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia baada ya huo utangulizi ni suala zima la kwamba Kamati hii ni chombo kinachojihusisha na utoaji haki. Hii sio sahihi na sio sahihi hata kidogo na ningependa kwa kweli taarifa hii ya Kamati iweze kurekebisha. Kamati hii haihusiki kabisa na suala la utoaji wa haki.

Mheshimiwa Spika, kamati hii inahusika na usimamiaji wa uhuru wa Bunge, basi. Kwa hiyo, hata kama tukisema tueleze dhumuni moja la Kamati hii ni hilo tu, sio suala la utoaji haki. Maana nimeona mpaka wamekwenda kutembelea Mahakama, wamejifunza kazi za Majaji, mimi naona kabisa ni vitu ambavyo wala havikutakiwa kuwepo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja wa Wabunge ambao nimebahatika kupata safari mbalimbali ambazo zinatokana na Bunge na ningependa ku-*sight* mifano miwili ya safari ambazo nilizifanya.

Mheshimiwa Spika, moja ya safari ni safari tuliyokwenda Canada kwa ajili ya kuangalia jinsi gani ambavyo Bunge la Canada linafanya kazi yake na vilevile nilifanya safari ya kwenda Uingereza kupitia *Common Wealth Parliamentary Association* ambayo tulikuwa tunaangalia jinsi gani ya ku-*restore trust* kwenye *political processes* na moja ya taarifa ambayo tulikuwa tunapewa katika hizo safari zote ni jinsi gani *independence* ya Bunge ipo na jinsi gani ambavyo Kamati ya Maadili au Kamati ya Kinga za Bunge inafanya kazi zake.

Nilipokuwa Uingereza wakati ule Kamishna wa Maadili wa Bunge la Uingereza alivyokuwa anafanya *presentation* yake na majukumu ya kazi ya Kamati ya Maadili nilijaribu kufumba macho na kuiangalia Kamati yetu ya Kinga za Bunge na nikalinganisha na ile *presentation* ambayo alikuwa anafanya yule Kamishna wa Bunge la Uingereza, nikasema kabisa kwamba hii Kamati yetu ni *nothing*. Kwa sababu kimsingi kabisa zile kazi ambazo walitakiwa kuzifanya kwa kweli hazifanyiki.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Mabunge yote hayo mawili na baadaye katika tafiti zangu nikagundua kuwa na Bunge la New Zealand na Bunge la Australia vile vile ni kwamba moja ya Kamati *senior* katika Kamati za Mabunge hayo ni Kamati hii ya Kinga. Ni Kamati nzito sana ni Kamati kubwa sana na hata Wajumbe wake sio tu Wajumbe ilimradi kuwa Wajumbe.

Kwa mfano, katika Bunge la Uingereza, Australia na Bunge la Canada, Wajumbe wa Kamati ya Maadili ni *Senior Parliamentarians*. Watu ambao wamekaa ndani ya Bunge zaidi ya vipindi vitatu na watu ambao *either* ni *Former Cabinet Minister* kwa mfano Mwenyekiti wa sasa wa Kamati ya Maadili ya Bunge la Uingereza ni *Former Cabinet Minister* na baadhi ya Wajumbe wengine. Lakini vilevile kitu ambacho naamini hata hapa kimezingatiwa ni suala zima la ujumbe ule kuzingatia uwakilishi wa vyama ambao sina tatizo na hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini Kamati yetu kwa mfano ukiangalia katika Wajumbe hao kumi na tano, Wajumbe wanne ni Wabunge wapya ambao hata huo muda wa kuzifahamu na kuzielewa Kanuni, Sheria na hata hizo *Power* za Bunge haupo.

Bahati nzuri Wabunge karibia wote ni rafiki zangu kwa hiyo, hata sioni haya kuwazungumza. Mheshimiwa Maneno, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Ngeleja ambaye sasa hivi ni Naibu Waziri na Mheshimiwa Ole Sendeka. Wote ni Wajumbe wapya.

Kwa hiyo, hata unakuta ule umuhimu wa uzito wa Kamati yenyewe unakuwa ni mdogo. Hawa wenzetu kwanini waliweka *Senior Parliamentarians?* Ni kwa sababu ya ule umuhimu wa Kamati hii. Kwa sababu hii ndiyo Kamati *Senior* kuliko Kamati zote. Kwa hiyo, mimi kwa kweli ningependa tulione hilo pia katika upande wa Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nilikuwa napenda kulichangia ni suala zima la Kamati hii kusimamia shughuli za Ofisi za Wabunge. Hili ni suala la *administrative,* sio suala linalohusu kinga ya Bunge, sio suala linalohusu haki za Bunge, wala sii suala linalohusu *privilege* za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kusimamia Ofisi za Wabunge *if so far* tunahitaji chombo cha Bunge kuweza kusimamia ni kazi ya Tume ya Bunge sio kazi ya Kamati ya Kinga. Kazi ya Kamati ya Kinga ni kuangalia jinsi gani ambavyo *independence* ya Bunge haiingiliwi.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Tume ya Huduma za Bunge kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Bunge ndiyo inapasa kushughulikia suala zima la haya maofisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi sijui ni kwanini Kamati hii inafikiria kwamba inayo hiyo haki! Kwa sababu mimi sioni kama hapo ni suala la haki *or else* labda ni masuala ya kupata safari za kwenda kwenye Majimbo. Ndiyo kitu ambacho mimi nakiona hapa na mimi *I am very honest* na mara nyingi nazungumza *mind* yangu.

Mimi nadhani sioni umuhimu wowote wa Kamati hii kushughulikia Ofisi za Wabunge kwa sababu hili suala haliathiri uhuru wa Bunge. Kazi hii kama tunahitaji chombo cha Bunge cha kulishughulikia ni Tume ya Huduma za Bunge na kwamba shughuli zote za Ofisi za Wabunge ziwe chini ya Ofisi ya Katibu wa Bunge. Yaani zishughulikiwe ndani ya *umbrella* ya Bunge isiwe nje ya *umbrella* ya Bunge.

Kwa hiyo, isiende kuwa kwa Wakuu wa Wilaya wala kwa Wakurugenzi, ziwe ni shughuli ambazo zinashughulikiwa na Ofisi wa Katibu wa Bunge na masuala yote yanayohusiana na Ofisi za Wabunge kule chini zishughulikiwe na Katibu wa Bunge. Lakini vilevile kama *supervisory organ* iwe ni Tume ya Huduma za Bunge.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wajumbe wa hii Kamati, hili suala wala wasilizungumzie tena kwa sababu sioni kama lina uhusiano wowote na uhuru wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina tatizo. Kuna mapendekezo kadhaa ambayo Kamati imeyazungumza ikiwemo kwa ajili ya kufanya ziara za mafunzo na mambo kama haya. Ndiyo maana Mabunge ya wenzetu moja ya *condition* ya mtu kuwa Mjumbe wa Kamati kama hii ni kuwa *Senior Parliamentarian* kwa sababu tayari unakuwa na uzoefu.

Hili suala la kuchukua *junior MP's* kuwaingiza kwenye Kamati kama hii ndiyo mambo kama haya ya kutaka mafunzo na haya mafunzo sio bure, haya mafunzo ni fedha na tayari ni lazima tuangalie ni jinsi gani ambavyo tunadhibiti matumizi ya pesa zetu.

Kwa hiyo, kwa kumalizia na nitaomba radhi sana kwa Wajumbe wa Kamati hii katika hili. Mimi kwa kweli binafsi kama Mbunge siridhiki kabisa na huduma ya Kamati hii, yaani siridhiki na kazi ambazo Kamati hii inafanya na kwa kweli kama mimi leo ndiyo nakuwa Spika hii Kamati ningeiunda upya. Nazungumzia hisia zangu binafsi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto kaa chini. Unakaribia kabisa sasa kumkosoa Spika. Wewe kwanza unasema hawa wengine wadogo wewe ni mdogo kama wao, halafu sasa unaota ndoto za Uspika wewe huoni kama unajichanganya kabisa. Wewe ungekuwa Spika leo, utakuwaje Spika leo wewe? *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, rejea kwenye Kanuni, ni marufuku kuujadili mwenendo wa Spika ndani ya Bunge na pili nikufahamishe basi utamaduni wa Afrika na hasa Tanzania ni mfano mzuri na hao unaowataja Canada sijui nani hao waje wajifunze.

Sisi tunachanganya vizazi kadhaa pamoja ndani ya Kamati ili tuweze kurithisha uzoefu na hekima kwa hao. Hao ma-*Mabinet Ministers* umewataja wapo; Mheshimiwa Masilingi, Mheshimiwa Anna Abdallah, wakina Janguo wakina nani, kwa hiyo, wamo. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa sisi tunaomba uwafahamishe hao rafiki zako Canada na Uingereza waje wajifunze sisi tunavyochanganya uzoefu. Haya endelea sasa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi kama nimeanza kuingilia nafasi ya Spika na uhuru wa Spika. Sikuwa na lengo hilo, nilikuwa najaribu tu kutoa *experiences* mbali mbali. Lakini pia nakubaliana nawe kuwa ni vizuri kuchanganya vizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na naamini kuwa muda wangu ambao umeuchukua utaufidia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kupendekeza kwamba, naomba Kamati hii ijikite sana katika kuangalia ni jinsi gani ambavyo haki za Bunge zinaingiliwa yaani katika kuhakikisha kwamba vipengele vile vya Katiba ambavyo vinataja Bunge na vipengele vya Sheria Na. 3 vyote, kwa sababu vyote vinahusiana na Bunge, jinsi gani ambavyo haviingiliwi. Ningependa kuona kwa kweli kwamba Kamati yenyewe inachukua *initiative* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uhuru wa Bunge unazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna vitu ni lazima wapewe maelekezo na kiti, lazima wapewe maelekezo na Spika, lakini kuna mambo ambayo kwa kweli unayaona na mimi nitakupa mfano, jana Gazeti la Rai lilikuwa na kichwa cha habari kinachozungumzia

kwamba Mkurugenzi wa *PCB* amesema kwamba chombo kama Bunge kisiingilie kazi za *PCB*. Walikuwa wanazungumzia hilo kuhusiana na masuala ya *investigation* za Rada na *investigataion* za Kampuni ya *Richmond* ambayo imekuwa ikizungumzwa sana. Kwa hiyo, Mkurugenzi wa *PCB* akawa *quoted* kwenye Gazeti la Rai akisema kwamba Wabunge hawana haki ya kuzungumza hili kwa sababu linachunguzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kile kitu mimi ilinikera sana kwa sababu nikaona kwamba sisi tuna uhuru wa kuzungumza chochote kile, isipokuwa tu yale mambo ambayo yako Mahakamani. Mambo ambayo yanachunguzwa ni mambo ambayo yanachunguzwa, *PCB* wanaweza wakafanya hivyo, lakini pia sisi tunao uwezo. Mfano hii Kamati ya Haki na Maadili inao uwezo wa kumwita Mkurugenzi wa *PCB* na kumhoji kwa masuala mbali mbali ya utendaji na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kile kitu kilinikera sana, lakini baadae nika-*cross check* na watu wa *PCB,* nikagundua kwamba Mkurugenzi wa *PCB* hakuzungumza hayo maneno, hayo maneno amewekewa kinywani na waandishi wa habari. Kwa hiyo, kitu kama hiki hakihitaji Mwenyekiti wa Kamati ya Haki na Maadili ya Bunge aambiwe na Spika kukifuatilia. Kitu kama hiki Mwenyekiti anatakiwa kuchukua *initiative,* kuripoti kwa Spika na kuweza kuita wahusika kwa sababu ni kuingilia uhuru wa Bunge. Ningependa kuona Kamati inayofanya kazi namna hiyo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uhuru wa Bunge unaheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo ndiyo mambo ambayo nilikuwa napenda kuona yanafanywa na vile vile kuna masuala kama kwa mfano Wabunge wakihisi, labda Serikali inawaingilia na katika hili kwa kweli, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli ambayo ametoka kuizungumza sasa hivi ambayo inaongeza ile *independence* ya Bunge. Kwa kweli nimpongeze sana, maana yake Mzee Cheyo hakupata nafasi ya kusimama tena, naamini kabisa angeweza kumpongeza. Kwa niaba yake, mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tuweze kuangalia kwa sababu tupo kwenye mabadiliko ya Kanuni za Bunge, masuala kama haya yanayohusiana na kazi za Kamati nyeti kama hii yaangaliwe upya ili Kamati hii isionekane ni kamahakama kadogo. Sisemi hivi ka sababu mimi ni mmoja wa watu ambao wamehojiwa na Kamati, kwa sababu walikuwa wanatekeleza kazi yao, wamepewa maelekezo na Spika. Lakini isionekane kwamba kila mwaka katika kazi za Kamati wanaleta kesi hii, kesi hii, kesi hii. *No!* Waonyeshe ni jinsi gani ambavyo uhuru wa Bunge unazidi kuongezeka, waonyeshe jinsi gani ambavyo wameshughulikia masuala ambayo yanaingilia uhuru wa Bunge. Hayo ndiyo mambo ambayo nilikuwa napenda niyaone katika ripoti hii ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mengine ambayo nilikuwa nataka kuyasema, umeya-*pre-empt* kwa *intervention* yako na naomba kwa kweli nisiyaseme kwa heshima ya kiti na kwa sababu katika maelezo yako nimeweza kupata ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo naomba nimalizie kwa kuiomba Kamati hii izitumie *instruments* tatu muhimu kwenye kazi yake ambazo ni Kanuni za Bunge, Sheria Na. 3 na Katiba ya nchi Ibara ya 8, Ibara ya 100 na Ibara ya 63.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabwe Zitto, ahsante sana na kwa taarifa ya Wabunge wote ni kwamba Kamati ya Kanuni inaendelea na kazi yake na hata siku ya Jumanne na Jumatano tutakuwa hapa tunaendelea na kazi na mengi haya tunayazingatia. Sasa ni zamu ya Mtoa Hoja, Mheshimiwa Athumani Janguo, ametoka!

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nimeamua kurudi kwenye kiti changu, nitajibu kuanzia hapa ukiniruhusu! *(Makofi)*

**SPIKA:** Ni vema, karibu! Sawa kabisa!

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya pili tena ya kuweza kufanya mapitio ya michango ya Waheshimiwa Wabunge mbali mbali na ningependa niwatambue Waheshimiwa ambao wamechangia katika hoja hii.

Kwanza, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Kabwe Zitto na kwa mara ya kwanza kabisa, Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninamshukuru sana kwa kuingilia kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nitakuwa sijakutendea haki kwa kuwa na wewe umeweza kuingilia kati na ukachangia yale ambayo kwa kweli nilikuwa tayari niyachangie. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu...

**SPIKA:** Mheshimiwa, kaa chini! Mimi nilikuwa sichangii. Mimi naongoza tu utaratibu na kusahihisha pale ambapo pana kasoro. Nisije nikaeleweka kwenye *Hansard* kwamba Spika naye alisimama kuchangia! Endelea! *(Kcheko)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru! Ninafuta usemi wangu, bali nasema umetusaidia kwa kutoa ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu nakubaliana na mengi ambayo ameyasema Mheshimiwa John Cheyo na pale ambapo kidogo alikwenda nje, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa ufafanuzi mzuri sana na nadhani mengi yameeleweka. Lakini, kubwa alilokuwa akisema tu, ni kwamba alikuwa anataka aone Bunge limechukua nafasi yake na Kamati yangu inakubaliana naye kwenye maoni haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, yale yote ambayo yamesemwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na namshukuru sana kwa kutetea haki za Bunge, kutetea haki za Kiongozi wa Bunge, Mheshimiwa Spika wetu na kutetea haki za Wabunge hasa kule Majimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi nilipata nafasi ya kusafiri na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo katika ile Kamati ambayo uliiteua kwa ajili ya kuangalia upya kanuni na kila mahala alipokwenda, alikuwa kweli akiliwakilisha Bunge na alikuwa akitetea sana viongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya ofisi za Wabunge, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na wengine wote kwamba tukipata nafasi tutatembelea ofisi zilizokuwa zimetengenezwa vizuri na zile mbaya ili kusudi tuweze kuishauri Serikali vizuri pale inapowezekana na hapa sikubaliani na Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba hii siyo kazi ya Wabunge. Sasa tukizungumzia haki za Wabunge, ni pamoja na mambo ambayo wanatakiwa wawe nayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii ya kuangalia masuala ya Wabunge iko katika Kamati tatu, nikitaja tatu tu ambazo nyingi nimehusika nazo ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Tume ya Bunge yenyewe na Kamati hii ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge nazo zinaangalia baadhi ya mambo ambayo yanahusu haki za Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kugeuza taarifa yangu kuwa mabishano na Mheshimiwa Kabwe Zitto. Mheshimiwa Kabwe Zitto, ni mmoja wa Wabunge waliowahi kutokea mbele ya Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nisingemtegemea yeye aseme mazuri sana juu ya Kamati hii na tulipokutana naye, kwa kweli kulikuwa na *fracas* pale. Lakini ilibidi tutumie hekima na kumuonyesha bado yeye mdogo na kuna wakubwa ndani ya Kamati ile. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto ametaja Ibara ya 8, ya 10 na 63. Kwa kweli Kamati yangu inazipitia vizuri sana hizi na inajua nini maana yake. Lakini anasema Kamati hii imekaa kikesi kikesi. Kama unataka kutoa haki, utaifanyaje haki bila kujua angalau hata zile *elements* za kesi. Kwa hiyo, tutake tusitake, Kamati hii itakuwa inaangalia masuala ambayo yamekaa kikesi kesi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie moja tu. Nilisema umetusaidia sana kwa ufafanuzi. Hili, mimi nataka nikusifu sana jinsi ulivyoweza kuteua Kamati hii ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Tuna Wabunge ambao wamekaa miaka mingi sana ambao ni Mheshimiwa Anna Abdallah, hiki sasa ni kipindi chake cha saba na alikuwa Waziri katika Wizara mbali mbali katika Tanzania, Mwenyekiti wetu, hiki ni kipindi chake cha tano, mimi ninayesoma hapa hiki ni kipindi changu cha tatu na tuna wajumbe kama Mheshimiwa Haroub Said Masoud, hiki ni kipindi chake cha tatu na tuna wanasheria humo ndani na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ulivyofafanua ni kwamba shabaha ya Bunge hili ili liendelee vizuri, wale vijana na wao waanze kuingia mapema ili wajifunze kutoka kwetu wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto, anazungumza habari ya kwenda Uingereza, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa *CPA* kwa miaka isiyopungua sita, nimeshakwenda Uingereza zaidi ya mara tatu na hao aliokutana nao, nimekutana nao. Lakini, asije yeye akawa ameenda mara moja tu halafu akafikiri kajifunza mambo yote ya Uingereza! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kuendeleza sana, lakini nataka nieleze tu kwamba aliyoyasema tumeyasikia. Yale ambayo yatakuwa na manufaa kwa Bunge hili, Kamati yangu itayazingatia na yale ambayo tunaona kwamba lazima ajifunze, basi tutaendelea kumuelimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushuru, ahsante na baada ya hapo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liikubali na kuipokea ripoti ya Kamati hii pamoja na mapendekezo yake ili iweze kupitishwa katika Bunge lako. Nakushukuru, ahsante! Naomba kutoa hoja!

**SPIKA:** Mheshimiwa Athumani Janguo, ahsante kwa ufafanuzi huo! Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu ni kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hiyo.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## HOJA ZA WABUNGE

## AZIMIO

### Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Rais Kuhusu Hatua Yake ya Kuiita Serikali ili Kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2006

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 23(5) ya Kanuni za Bunge, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Rais kuhusu hatua aliyochukua ya kuiita Serikali ili kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mnamo tarehe 15 Aprili, 2007 Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania aliitisha Kikao Maalum cha Viongozi Wakuu wa Serikali kwa kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Taifa ili kujadili Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kwa Mheshimiwa Rais kuitisha Kikao Maalum cha Viongozi wote wa Serikali kujadili na kutoa malekezo ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Ni mara ya kwanza pia, kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kukamilisha na kuwasilisha Taarifa yake ya Ukaguzi kwa wakati. Siku za nyuma taarifa hizi zilikuwa zikichelewa kukamilishwa na kuwasilishwa Bungeni, jambo ambalo liliwanyima Waheshimiwa Wabunge nafasi ya kuzipitia, kuzijadili na kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Serikali kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua aliyochukua Mheshimiwa Rais inatekeleza Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayosema: “Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa

Hesabu atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii. Baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye Kikao cha Kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho...”

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya kazi za Bunge kama zilivyotamkwa katika Ibara ya 63(2) kinasema: “... Bunge litakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.”

Mheshimiwa Spika, hatua hii ya Mheshimiwa Rais ya kuwataka Viongozi Wakuu wa ngazi zote katika kusimamia fedha za umma kwa manufaa ya wananchi wawajibike, italeta mabadiliko makubwa na kuimarisha majukumu na kazi za Kamati za Bunge na Bunge kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono dhamira na juhudi za Mheshimiwa Rais, watumishi wa Serikali wenye dhamana ya kusimamia matumizi ya fedha za umma wanawajibika kuzingatia mambo muhimu yafuatayo kwanza, kuzuia matumizi yasiyo na faida kwa umma, pili, kuongeza bidii ya ukusanyaji wa mapato na tatu, kukomesha uzembe, ukiukwaji wa sheria na kanuni za fedha pamoja na kutokomeza rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati za Bunge ni vyombo muhimu kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyoainishwa hapo juu, Bunge lihakikishe kuwa Kamati za Bunge zinawezeshwa kikamilifu ili zitekeleze majukumu yake ipasavyo sanjari na dhamira iliyoonyeshwa na Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninayo heshima ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio lifuatalo:-

KWA KUWA Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inamtaka Rais kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kikao chake cha kwanza mara tu baada ya kuipokea;

NA KWA KUWA ni mara ya kwanza kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kuwasilisha Taarifa yake kwa wakati, na kwa kuwa Rais aliwasilisha Taarifa hiyo Bungeni kwa taratibu zinazotakiwa kwa wakati;

NA KWA KUWA baada ya kujadili Taarifa hiyo Bungeni, Mheshimiwa Rais aliitisha Mkutano wa Watendaji wote Wakuu wa Serikali wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara zinazojitegemea, Naibu Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wahasibu Wakuu, kujadili kasoro zilizobainishwa katika ripoti hiyo kwa lengo la kuwakumbusha na kuwaelekeza wajibu wao katika jukumu la kusimamia kikamilifu fedha za Serikali kwa manufaa ya wananchi;

NA KWA KUWA hatua hii inaimarisha zaidi na kuchukulia maanani kilio cha Waheshimiwa Wabunge kuhusu nia ya kuwepo kwa utaratibu mzuri wa Serikali wa

kudhibiti fedha za umma kutokana na kasoro ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara wakati wa mjadala Bungeni;

NA KWA KUWA hii ni mara ya kwanza katika nchi yetu kwa Rais wa nchi kuitisha mkutano wa aina hii ili kujadili ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, jambo linaloonyesha dhamira madhubuti ya Rais katika kuhakikisha kunakuwepo uwajibikaji na nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali;

KWA HIYO BASI Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililoanza tarehe 10 Aprili, 2007 na linaloendelea na Mkutano wake wa Saba hapa Dodoma, linapokea na kukubali pendekezo la kutoa pongezi maalum kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwanza kwa kuiwasilisha Bungeni Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati; na pia kwa kuitisha Mkutano wa Watendaji Wakuu wa Serikali na kutoa maelekezo ya uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe na Rais wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo jopo zito hapa la wachangiaji, idadi yao ni sita. Sasa kwa sababu jambo hili lipo wazi kabisa lakini pia kwa kutambua uwakilishi wa jopo hili nitakalolitaja, nawapa dakika tano, tano tu kusema kitu kimoja, tumalize ndani ya nusu saa. Nadhani inakubalika.

Jopo, langu ni Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa *PAC,* Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni *Presiding Officer*, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Wilson Masilingi, ni *Senator* huyu, ni Mbunge mashuhuri, Mheshimiwa Kabwe Zitto, ni kijana, lakini kwa utaratibu wangu ule ule namchanganya humo humo na tutahitimisha na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. Naanza na Mheshimiwa John Cheyo, dakika zisizozidi tano, ukisema kwa dakika tatu vizuri zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi nasimama hapa kuunga mkono Azimio la kumpongeza Rais kwa kuchukua hatua ambayo haijachukuliwa katika dunia nzima ya kuita Serikali yote kuzungumzia utendaji wa Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kuja na kuizungumza Serikali yake juu ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, anathibitisha kwamba analiunga mkono Bunge lako kwa mantiki kwamba sheria ya *Public Finance Act No.6(31)(1),* inasema kwa Kiingereza, nanukuu: *"The Controller and Auditor General shall on behalf of the National Assembly..." and I insist, "...on behalf of the National Assembly, examine, inquire into and audit the Accounts submitted to him under section 25 of this Act and perform any other functions which he is authorized to perform by/under this Act."*

Mheshimiwa Spika, ndio kusema ripoti hii ambayo Mheshimiwa Rais ameizungumza, ni ripoti ya Bunge hili kwa sababu Bunge hili ndiyo limepewa majukumu

ya kuweza kuidhibiti Serikali na mambo ya *audit* yanafanywa kwa niaba ya Bunge hili. Kwa hiyo, yeye kuweza kulichukulia jambo hili maanani, amelipa Bunge hili nguvu ya kuwasimamia Ma-*Accounting Officers*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wito wangu ni kwamba, kwa kitendo hiki cha Mheshimiwa Rais, basi Maafisa Wahasibu wote wanaotokea mbele ya Kamati ya *PAC* na ya *LAAC,* wayachukulie yale maagizo ambayo yanatolewa na Kamati hizi kwa umuhimu ule ule ambao Mheshimiwa Rais ameuonyesha anataka yachukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii inapokea misaada mingi sana kutoka sehemu mbalimbali na hizo fedha siyo za mtu binafsi, ni fedha ambazo zinaidhinishwa na Mabunge mbalimbali ya nchi mbalimbali. Mabunge hayo yanategemea sana uwezo wa Bunge hili na uhakika kwamba Bunge hili litaangalia fedha ambazo zinatolewa na Bunge hili, litathibitisha kwamba fedha hizi zimetumika vizuri kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo, sisi kuweza kuchukulia kwamba hii ripoti ni yetu, hii inaleta *confidence* au inaleta watu kuamini kwamba hata wakileta pesa zao kwa mkondo ambao sasa hivi Serikali yetu inaujenga wa *General Budget Support,* Bunge ambalo litahakikisha kwamba vitabu vimekaguliwa vizuri na kwamba wale ambao wamechezea chezea fedha za Serikali, wataweza kudhibitiwa vizuri na kuadhibiwa inavyopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka kutoa mwito katika mlolongo wote huu, kuna zaifu mbili, kwanza, tungependa kuona kwamba kama vile sheria inavyosema, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, asogee zaidi Bungeni kuliko kusogea upande wa Serikali ili ile dhana kwamba anafanya kazi hii kwa niaba ya Bunge, ionekane bayana kwa watu wote. Hilo ombi langu la kwanza.

Ombi la pili, ningependa kuona kwamba zile adhabu ambazo zimetajwa kwa Maafisa Wahasibu ambao ni wadhaifu, hazitoshi! Ni vizuri mtu unamwambia kwamba utamkata mshahara asilimia 10. Mishahara yetu tunaijua ni duni, ndio maana watu wanakuwa hawahamasiki kuangalia fedha za Serikali kwa sababu anajua adhabu yenyewe tozo la asilimia 10, ni kitu gani ! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni sawa sawa na yule mtu anayechukua *imprest* ya milioni 350 ambao wengine tumewagundua halafu anakubaliwa atalipa shilingi 10,000 kila mwezi kwa sababu mshahara haukubali akakatwe zaidi. Inamchukua miaka 350 kuweza kukatwa fedha kama hizo. Kwa hiyo, naomba Wizara na zaidi *Pay Master General* aangalie ni jinsi gani ataweza kudhibiti. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi uliyonipa. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuunga mkono azimio ambalo limeletwe leo mbele yetu. Nianze kwanza kwa kumpongeza sana *CAG* wetu kwa kutambua wajibu mkubwa aliopewa na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *CAG* ametekeleza wajibu wake kwa kufuata Katiba ya nchi, ibara ya 143(2) ambacho kinamtaka *CAG* kufanya mambo makubwa matatu. Lakini nitasisitiza mawili ambayo ni ya muhimu zaidi. Kwanza, anatakiwa yeye ahakikishe anaidhinisha fedha zote ambazo zimetakiwa ama zinatarajiwa kutumika na Serikali yetu katika nchi yetu ya Tanzania. Lakini vile vile *CAG* wetu anatakiwa ahakikishe kwamba fedha zilizopitishwa na kuidhinishwa na Bunge letu Tukufu zinafanya kazi iliyopangwa na kulingana na jinsi Bunge lilivyopitisha fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, *CAG* ametimiza wajibu wake na naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana. *CAG* ametusaidia, ameisaidia Serikali yetu, lakini ametusaidia hata sisi wawakilishi wa wananchi na watendaji wote kwa ujumla kutambua chanzo cha tatizo kubwa la kufujwa kwa fedha za Serikali katika nchi yetu ni nini? Uzuri ukigundua dalili za ugonjwa ni rahisi sana kuutibu ugonjwa huo. Kwa hiyo, changamoto kubwa iliyopo mbele yetu sasa ni kushirikiana sisi wote, Serikali, Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote ndani ya nchi yetu ya Tanzania, kuhakikisha kwamba tunamsaidia Mheshimiwa Rais katika azma yake kubwa aliyoionyesha mbele ya umma wa Watanzania safari hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kwamba kwa nini nimesimama kuunga mkono Azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais. Nimegundua kwamba Mheshimiwa Rais ametambua umuhimu wake kama Kiongozi Mkuu wa nchi wa kusimamia utawala bora wa wananchi wa Tanzania. Kwa kutambua haraka sana tatizo lililojitokeza katika nchi yetu. Lakini vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu si kwamba ametambua tu angeweza kutambua na akaamua kuendelea na utaratibu mwingine. Lakini mara baada ya kutambua, akachukua hatua za haraka sana. Kwa hiyo, ninaomba nimpongeze sana Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile hajaishia hapo alipochukua hatua za haraka ameleta changamoto ya utekelezaji wa kupambana na tatizo hilo kubwa la ufujaji wa fedha za Serikali. Fedha ni rasilimali kubwa katika kuleta maendeleo ya Watanzania na kuondoa tatizo la umaskini. Kama fedha zitaendelea kufujwa kwa kiasi kikubwa basi hatutafikia maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka usemi wa babu yangu. Aliniambia siku moja Jenista ukitaka kuona mbio za mzee fungua mbuzi wakale mihogo yake. Kwa hiyo, mimi nimegundua Mheshimiwa Rais, ametuonyesha mbio zake katika kusimamia maisha bora kwa Watanzania zikoje. Kwa hiyo, ninampongeza sana baada ya kusema hayo, changamoto kubwa imewekwa mbele yetu siyo sisi tu Waheshimiwa Wabunge kama chombo cha wananchi lakini na Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuunga mkono Azimio hili la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na tunamtakia kila la kheri katika kuonyesha uadilifu mkubwa kwa wananchi wa Tanzania. Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa sababu ya dakika tano nitazungumza kwa ufupi sana. *(Makofi)*

Kwanza, nami niungane na wenzangu kwanza kumshukuru Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, kwa kuleta Azimio hili na kwa kweli amefanya jambo la maana

sana. Lakini pili, kila Rais ana utaratibu wake. Mimi nilikuwa Mjumbe wa *PAC* mwaka 1978, mwalimu alikuwa akisoma taarifa za Mdhibiti Mkuu wa Serikali na akimaliza kusoma huwa vile vile anajitahidi kupitia Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali. Nakumbuka alichukua hatua haraka za kuwastafisha maafisa wa jeshi ambao walikuwa hawaguswi wakati huo kwa sababu ya ripoti ya taarifa ya Mdhibiti Mkuu na Kamati ya Hesabu za Serikali. Kwa hiyo, ninachojaribu kusema nasema kila mmoja ana *methodology* yake ya kufanyakazi. Rais Jakaya Kikwete, kaja na utaratibu mpya tuna upongeza sana ni wa wazi zaidi. *(Makofi)*

Sasa kinachotakiwa ni kuchukua hatua. Rais amewaita viongozi, Wakuu wa Serikali, ipo Katiba, ipo sheria, ziko taratibu wanazifahamu, wamezikiuka na ndiyo tuna matatizo haya na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, ndiyo akatoa taarifa yake. Ninachoomba sasa hatua inayofuata ni kuchukuliwa hatua madhubuti kwa wale ambao wamevunja taratibu za fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kazi hiyo ikamilike Bunge hili lina wajibu mkubwa sana kusaidia tatizo hili. Kwa sababu wahasibu wanatumia kalamu zao na karatasi zao. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali atakapokwenda kukagua mara ya pili atakuta *documents* zote zinazotakiwa zipo na kwa hiyo, atatoa shahada. Kitakachokosekana kinaitwa *performance auditing*. *Performance auditing* itaweza kufanywa na Bunge hili lako Tukufu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ushauri wangu ili ile kazi ya Rais aliyoitoa ya Rais kusimamia kwa upande wake na taarifa ambazo atazipata baadaye ni vizuri hili liwezeshwe kikamilifu. Namshukuru sana Waziri Mkuu kwa kusema kwamba Bunge sasa litakuwa na *independent budget* ya kuwezesha Bunge kufanya *performance auditing* ili kuweza kusimamia matumizi na mapato ya Serikali.

Kwa hiyo, nasema kwanza hatua hii aliyochukua Rais tunamshukuru sana ni hatua ya kwanza. Lakini vile vile wale anaowa-*point* yeye Rais akiona bado wanaendelea achukue hatua kama zile alizochukua akichukua Baba wa Taifa haraka sana wakati uchunguzi wa kesi unaendelea. Hiyo itasaidia sana kuweka *discipline* ya matumizi na mapato ya Serikali. Haya ya kuambiana tu na kuhimizana na kukumbushana wakati wake umeshapita sasa. Tunaendelea na umaskini, Watanzania bado wana matatizo lakini wenzetu wanavuna mali kwa makusudi hilo lilikuwa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ukitazama taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, mara nyingi tunazungumzia fedha. Lakini ukienda ukikagua vifaa ambavyo viko kwenye maghala ambavyo vimetupwa havina kazi yoyote watu hawajui na watu hawaoni kama zile ni fedha. Chombo ambacho kitasaidia kugundua hayo ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Kamati zake. Kwa hiyo, ningeomba vile vile ili kuisaidia Serikali, sisi Wabunge ni vizuri tutakapokwenda katika ziara mbalimbali za Kamati zetu tusaidie kuangalia vifaa vilivyonunuliwa na Serikali kama kweli vina thamani halisi na kama kweli vinatumika inavyotakiwa. Hiyo tutakuwa tumemuunga mkono Rais katika hatua zake. Vinginevyo kwa kupitishwa Azimio bila ya kwenda kufanyakazi kwenye *field* tukaangalia hasa bado hatujasaidia Serikali na hatujafanya wajibu wetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali isaidie Bunge lifanye kazi zake na Wabunge tuisaidie Serikali kwa kuchunguza yale maeneo ambayo *auditor* hakuweza kufika maana hawezi kufika kila mahali.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kweli amefanyakazi nzuri. Miaka yote tulikuwa tunakaa miaka miwili, mitatu ndiyo tunapata taarifa sasa tumepata taarifa kwa wakati. Nasema kunahitaji kupongezwa, kunahitaji kutoa moyo na kwa kweli wanahitaji sana kusaidiwa kufanyakazi zao. Tunaishauri Wizara ya Fedha inayosaidia sana idara hii washirikiane zaidi ili waweze kufanyakazi yao kwa ufanisi zaidi na waisaidie sana Kamati za Hesabu za Serikali na Kamati ya *LAAC* ambazo ndizo zenye majukumu makubwa sana ya kusimamia hasa haya mambo ya *auditing* ya Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika mjadala huu wa Azimio la Bunge na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya. Lakini kabla sijaendelea naomba nimpongeze Mheshimiwa Spika, umenipa sifa ambayo imekuwa nzito sana kuibeba. Kuniita *Senator,* nimekaa kwenye kiti hapa nikafikiria kujitoa katika kuchangia lakini nikaona muda hautoshi karatasi kukufikia. Maana yake baada ya kupewa sifa za u-*senator* halafu ukachangia ovyo. Ni sawa na fursa ya kufukuzwa kwenye u-*senator*. Kwa hiyo, mtanivumilia hili ni Azimio la Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunitia moyo. Muda ni mfupi napenda kuungana na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe na Rais wa Bunge la Afrika, kwa kuwa na wazo la kuleta Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais. Katika mila zetu za kabila langu tunalotoka tunasema ukikuta mtu analima ukimpita hivi hivi, humsaidii lakini ukimwambia pole na kazi hata kama akiondoka baada ya dakika tano wanasema umempa shime na kumtia moyo wa kufanyakazi. Anayejenga nyumba akaanza, akashindwa kumaliza naye ni mwanaume kwa sababu ana wazo la kujenga, ameanza akashindwa, naye ni mwanaume kama waliomaliza. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nimetoa mifano hiyo miwili Mheshimiwa Rais kwa kuwaita watendaji wake baada ya kupokea *surprise* ya *Controller and Auditor General* (Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali) kuleta taarifa kwa wakati hilo jambo la kwanza la kihistoria kwamba Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa ya hesabu za Serikali kwa wakati za mwaka jana. Ni miaka mitatu nyuma na kadhalika na mimi nimetoka kwenye Serikali.

Kwa hiyo, napenda kuungana na wenzangu waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa dhati kabisa ameitikia wito wa *Controller and Auditor General* lakini kuungana na wenzangu kumpongeza *Controller and Auditor General* kwa kufanyakazi vizuri na timu yake yote. Sasa mimi napendekeza *amendmenst* itoke *specifically* siyo kumpongeza tu kwenye *Hansard* kwenye Azimio hilo Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali *draft* ifanyike kadri inavyozungumza kwamba tunampongeza kwa kufanyakazi kwa bidii, kwa wakati na kuleta hesabu kwa wakati muafaka kinyume na huko nyuma. Kwa sababu ni chombo cha Kikatiba anaripoti kwetu. Hilo la kwanza na-*amend* hilo Azimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Bunge tuongeze kwenye *amendments* litenge muda katika kikao kinachokuja maana yake tunakuwa muda mfupi na sisi tukae na Mheshimiwa Rais alivyowaita watendaji wake, tuangalie taarifa hii maana yake imeletwa kwetu. Mheshimiwa Rais akaita watendaji hapa Dodoma kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa, sisi hatujakaa. Kwa hiyo, na sisi tuazimie kukaa hata kama ni siku mbili/tatu kabla ya Bajeti tutafakari haya yalimo ili tuweze kushauri. Hilo ni pendelezo la pili la ku-*amend* hilo Azimio. Isije ikaonekana sisi tunampongeza Rais kwa kufanyakazi yake nzuri ni kama mtu analima. Unamtia moyo afanye kazi anayopaswa kufanya lakini mwisho wa kazi ya Bunge, ni kumsimamia na Serikali yake hata aliyoyaagiza yatekelezwe kweli kweli. *(Makofi)*

La mwisho kusahisisha, si kweli na naungana na Mheshimiwa kwa mara ya pili, ana bahati huyu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani mara ya pili namuunga mkono na tena ni *CUF* si sahihi kwamba ni katika historia ya Tanzania, bahati nzuri na mtoa hoja Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, aliwahi kuwa Waziri. Marais si kuwa Waziri katika Serikali ya Awamu ya Kwanza na ya pili sijui wale walikuwa wanafanyaje. Lakini wenzangu na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulikuwa wote, *Controller and Auditor General Report* ni hoja ya kujadiliwa mbele ya *Cabinet* kwa hiyo, kusema ni mara ya kwanza kuita Serikali kujadili taarifa ya Mkaguzi wa Serikali katika historia ya nchi si sahihi irekebishwe na ifutwe kwenye Azimio.

Kama alivyosema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mwalimu Nyerere alikuwa na utaratibu wake. Kuna alivyokuwa anafanya hiyo si sahihi kufanya kitu kihistoria na katika dunia nzima Mheshimiwa John Cheyo, ametia chumvi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana, tumesikia. Waheshimiwa Wabunge, nisingependekeza tuendelea na vitu kama kubadilisha hii hoja. Kwanza inalenga kumpa shime Rais wetu, kumchanganya yeye na Mkaguzi hii si sahihi. Tunayo nafasi nzuri tu kwenye Mkutano wa Nane wa Bunge ambapo tutaijadili taarifa hii, pale tunaweza kumpongeza lakini kwa sasa na kwa kuzingatia na muda na uzito wa Azimio lenyewe ningefurahi kama lingebaki lilivyo na pia kwa kumsaidia Mheshimiwa Wilson Masilingi, ni mara ya kwanza kufanya hivi ilivyofanyika. Kuita *cabinet* sawa, lakini huyu kaita mpaka Wakaguzi wa Ndani, Ma-*RAS,* Wakuu wa Mikoa kwa mikutano ya pamoja hicho ndiyo tumekiona ni maalumu. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, na mimi pia niseme kwamba umenipa heshima kubwa sana kuweza kusimama na kuchangia Azimio hili na ni heshima zaidi pale ambapo wachangiaji hao sita karibuni wote ni *senior parliamentarians* na kwa kweli napata uzoefu kutokana na wao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, siku ya Jumapili mimi nilikuja hapa katika Ofisi za Bunge kufanyakazi zangu za kujiandaa na Muswada wa Rushwa. Nikakuta magari mengi sana na bahati mbaya siku ya Jumamosi sikulala mapema, nilala *late* sana. Nikashtuka nikadhani labda ni Jumatatu Bunge linaendelea. Nikakutana na Mheshimiwa Anthony Diallo pale nikamuuliza nini kinachoendelea hapa, Mheshimiwa Diallo akanionyesha bendera ya Rais. Kuiona nikasema Rais yuko hapa nini, akasema wanajadili taarifa ya

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Nikamwambia Mheshimiwa Diallo kazi mnayo. Nikaondoka nikaenda zangu kwenye Ofisi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimeanza na hilo ni kwamba inawezekana kabisa watu wakaona ni suala la kawaida kwa Rais kuzungumza na watendaji kuhusiana na taarifa ya Ofisa wa Serikali. Lakini kwa kweli siyo suala la kawaida, kwa sababu kitendo cha Rais kuondoka Dar es Salaam kuja Dodoma kuita Wakuu wa Mikoa, kuita Wakaguzi wa Ndani, kuita Ma-*RAS* na kuzungumza nao kuhusiana na suala la Hesabu za Serikali ni suala ambalo linahitaji pongeza ya hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais alikuwa na *option* nyingi sana, angeweza kujadili suala hili kwenye *cabinet* kama jinsi ambavyo labda Rais wa awamu iliyopita alikuwa anafanya. Angeweza kutoa *circular* kwa Wakuu wa Mikoa. Lakini alitaka watendaji hawa wa Serikali wamwangalie machoni na kumuona ni jinsi ambavyo yuko *serious,* jinsi gani ambavyo yuko *committed* na jinsi gani ambavyo hayuko tayari kuruhusu ubadhilifu ambao unaweza ukaendelea katika Serikali ambayo yeye anaiongoza. Kwa kweli kwa hili Rais anahitaji shime, Rais anahitaji kupewa hongera na Rais anahitaji kupewa nguvu zaidi ili kupata nishati zaidi kubwa zaidi ya kuweza kushughulikia masuala yetu mbalimbali ambayo yanaathiri nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, na mimi kwa dhati kabisa na kwa uzalendo wa hali ya juu napenda niungane na wenzangu ambao wametangulia kuzungumza kuunga mkono hoja ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua aliyoichukua. Kwa kweli taarifa ya mwaka huu imekuwa ni taarifa ambayo imeandikwa sana na vyombo vya habari, imekuwa *reported* sana na vyombo vya habari mbalimbali. Iwapo Rais angeichukua na kuikalia kimya, sidhani kama ingepata *coverage* jinsi ambavyo imepata *coverage. (Makofi)*

Kwa hiyo, kitendo na inawezekana labda taarifa nyingine zilikuwa na zile *magnitude* ya ubadhilifu labda ilikuwa ni kubwa zaidi kuliko ya sasa. Lakini kitendo cha Rais, kuichukulia na kuijali na kuifanyia kazi kimetoa uhuru kwa wananchi kuijadili ndiyo mpaka leo ukisoma magazeti unaona taarifa hii ikijadiliwa na wananchi mbalimbali ni kwa sababu juhudi hii ambayo ameifanya Rais ambayo kwa kweli nafarijika sana kuwa miongoni mwa watu ambao tunaungana mkono na hoja hii ya kumpongeza Mheshimiwa Rais na kumtaka aendelee hivi hivi, mwakani aende achukue hatua zaidi kwa sababu kila kitu kina hatua zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe Zitto. Msemaji wangu wa mwisho naye ni *Senator* mtu aliyekaa Bungeni kiasi cha miaka 40, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa heshima hii uliyonipa niweze kuchangia wasemaji waliotangulia wamesema maneno ya hekima na mazuri kweli. Lakini ningependa nianzie kwanza kupongeza hekima na heshima ya mwenzetu Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe kwa kufikiria kuleta hoja hii. Hongera sana. *(Makofi)*

La pili, nisingependa kupoteza muda lakini nataka niseme tu kwamba mimi nimewahi kuwa Mjumbe wa Kamati ya *PAC* mwaka 1972 mpaka 1973 na safari hii umenichagua katika Kamati. Safari hii mimi nilipokwenda kwenye ile Kamati nimemwambia Mwenyekiti naona kama hakuna kazi kwa sababu tunaweza tukawa tunajadili taarifa za miaka mitatu, minne iliyopita. Tulipokutana na *CAG* aliyeteuliwa mpya, Kamati ikasema hebu iokoe nchi, jitahidi kufanyakazi tupate taarifa zinazozungumzika na ameifanya hivyo, kwa hiyo, tunampongeza. *(Makofi)*

Pili, Serikali ilishaanza kutangaza hadharani namna fedha zinavyogawiwa. Nataka niende moja kwa moja kwenye faida ambazo zimepatikana kutokana na kitendo cha Rais. Ya kwanza taarifa ya fedha za wananchi ni taarifa ya wazi hadharani. Mwenyewe kitendo alichofanya amejenga imani kubwa sana kwa wananchi wa Tanzania. Maana ingekuwa amefanya ndani watu wasingejua na imepata nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, Kamati yetu ya *PAC* tuna nguvu mpya. Tumezaliwa upya na tunakushukuru kutuchagua, sasa tutafanyakazi kazi kwa bidii kweli kweli. Halafu vile vile heshima alikwishaanza kuijenga Rais wetu ndani na nje ya nchi inafanana na kazi hii aliyoifanya. Wanaotusaidia kutoa fedha, kutendo cha Rais kuvalia njuga jambo hili imekwishaongeza imani kwa wanaotupa misaada kutoka nje ya Tanzania. Baadhi yetu kwa sababu tuna marafiki wameanza kutupigia simu kutuambia kweli sasa tutaongeza misaada zaidi maana Rais wenu anaonyesha anajali kabisa matumizi ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo kingine kizuri ambacho kimetokana na hekima ya Rais ni kwamba wote wanaotumia fedha wameshikwa woga/ganzi, maana wameitwa wote. Makatibu, Wahasibu wote wameitwa na tuna taarifa kwamba tarehe 29 anakutana na Wakurugenzi wote nchi nzima ili wote walipate joto lile lile. Kwa hiyo, hii nayo itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, uwajibikaji. Mambo haya binadamu ni mzuri, lakini anaandaliwa kuwa mzuri. Binadamu huyo huyo anaweza kuwa ovyo, sasa watu kwa kawaida kwa kuwa huandaliwa kuwa wazuri, mimi nina hakika moyo huu ni nia ya kuandaa watu wafanye vizuri na nina hakika wale wote waliokwishafanya kosa watasamehewa katika utukufu wa mambo haya mapya ili wafanye vizuri zaidi kuliko kuendelea kufanya makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa kulisema hapa ni kuwa sisi Watanzania ni nchi changa, nchi inayoendelea. Tunahitajiwa kujali kila shilingi ya nchi inayotumika tujali. Napendekeza alivyosema Mheshimiwa Wilson Masilingi, ni sawa ila sisi Kamati yako katika taarifa tumekuletea tunapendekeza kwamba ndani ya Kanuni zenyewe za Bunge, Bunge lipate nafasi ndani ya Kanuni ya kujadili taarifa ya Mkaguzi wa Fedha za Serikali kwa siku tatu iwe ni Kanuni. Tumesema hivyo kwa sababu gani, Bunge hili litakaa miezi miwili kujadili Mapato na Matumizi, lakini tunapoletewa taarifa tunanyamaza kimya. Kwa hiyo, lazima tuzungumze vile vile kwa jasho kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa ni zamu ya mtoa hoja na bila shaka kazi yake ni nyepesi tu kwa sababu wote waliozungumza wameiunga mkono hoja hii ya Azimio la kumpongeza Rais. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella, umepewa dakika tatu.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kama mtoa hoja na kwa sababu tumezoea nidhamu ya Bunge la Afrika wanaozungumza wanazungumza dakika tano na wengine dakika moja, kwa hiyo, nitajitahidi kwa dakika ulizonipa. *(Makofi)*

Kwanza, niwatambue wale wote ambao wamechangia kwa mjadala ambao ni Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Joyce Masunga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nataka nisisitize jambo ambalo limejitokeza hapa kwanza. Kwanza nashukuru kuwa kidogo na woga ya kwamba ningewasilisha hoja hii halafu kila mtu akaiponda ningejisikia vibaya sana.

Lakini nadhani watu wametazama zaidi umuhimu wa hoja. Hoja hii msingi wake ni kwamba alichokifanya Rais, siyo kile *business as usual. You can have a business but this is not business as usual.* Amekwenda katika hatua ya kuwa muwazi na kuwaita wanaohusika na kutoa angalia. Ukita kumuua nyani usimwangalie usoni. Kwa hiyo, nina uhakika humo ndani kuna watu ambao wana aibu, lakini bado amejitolea kuzungumza nao. Kwa hiyo, katika pongezi hizi nakubali kwamba mdhibiti ametuwezesha kufika hapo tutampa pongezi wakati wa Bajeti na aendelee na kazi hiyo nzuri na mawazo mengi yaliyotolewa hapa ni mazuri ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi kwa makini. Natumaini yamezingatiwa hasa na Kamati zile zinazohusika na ukaguzi wa fedha za Serikali kuu na *Local Government* wakiongoza Kamati nyingine ambazo pia zinaangalia maeneo mbalimbali ya matumizi ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nimtakie tu Rais wetu maisha mema na aendelee na kazi nzuri ya kuwajali Watanzania na kujali fikra za Wabunge ambazo tumekuwa tukipiga kelele bila kufanikiwa. Sasa kwa kweli tunayo nguvu na tunaweza tukaifanyakazi hii kwa mshikamano wa karibu na hakuna atakayetumia nafasi ya Wabunge kutoa mawazo yao kama ni nafasi ya kupinga. Katika hoja hii Wapinzani wote na wana CCM wote tumejumuika pamoja kumpongeza Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu ni ya kupitisha Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa hatua yake ya kuita Serikali kujadili taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu, kwa hesabu zinazoishia Juni, 2006. Hoja hiyo imetolewa na Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafurahi kutangaza kwamba Azimio la kumpongeza Rais wetu kuhusu hatua yake la umakini kuzingatia Hesabu za Serikali limeungwa mkono na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante sana. *(Mkaofi)*

Waheshimiwa sasa ni saa 1.00 za jioni. Sielewi ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu atataka kusema nasi, lakini siwezi nikaachia ule uwezekano kwamba tutafika saa mbili kasoro robo bado awe anaongea. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Maswala ya Bunge Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, aweze kutoa hoja ya kutengua Kanuni ili kumwezesha mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu aendelee kidogo baada ya wakati hadi amalize hoja yake ya kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, hivi punde Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa hotuba yake ya Kuliahirisha Bunge. Hivyo basi Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liendelee na shughuli hadi hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapomaliza kusoma hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa imauliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu tutakapomaliza ndiyo itakuwa tumemaliza. Mheshimiwa Abdallah Sumry, ameniomba niwatambulishe kwa haraka wageni walioko hapa ambaye ni Mheshimiwa Askofu Eliudi Sanja wa *International Evangelist Church* na wenzake Wachungaji Maasa Ulomi Sylvester na Age, wale pale wamesimama pale. Karibuni sana na poleni sana kwa safari ndefu kutoka Mpanda. *(Makofi)*

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa hoja ya kuliahirisha Bunge, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutekeleza shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano wa Saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa Mjini Dodoma. Katika Mkutano huu, jumla ya maswali ya msingi 125 yameulizwa pamoja na maswali mengi mengine ya nyongeza na yakajibiwa na Serikali. Aidha, Miswada ya Sheria tisa imesomwa, kujadiliwa na kupitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Tunduru kwa kura nyingi kupitia Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi mdogo uliofanyika tarehe 18 Machi, 2007. Kuchaguliwa kwake kunadhihirisha imani kubwa waliyonayo wananchi wa Tunduru kwake na kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa salaam za pole kwa Mheshimiwa Harith Mwapachu, Waziri wa Usalama wa Raia na Balozi Juma

Mwapachu, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kufiwa na mama yao mzazi.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Profes Peter Msolla, Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na familia zao kwa misiba iliyowafika. Vile vile, natoa salaam za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha Dr. Aaron Chiduo, aliyewahi kuwa Mbunge na Waziri kwa nyakati mbalimbali katika Serikali za awamu zilizopita. Mwenyezi Mungu awape faraja na nguvu katika wakati huu mgumu.

Aidha, kwa masikitiko makubwa sana natoa salaam za rambirambi kwa wananchi, ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza ndugu zao katika ajali mbaya ya basi la abiria la Buffalo, iliyotokea Wilayani Mwanga tarehe 15 Aprili, 2007. Ajali hii imesababisha msiba mzito na hasara kubwa kwa Taifa letu. Nawaomba wananchi wote tushirikiane kuwaombea ndugu, jamaa na marafiki waliofikwa na msiba ili Mwenyezi Mungu awape nguvu za kuhimili msiba huo. Mwenyezi Mungu azilaze roho zote za marehemu mahali pema peponi, *Amin!*

Aidha, nawapa pole na kuwaombea majeruhi wote, Mwenyezi Mungu awasaidie waweze kupona haraka na kurejea katika shughuli zao za kila siku. Lakini ni vizuri tukachukua ajali hii kutafakari njia za kuzuia ajali za aina hii zinazoendelea kutokea mara kwa mara katika nchi yetu. Nimependezwa sana na Shirika la *SUMATRA* ambao wameanza kujadili jambo hili ili kupata muafaka wa hatua za kuchukuliwa katika masuala haya.

Mheshimiwa Spika, tunahitimisha mkutano huu leo baada ya kukamilisha kwa ufanisi mkubwa mijadala juu ya Miswada mbalimbali ya Sheria iliyowasilishwa na Serikali. Miswada ambayo imejadiliwa na kupitishwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2007 *(The Prevention and Combating of Corruption Bill, 2007);*

(ii) Muswada wa Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara wa mwaka 2007 *(The National Bank of Commerce (Re-organisation and Vesting of Assets and Liabilities) Bill, Cap. 404);*

(iii) Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa na Kutekeleza Masuala mbalimbali yanayohusu Mipango Miji wa mwaka 2007 *(The Urban Planning Bill, 2007);*

(iv) Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Usajili ya Mipango Miji wa mwaka 2007 *(The Town Planners (Registration) Bill, 2007);*

(v) Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa, Kuendesha na Kutekeleza Sheria ya Mipango ya Ardhi wa mwaka 2007 *(The Land Use Planning Bill, 2007);*

(vi) Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali ya mwaka 2007 *(The Supplementary Appropriation Bill, 2007);*

(vii) Muswada wa Sheria ya Kusimamia Huduma ya Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona wa mwaka 2007 (*The Optimetry Bill, 2007);*

(viii) Muswada wa Sheria ya Barabara wa mwaka 2007 *(The Roads Bill, 2007);* na mwisho;

(ix) Muswada wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji wa mwaka 2007 *(The Fire and Rescue Services Force Bill, 2007).*

Aidha, Bunge lako limepokea taarifa za Kamati zifuatazo:-

(a) Taarifa ya Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala;
(b) Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje;
(c) Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii;
(d) Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi; na
(e) Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Aidha muda mfupi uliopita Bunge lako Tukufu limepitisha Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na Homa ya Bonde la Ufa. Mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa *(RVF)* nchini bado ni tatizo. Ugonjwa huu umeonekana katika Wilaya 28 katika Mikoa ya Arusha, Manyara, Tanga, Kilimanjaro, Morogoro, Dodoma, Iringa, Singida na Mbeya. Takwimu zinaonyesha kuwa jumla ya ng'ombe 46,600, mbuzi 56,900 na kondoo 32,800 wameathirika na ugonjwa huu. Aidha, jumla ya ng'ombe 5,580, mbuzi 6,866 na kondoo 3,898 wamekufa. Takwimu pia zinaonyesha kuwa hadi kufikia tarehe 18 Aprili, 2007, kulikuwa na jumla ya wagonjwa 249 waliokuwa wamefikishwa hospitalini. Kati ya hao, 73 waliruhusiwa kutoka hospitali, 87 bado wamelazwa na 89 wamefariki. Mkoa wa Dodoma umeathirika sana na ugonjwa huu ambao hadi tarehe 18 Aprili, 2007, wagonjwa 144 walikuwa wamefikishwa hospitalini. Kati ya wagonjwa hawa, 33 waliruhusiwa kutoka hospitalini, 55 walikuwa bado wamelazwa na 56 wamefariki.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lililosababisha ugonjwa kuenea haraka ni wananchi walio wengi kutokuwa na ufahamu wa kutosha na kujua njia za kujikinga na wengine kudharau maelekezo wanayopewa na wataalamu kuhusu ugonjwa huu. Hali hii imesababisha vifo vingi na kuendelea kusambaa kwa ugonjwa katika baadhi ya maeneo nchini. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais katika hotuba yake kwa wananchi tarehe 31 Machi, 2007, alieleza hatua ambazo Serikali imechukua ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(a) Kuagiza dozi milioni mbili za chanjo. Hadi sasa tumepokea dozi 1,620,000 na zimesambazwa kwenye Wilaya 28 zenye maambukizi na Wilaya 9 zilizo kwenye hatari ya kuambukizwa ugonjwa huu. Jumla ya shilingi bilioni 1.7 zimetumika;

(b) Kuzuia kwa muda kufanyika kwa minada ya mifugo nchini kote;

(c) Kuimarisha utoaji wa chanjo za mifugo dhidi ya ugonjwa huu; na

(d) Kuandaa mpango wa dharura wa kudhibiti ugonjwa huu wa Bonde la Ufa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kudhibiti ugonjwa huu na changamoto tuliyonayo sote kama viongozi hasa wale wanaotoka katika maeneo yaliyoathirika ni kuendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu dalili, athari na njia za kujikinga na ugonjwa huu. Hivyo, naendelea kusisitiza kuwa elimu kuhusu ugonjwa huu itolewe kwa mapana zaidi ili wananchi waweze kuufahamu na kuepukana na athari zinazotokana nao. Napenda kusisitiza kuwa ugonjwa huu ni hatari na unauwa. Tusiufanyie mzaha. Hata wahenga walisema, mchezea mwiba mguu huota tende. Tuzingatie ushauri unaotolewa na wataalamu.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii pia kuwapongeza viongozi na watendaji wote ambao wanafanya kazi usiku na mchana katika juhudi za kupambana na ugonjwa huu. Aidha, niwashukuru kwa njia za kipekee kabisa madaktari na manesi wote katika mikoa iliyoathirika kwa kuwahudumia wagonjwa kikamilifu. Kazi hii ni nzito, lakini inalenga kuokoa maisha ya watu. Hili ndilo tunalolidhihirisha madaktari na wauguzi wetu. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishati mbadala, kwa kipindi chote cha mwaka jana nchi yetu ilikabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa umeme kutokana na ukame wa muda mrefu ambao ulisababisha kukauka kwa mabwawa ya kuzalisha umeme nchini. Tatizo hili na athari zake zimekuwa kubwa kutokana na sababu za kihistoria, ambapo nchi yetu ilitegemea kwa kiwango kikubwa nishati itokanayo na nguvu za maji kwa asilimia 90. Kitendo hiki cha kutegemea nishati ya aina moja ni sawa na kuweka mayai yote kwenye kapu moja! Kapu likipata msukosuko wa aina yoyote, mayai yote hupasuka. Wakati akiwahutubia wananchi kwa njia ya redio na televisheni tarehe 28 Februari, 2006 Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wetu kama Taifa wa kupunguza utegemezi wa umeme unaotokana na nguvu za maji. Ni hivi karibuni tu baada ya kuanza kutumia umeme unaozalishwa kwa gesi asili ndipo utegemezi wa umeme utokanao na nguvu za maji umepungua kutoka asilimia 90 na kufikia asilimia 63. *(Makofi)*

Lengo ni kupunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa nguvu za umeme wa maji na kuongeza uwezo wetu wa uzalishaji wa nishati mbadala na kuunganisha katika gridi ya Taifa ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka siku hadi siku. Aidha, pamoja na jitihada hizi, bado tunahitaji kuongeza juhudi za kupata umeme wa uhakika kutokana na vyanzo vingine vya nishati ambavyo tayari tunavyo. Serikali imeanza kuchukua hatua za kuendeleza nishati mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaliwa sana kuwa na vyanzo vingi vya nishati mbadala ambavyo vinajumuisha nishati jadidifu *(renewable energy)* na nishati zisizo jadidifu *(non-renewable energy).* Nishati zisizo jadidifu ni kama vile makaa ya mawe, gesi na mafuta ya petroli ambayo tunaendelea kufanyia utafiti. Miongoni mwa vyanzo vya aina nyingi za nishati jadidifu tulivyo navyo ni kama vile nguvu ya jua, upepo, maji, *volcano,* wanyama na mimea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna faida nyingi za kutumia nishati jadidifu ambayo ni rafiki wa mazingira. Tafiti mbalimbali zinazoendelea kufanywa hapa nchini zimethibitisha kwamba tuna fursa nyingi na kubwa ambazo zikiendelezwa zinaweza

kukuza matumizi ya nishati jadidifu kwa gharama nafuu. Miongoni mwa tafiti hizo ni zile zinazohusu uzalishaji wa mazao au mimea inayoweza kutumika kama *bio-fuels*. Mazao hayo ni kama vile miwa, michikichi, jatropha, alizeti, korosho, mbegu za pamba na ufuta na muhogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuelezea mifano michache ya nishati jadidifu tulizonazo:-

(i) Nishati itokanayo na miwa, tafiti zinaonyesha kuwa Tanzania ina uwezo wa kuzalisha zaidi ya megawati 200 za umeme utokanao na miwa kwa mwaka katika viwanda vya sukari vya Mtibwa, Kilombero, Kagera na *TPC*. Kwa mfano kiwanda cha sukari cha Mtibwa kina uwezo wa kuzalisha megawati 15 na hivi sasa kinazalisha megawati saba. Matarajio ni kuzalisha megawati tisa ifikapo Desemba, 2007. Kiwanda cha *TPC* pia kimewekeza kwenye mtambo utakaokuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 15 na kati ya hizo megawati 7 zinatarajiwa kuingizwa kwenye gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na fursa hii kubwa, Rais Jakaya Kikwete, hivi karibuni alipokuwa ziarani nchini Sweden alikutana na wawekezaji mbalimbali wa nchi hiyo ambao wameonyesha nia ya kuwekeza hapa nchini katika kilimo cha miwa. *(Makofi)*

Kampuni mojawapo ijulikanayo kama *Bio-Alcohol Fuel Foundation* (*BAFF*) tayari imeomba kupewa hekta 400,000 kwa ajili ya kilimo hicho. Uwekezaji huo pia utazalisha nishati nyingine (*Bio-alcohol*) ambayo itatumika kuendesha magari na mitambo mbalimbali. Hii ni fursa kubwa na ya kipekee kwa wakulima wetu kushiriki katika kilimo cha miwa kama *outgrowers* ili wanufaike na mradi huu. *(Makofi)*

(ii) Kilimo cha Michikichi, katika mkoa wa Kigoma, kuna Kampuni ya Watanzania inayojulikana kama *Farming for Energy in Southern Africa* (*FELISA*) ambayo inajihusisha na uendelezaji wa zao la Michikichi. Lengo la kampuni hiyo ni kuzalisha umeme wa kati ya megawati moja hadi 10 kwa kutumia mashudu ya michikichi. Pia wanatarajia kuzalisha *bio-diesel* kutokana na mafuta ya mawese kiasi cha tani 9,000 kwa mwaka. Ili kufikia lengo hilo, kampuni ina mpango wa kuendeleza eneo la hekta 5,000 la wakulima wadogo *(outgrowers)* wa zao la mchikichi ili wauze mazao yao kwenye kiwanda hicho. Hii tena ni fursa nyingine kwa wakulima wa mkoa wa Kigoma kujiongezea kipato, ajira, kupata umeme wa uhakika na wa gharama nafuu na kuzuia uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

(iii) Kilimo cha Jatropha au Mbono Kaburi ambacho hakina gharama kubwa za uzalishaji kimeonyesha kuwa na fursa kubwa ya kuzalisha mafuta yatakayotumika kuzalisha *bio-diesel*. Hivi sasa Jeshi la Kujenga Taifa linategemea kupanda jumla ya hekta 600 za Jatropha kwa lengo la kuzalisha mbegu zitakazosambazwa kwa wananchi ili kuzalisha zao hilo kuanzia msimu wa mwaka 2009/2010. Ili kuendeleza zao hili wataalamu kutoka Mikoa ya Tanga, Arusha, Mbeya, Pwani, Morogoro, Dodoma, Dar es Salaam na Ruvuma wamepata mafunzo ya kuwawezesha kulima kilimo bora cha Jatropha.

Aidha, baadhi ya asasi zisizo za kiserikali kama vile Kampuni ya Kijerumani *(PROCON)* yenye tawi Wilayani Mpanda tayari imeshirikisha wakulima zaidi ya 1,800

kuzalisha Jatropha kwa makubaliano kwamba watanunua mbegu za zao hilo. Pia Kampuni ya Kuendeleza Teknolojia (KAKUTE) ya Arusha inanunua mbegu za zao hilo kutoka kwa wakulima wa Kata ya Engaruka, Wilayani Monduli. Changamoto kubwa kwa viongozi ni kuhamasisha wananchi kuona umuhimu wa kulima zao la Jatropha. Hii ni neema kubwa. Tusisubiri zaidi. Tuanze kulima zao hilo kwa kujipatia maendeleo. *(Makofi)*

(vi) Nishati ya Mabaki ya Mazao ya Misitu, Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo huzalisha takriban megawati 40 kwa kutumia mabaki ya miti. Nishati hiyo hutumika kuendesha mitambo ya kutengeneza karatasi. Aidha, kiwanda cha Miwato cha Njombe *(TANWAT)* hivi sasa kinazalisha megawati 2.5 za umeme kutokana na kuchoma mabaki ya miti ya Miwato. Kiwanda hicho kina mpango wa kuzalisha kiasi cha megawati 15 za umeme na kuiuzia *TANESCO.* Utafiti unaonyesha kuwa kilo 2.4 za kuni za miwato zinaweza kuzalisha uniti moja *(1 kWh)* ya umeme. Ni dhahiri kuwa ipo fursa ya kuanzisha viwanda vingine vidogo vidogo nchini ambavyo vingeweza kutumia mabaki ya miti kuzalisha nishati mbadala kama viwanda vya Mgololo na *TANWAT*.

(v) *Biogas* ya taka za Mkonge, katika Mkoa wa Tanga, Bodi ya Mkonge Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa *(UNIDO)* wameanzisha mradi ambao unatarajiwa kuzalisha kilowati 150 kwa kutumia *biogas* itokanayo na taka za mkonge huo, kazi hiyo inafanyike kule Hale. Mafanikio ya mradi huu yatatumika kueneza teknolojia hii katika maeneo mengine yanayolima Mkonge nchini. Bodi ya Mkonge inakisia kuwa mashamba yote ya Mkonge nchini yakiendelezwa yana uwezo wa kuzalisha hadi megawati 400 za umeme.

Mheshimiwa Spika, kutokana na fursa zote hizi, sisi viongozi tunayo changamoto kubwa ya kuwaelimisha wananchi kuhusu manufaa ya kilimo cha mazao yanayozalisha nishati jadidifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nishati hizo nilizozielezea, ipo miradi mingine inayoendelea hapa nchini ya utafiti wa nishati itokanayo na jua, upepo, *volcano*, mifumo midogo ya nguvu za maji na *Biomass*. Matokeo ya awali ya tafiti hizo zinazofanywa ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu nishati ya upepo, utafiti umeonyesha kuwa kuna fursa kubwa ya kuzalisha nishati itokanayo na upepo katika Mkoa wa Singida na Wilaya za Njombe (Makambako). Utafiti umebainisha kwamba katika maeneo hayo, kasi ya upepo ni kubwa kiasi cha meta nane kwa sekunde kiwango ambacho ni kizuri kuzalisha umeme wa gharama nafuu. Maeneo mengine yenye upepo wa kasi ya wastani wa meta 4.5 kwa sekunde ni Mkumbara, Karatu na Same.

(b) Kwa nishati itokanayo na mionzi ya jua, utafiti umeonyesha kuwa Tanzania ina fursa kubwa za uzalishaji wa nishati hiyo kwa sababu ipo katika eneo linalopata jua kwa wingi *(solar belt).* Kwa mfano, hospitali za rufaa za Bugando na Mbeya zinatumia nishati hii kuchemsha maji. Aidha, majokofu zaidi ya 100 katika hospitali, vituo vya afya na zahanati yanaendeshwa kwa mionzi ya jua.

Vile vile, mashirika ya *TAZARA, TRC,* Simu, Bandari, *TAZAMA* na kampuni ya uegeshaji magari jijini Dar es Salaam yanatumia vifaa vinavyoendeshwa kwa nishati hii.

Asasi zisizo za kiserikali na watu binafsi wanaotumia nishati hii kuwashia taa na kuendesha mashine za kusukuma maji. Kutokana na uzoefu huo, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi na watu binafsi kukuza matumizi ya nishati ya mionzi ya jua nchini na hasa vijijini.

Kwa upande wa nishati itokanayo na mifumo midogo ya nguvu za maji, utafiti umebainisha kwamba upo uwezekano wa kuzalisha zaidi ya megawati 300 za umeme utokanao na maporomoko madogo madogo yaliyopo nchini. Imebainika kuwa fursa za aina hiyo zipo katika mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Kigoma na Kagera. Hadi sasa kiwango cha uzalishaji kilichofikiwa ni megawati nne kutokana na chanzo hicho katika maeneo ya Muleba na Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziko nchi nyingi duniani ambazo zinashughulika na mambo hayo, uzoefu wa nchi mbalimbali duniani umeonyesha kwamba nchi hizi ziliwekwa kwa makusudi, taratibu muafaka zilizowezesha ukuaji wa kasi ya uzalishaji na matumizi ya umeme utokanao na nishati jadidifu. Kwa mfano, nchi ya Sweden imeweka lengo kwamba ifikapo mwaka 2020 itaongeza matumizi ya *biofuels* hivyo kuweza kupunguza matumizi ya mafuta ya petroli kwa asilimia 50 ya kiwango cha sasa. Hivi sasa Sweden inatumia asilimia 20 ya mahitaji ya mafuta ya magari na mitambo kutokana na *bio fuels*.

Kwa upande mwingine, nchi ya Ujerumani inazalisha megawati 18,400 za umeme kutokana na nguvu za upepo na megawati 758 kutokana na nishati ya mionzi ya jua. Katika Bara la Afrika, nchi inayoongoza kwa uzalishaji wa nishati ya upepo ni Misri inayozalisha megawati 150 ikifuatiwa na Morocco megawati 60. Aidha, utafiti uliofanywa kuhusu umeme utokanao na nishati ya *volcano* katika nchi za Afrika zinazounganishwa na Bonde la Ufa, umeonyesha kwamba nchi hizo zina uwezo wa kuzalisha nishati kama ifuatavyo:-

Kenya ina uwezo wa kuzalisha *(MW 2,000),* Ethiopia *(MW 1,000),* Djibouti *(MW 230-860),* Uganda *(MW 450)* na Tanzania *(MW 150).* Hivi sasa Kenya inazalisha megawati 127 kutokana na nishati hiyo.

Mifano ni mingi kuhusu uzoefu wa nchi nyingine kama vile Brazil, Sweden, India, Marekani, Mauritius, Thailand na Ghana ambazo zinatekeleza miradi mbalimbali inayolenga kukuza matumizi ya nishati jadidifu kwa gharama nafuu. Kwa nini nasema haya, napendekeza nini tufanye.

Mheshimiwa Spika**,** kutokana na mifano hiyo na uzoefu wetu mdogo wa ndani, ni dhahiri kwamba tunaweza kukuza uzalishaji wa matumizi ya nishati jadidifu. Kwa misingi hiyo ili na sisi tufanikiwe katika uzalishaji wa nishati hiyo inatulazimu kufanya yafuatayo:-

(a) Kuweka miundombinu muafaka na kuandaa sheria itakayoruhusu wazalishaji wa nishati jadidifu kuingizwa katika gridi ya Taifa. Sheria hii ndiyo iliyoiwezesha nchi ya Ujerumani kupiga hatua katika matumizi ya nishati ya jua na upepo. *(Makofi)*

(b) Kuwekeza na kuimarisha utafiti ili kuwezesha wataalamu kubuni vyanzo mbalimbali vya nishati zinazoweza kutumika kwa bei nafuu kwa wananchi walio wengi;

(c) Kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji; na

(d) Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi na ushirikiano wa Kimataifa katika kubuni, kutafiti na kuendeleza nishati za aina hii hiyo.

Mheshimiwa Spika, Rais wa zamani wa Marekani Richard Nixon aliwahi kusema, na mimi nanukuu: *"Never let your head hang down. Never give up and sit down and grieve. Find another way. And don't pray when it rains if you don't pray when the sun shines."* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine tukipata tatizo tusijikunyate bali tutafute njia mbadala za kulitatua. Nishati jadidifu ni njia mbadala ya kukabiliana na mahitaji ya umeme katika miaka ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nategemea Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na wadau wengine watatayarisha na kuwasilisha Serikalini sera na programu maalumu ya kukuza na kuendeleza uzalishaji na matumizi ya nishati mbadala kwa kutumia uzoefu wa nchi nyingine. Zoezi hili likamilishwe na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu kabla ya mwezi Septemba, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha huduma za afya nchini. Hata hivyo jitihada zaidi zinahitajika kusogeza huduma hizo karibu zaidi na wananchi na hasa vijijini. Takwimu zinaonyesha kuwa hadi sasa tunazo hospitali 219, vituo vya afya 481 na zahanati 4,679. Kutokana na takwimu hizi ni dhahiri kwamba tunahitaji kuongeza idadi ya hospitali, vituo vya afya na zahanati ili kutimiza malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 na yale ya milenia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ni kuendelea kuzipatia wataalamu na vifaa vya kisasa hospitali, vituo vya afya na zahanati za Serikali. Aidha, malengo matatu ya milenia (4, 5 na la 6) yanaelekeza nguvu zake kwenye masuala ya afya. Malengo haya yanaelezea kupunguza vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kwa theluthi mbili, kupunguza vifo vya mama wajawazito kwa asilimia 75 na kupunguza maambukizi ya UKIMWI, Malaria pamoja na magonjwa mengine makubwa ifikapo mwaka 2015.

Wakati akifungua rasmi Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 30 Desemba 2005, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alisema; nanukuu: "…Serikali ya Awamu ya Tatu imechukua hatua mbalimbali kuboresha sekta ya afya kwa lengo la kuinua kiwango cha ubora wa huduma za afya, kuzisogeza karibu na wananchi na kuongeza uwajibikaji wa watumishi wa sekta hii. Tutaendeleza hatua hizo…, tutaendelea kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali zaidi mijini na vijijini…." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika**,** ili kujenga hospitali, vituo vya afya na zahanati kwa kasi mpya, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, amewaagiza viongozi wa Mikoa na Wilaya waishirikishe jamii ili waweze kuiunga mkono Serikali katika kukabiliana na ugonjwa wa malaria, kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto, kuongeza idadi ya vituo vya afya na zahanati na kukabiliana na ugonjwa wa kifua kikuu. Mheshimiwa Rais ameelekeza kuwa kama tulivyotoa msukumo katika elimu ya msingi

na sekondari, kuanzia mwezi Julai, 2007 tuanze ujenzi wa zahanati kwa kila kijiji na vituo vya afya kwa kila kata. *(Makofi)*

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wakishirikiana na wadau wengine wameagizwa kuandaa mpango na mkakati maalumu wa utekelezaji wa agizo hilo, ikiwa ni pamoja na suala la upatikanaji wa wataalamu wa afya. Napenda kutoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya na viongozi wa ngazi za tarafa, kata na vijiji wawahamasishe wananchi katika kuchangia ujenzi wa zahanati na vituo vya afya. Tuwashirikishe kuanza mbinu mpya ya kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ipo methali isemayo mwezi hauwezi kuandama mpaka uliotangulia umeondoka, nasi hatuwezi kupata maisha bora kama bado tutaendelea na taratibu za kung'ang'ania hulka na mienendo ya kufanya kazi kizamani. Tukiwa wabunifu zaidi, tukijituma zaidi na tukifanya mambo yetu kisasa zaidi tutaweza kupata maisha bora zaidi. Mimi ninaamini kwamba tukiamua tunaweza na tutafanikiwa na hata wahenga walisema penye nia pana njia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchangiaji wa elimu ya juu, alipokutana na baadhi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mheshimiwa Rais aliahidi kushughulikia suala la uwezo wa wanafunzi wa vyuo vikuu kuchangia asilimia 40. Alieleza kuwa anatambua hata kwa asilimia hiyo 40 wapo wanafunzi ambao hawataweza kumudu. Aidha, aliahidi kwamba hakuna mwanafunzi hata mmoja atakayekosa elimu kutokana tu na kukosa fedha hizo. *(Makofi)*

Tangu Mheshimiwa Rais atoe ahadi hiyo Serikali imekuwa inalifanyia kazi suala hili kwa kuzingatia hali ya sasa ya mwaka wa fedha wa Serikali na vile vile mpango na Bajeti wa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema na ahadi ya Mheshimiwa Rais, wanafunzi wa baadhi ya vyuo vikuu wameamua kutokuwa na subira na hivyo kugoma. Tulitegemea wanafunzi hawa wangekuwa na subira ya kuzingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo ana nia ya kuitekeleza. *(Makofi)*

Hata hivyo, kutokana na hali zilizojitokeza za kuashiria vurugu katika vyuo hivyo, uongozi wa Vyuo Vikuu uliamua kuvifunga kwa muda ili kuepusha vurugu zaidi. Serikali inaunga mkono hatua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana uongozi wa Vyuo Vikuu umejitahidi sana kutoa maelezo kwa uongozi wa wanafunzi ili wawe na subira bila mafanikio. Uongozi huo ulichukua hatua za kulegeza masharti ya ulipaji wa asilimia hiyo 40 ili kuwawezesha wanafunzi kuendelea na masomo, kujadiliana na wanafunzi kuona jinsi ya kupunguza gharama ya mafunzo kwa vitendo kwa kuwapanga katika maeneo ambayo siyo mbali sana. Kuhusu uchangiaji wa matibabu ambazo ni shilingi 100,000/= kwa kila mwanafunzi, chuo kilikubali kusitisha uchangiaji wa fedha hizo hadi hapo baadae. Hivi sasa uongozi wa vyuo unachukua hatua za haraka za kurejesha hali ya kawaida kwenye vyuo.

Napenda kutumia fursa hii kukariri ahadi na dhamira ya Mheshimiwa Rais kuwa pamoja na haya yaliyotokea, nia ya Serikali ni kuwawezesha wanafunzi wengi kadiri

iwezekanavyo kupata elimu ya juu kwa gharama nafuu sana kwao na ambayo wanaweza kuimudu. Tukifika mahali uchumi wetu unaotuwezesha kutoa elimu hiyo ya Chuo Kikuu bure tutafanya hivyo!*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niongeze, wapo watu wanasema Serikali haina mapenzi na wanafunzi, hii ni Serikali moja ambayo inawajali sana na inajali elimu ya vijana wake. Hii ni Serikali ambayo tunahangaika nchi nzima kuongeza shule kwa ajii ya wanafunzi wetu.Hii ni Serikali ambayo tunahangaika kujenga vyuo vikuu vingi nchini kwa ajili ya watoto wetu, tutaendela na tungependa kuwashauri wanataka kutushinikiza wasipoteze muda wao, tupo na tunaendelea kufanya yale ambayo yanapaswa. Lakini vile vile tutaachia uongozi wa vyuo vikuu ufanye kazi kwa mujibu wa sheria bila kuingiliwa na mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhamishaji mifugo, IHEFU, mwezi Aprili, 2006, Serikali ilitoa tamko kuhusu hatua za haraka za kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji nchini. Pamoja na mambo mengine, tamko hili lilitaka wafugaji na wakulima waliovamia bonde la Usangu hususan maeneo ya ardhi oevu ya Ihefu waondolewe. Kutokana na agizo hili ilikadiriwa kuwa takribani ng'ombe 235,000 walitakiwa waondolewe katika eneo hili na kuhamia maeneo yenye nafasi ya kutosha. Pia, Serikali ilipiga marufuku uingizaji wa mifugo nchini toka nchi jirani kwa ajili ya malisho na maji na pia kuzuia uhamishaji wa mifugo kiholela nchini kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa maelekezo na mikakati endelevu mbalimbali kwa viongozi na wananchi jinsi ya kufanikisha zoezi hilo. Napenda kurejea kwa kifupi baadhi ya maelekezo hayo.

(1) Utaratibu wa kuhamisha mifugo katika maeneo yote nchini uzingatie Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 2002 na Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya mwaka 2003 zinazozuia kuhamisha mifugo kiholela kutoka eneo moja hadi jingine pasipo kufuata taratibu kikamilifu;

(2) Wakuu wa Mikoa na Wilaya na viongozi katika ngazi mbalimbali za Serikali wasimamie kikamilifu utaratibu wa kuhamisha wafugaji na mifugo yao;

(3) Uhakiki wa uwezo wa maeneo ya mifugo ufanyike katika maeneo mbalimbali nchini ili baada ya zoezi hilo wafugaji wahame kwa utaratibu unaokubalika na ulio endelevu;

(4) Hatua za dharura na za dhati zichukuliwe na viongozi wa Wilaya za kuwatengea wafugaji maeneo hasa walio katika maeneo ambayo uwezekano wa kuzuka migogoro kati ya wafugaji na wakulima ni mkubwa;

(5) Viongozi wa mikoa husika wahakikishe kuwa maeneo yanayopelekwa wafugaji yanapimwa na kujengewa miundombinu pamoja na uwezekano wa kupatikana kwa madawa ya mifugo;

(6) Uongozi wa Mkoa wa Mbeya uchukue hatua za dharura kutenga maeneo yaliyo mbali na vyanzo vya maji na hifadhi ya misitu kwa ajili ya mifugo iliyoko katika

vijiji vya jirani na Ihefu, wakati Serikali Kuu ikitafuta ufumbuzi wa kudumu kuhusu tatizo hili;

(7) Njia za kupitisha mifugo zifufuliwe;

(8) Elimu itolewe kwa wafugaji juu ya athari za kuwa na mifugo mingi na faida ya kuwa na idadi ndogo ya mifugo yenye tija; na

(9) Kila Halmashauri ipange matumizi mazuri ya ardhi *(Land use Master Plan)* kwa sekta mbalimbali, kama vile makazi, mifugo, kilimo, viwanda, hifadhi, miundombinu, huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, pia yalitolewa maelekezo kwa Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Katiba na Sheria; Usalama wa Raia; Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa, kushirikiana na uongozi wa Mikoa na Wilaya kuandaa programu ya utekelezaji wa mapendekezo hayo ili kuwezesha wafugaji kutulia na kuendeleza mifugo kwa manufaa yao na kwa Taifa kwa jumla.

Takwimu zinaonyesha kuwa zoezi hili limefanikisha uhamishaji wa jumla ya mifugo 303,354 kutoka Wilaya ya Mbarali kwenda Mikoa ya Lindi ambako wamekwisha kuwa na ng'ombe 130,737, Pwani 72,517 na Mbeya-Chunya bado wako 100,000. Pamoja na uamuzi huu mzuri na dhamira njema ya Serikali iliyoambatana na maelekezo sahihi, yamejitokeza malalamiko mbalimbali kutoka kwa wafugaji waliohamishwa.

Kutokana na hali hii, Serikali imeamua kuunda Tume ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa zoezi zima la kuhamisha mifugo kwa lengo la kuainisha mafanikio na mapungufu yaliyojitokeza na kuishauri Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume hiyo itaongozwa na Mheshimiwa Jaji Othman Chande**.** Wajumbe wengine wa Tume ni Bwana Stephen Mashishanga, Mheshimiwa Dr.Christant Mzindakaya, Mheshimiwa Esterina Kilasi, Mheshimiwa Yonas Assechek, jina hili kama la kizungu, lah ni mwana wa Kibaragaig aliyeko kule Helda chini Mbulu, Bwana Wilson Mukama, Profesa Rudovick Kazwala, Bwana Reuben Ole Kuney na Bwana Maulid O. Mvungi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekretarieti ya Tume hii itakuwa ni Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Katiba na Sheria. Tume inatakiwa kuanza kazi mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wilaya na viongozi na wananchi wote kwa ujumla waipe ushirikiano thabiti Tume hii ambayo imeundwa ili iweze kufanya kazi zake vizuri na kuiwezesha kutoa tathmini sahihi ya utekelezaji wa zoezi zima la kuhamisha mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Vyombo vya Usafiri, yamekuwepo malalamiko mengi kuhusu kuzuiwa kwa pikipiki ikiwa ni pamoja na *Bajaj* na baiskeli kutumika kwa biashara ya usafirishaji wa abiria na mizigo. Malalamiko hayo yametokana na ukweli kuwa katika baadhi ya miji na vijiji kuna tatizo kubwa la usafiri ambapo usafiri wa pikipiki pamoja na *Bajaj* na baiskeli ndiyo usafiri pekee na wa nafuu unaotegemewa na wananchi walio wengi. *(Makofi)*

Hata hivyo, sheria zinazotumika kuratibu na kuongoza matumizi ya vyombo vya usafiri yakiwemo magari, pikipiki, baiskeli na kadhalika haziruhusu pikipiki, *Bajaj* na baiskeli kutumika kibiashara kusafirisha abiria. Sheria hizo ni Sheria Na. 30 ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973, Sheria ya Bima za Magari ya mwaka 2002 na Sheria Na. 1 ya Leseni za Usafirishaji ya mwaka 1973 pamoja na kanuni zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria hizo hata hivyo hazizuii pikipiki au baiskeli kubeba mtu asiyezidi mmoja kwa safari binafsi. Lakini, kwa kuwa suala hili limeleta malalamiko mengi kutoka kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge wao kutaka sheria hizo zifanyiwe marekebisho, Wizara za Usalama wa Raia, Fedha na Miundombinu wataleta sheria kwa ajili ya kuzibadilisha katika Bunge la mwezi wa kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu safari za Mheshimiwa Rais nje ya nchi, katika mkutano huu yametolewa maelezo ndani ya Bunge lako Tukufu kuhoji safari za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nje ya nchi. Napenda kutoa ufafanuzi ufuatao wenye lengo la kueleza umuhimu wa ziara za Mheshimiwa Rais nje ya nchi kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa kufahamisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kuwa ziara anazofanya Mheshimiwa Rais nje ya nchi ni za kikazi na zenye malengo maalum. Matokeo ya ziara hizo yameanza kuonekana yakiwa na faida kubwa kwa nchi yetu. Naomba nitoe mifano michache. *(Makofi)*

(a) Mwezi Septemba 2006, Mheshimiwa Rais alitembelea nchi ya Marekani. Akiwa nchini Marekani, Mheshimiwa Rais alifanya mazungumzo na Rais wa Marekani na kutokana na mazungumzo hayo, Rais wetu ameahidiwa kupata msaada kutoka *Millenium Challenge Corporation*. Tanzania itanufaika kwa kupatiwa msaada wa jumla ya fedha ya dola za Kimarekani milioni 800 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maendeleo. Msaada huu umeweka rikodi miongoni mwa nchi za Afrika ambapo awali nchi iliyokuwa ikipata fedha nyingi kutoka Marekani ni Ghana ambayo imepata dola za Kimarekani milioni 500, tukipata zetu sisi tutakuwa tunaongoza; *(Makofi)*

(b) Mwezi Februari 2007, Mheshimiwa Rais, alipofanya ziara ya kikazi nchini Uingereza, ujumbe wake ulikutana na wawekezaji wakubwa wa Uingereza kuzungumzia mipango ya maendeleo kwa nchi ya Tanzania. Pia, ulifanya mazungumzo na Waziri Mkuu wa Uingereza Bwana Tony Blair. Kufuatia mazungumzo hayo, Serikali ya Uingereza imetoa jumla ya paundi milioni 105 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo nchini; *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Rais alipotembelea Jamhuri ya Muungano wa Nchi za Kiarabu mwezi Mei, 2006 alifanya mazungumzo na viongozi wa Abu Dhabi, Dubai na Ras Al Khaimah. Matokeo ya mazungumzo hayo yamejenga mahusiano mazuri sana ambapo Abu Dhabi itasaidia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na ujenzi wa barabara kuanzia Manyoni, Tabora mpaka Kigoma. Dubai wameahidi kuwekeza katika ujenzi wa Bandari ya Mbegani na kuboresha utendaji wa kazi katika Bandari ya Dar es Salaam. Ras Al Khaimah wameahidi kuwekeza katika nishati ya mafuta na *ceramics.* Wataalamu wao tayari wameanza kazi nchini kutafuta mafuta katika ukanda wa bahari; *(Makofi)*

Aidha, Mtawala wa Dubai aliahidi kusaidia Jeshi la Polisi magari 40 na pikipiki 177. Hadi sasa tumepokea magari 38 na pikipiki 22. Utaratibu wa kuletwa kwa magari mawili yaliyobaki pamoja na pikipiki 155 unakamilishwa.

(d) Mheshimiwa Rais alipotembelea nchi za China, Korea na Japan mwezi Novemba 2006, yafuatayo yalijitokeza, China imekubali kuongeza uzalishaji wa nishati ya umeme kwa kutumia makaa ya mawe huko Kiwira kutoka megawati 6 hadi megawati 200.

Sambamba na azma hiyo, nchi yetu imetakiwa kupeleka orodha ya miradi itakayofadhiliwa kwa mpango wa *Forum of China - Africa Cooperation (FOCAC)* ambayo ni ya kilimo, teknolojia ya mawasiliano, mradi wa kuboresha reli ya *TAZARA* na miradi ya kusomesha Watanzania katika lengo la kutujengea uwezo zaidi. Japan imekubali kusaidia ujenzi wa barabara kutoka Masasi mpaka Mangaka kwa kiwango cha lami.

Pia, Kampuni ya *Oji Paper* ya Japan imeanza kupanda miti ya mikaratusi kwa majaribio ili kutengeneza karatasi. Jamhuri ya Korea imekubali kusaidia ujenzi wa Daraja la Mto Malagarasi na imeahidi kutoa dola za Kimarekani milioni 25 katika mwaka wa fedha 2007/2008; *(Makofi)*

(e) Katika ziara aliyofanya Mheshimiwa Rais nchi za Scandinavia, Sweden mwezi Februari, 2007 Sweden iliahidi kuanzisha mashamba ya miwa nchini kwa ajili ya kutengeneza *ethanol* kama nishati mbadala. Vile vile, imeahidi kuboresha bandari ya Kilwa iwe *Deep Sea Port. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa ziara za Mheshimiwa Rais zimeiletea nchi yetu faida kubwa katika kuimarisha uhusiano wetu na nchi husika na pia kuongeza uwekezaji hapa nchini. Hivyo, gharama zilizotumika katika ziara za Mheshimiwa Rais nje ya nchi zilinganishwe na malengo pamoja na matokeo yaliyopatikana. Kutokana na ziara za Mheshimiwa Rais, hivi sasa nchi yetu inaheshimika na kutambulika kama nchi inayofanya vizuri katika mageuzi ya kisiasa na kiuchumi. Isitoshe, hivi karibuni Taifa letu limepata nishani ya Uwekezaji Bora katika Bara la Afrika na pia kupata Hati ya kuwa Mwanamageuzi Bora *(Good Reformers Club Certificate in Africa).* Ziara za Rais zimetutoa kwenye ule utaratibu wa nchi za Afrika wa kujulikana kwenye vyombo vya habari vya nje pale tu panapokuwa na maafa au vita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha hoja yangu, napenda kuweka msisitizo katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

(i) Tuanze kufikiria suala la kutumia nishati mbadala, ndivyo dunia nzima inavyofanya sasa. Tunayo fursa ya kutumia mimea ambayo huzalishwa kwa gharama nafuu. Tuhimize wananchi kuanza kulima mazao hayo ili kujiletea maendeleo. Aidha, sekta binafsi ni muhimu ikatoa mchango wake katika tafiti zinazoendelea kote nchini kwa ajili ya kupata na kutumia nishati mbadala;

(ii) Tuongeze nguvu na juhudi katika ujenzi wa vituo vya afya kwa kila kata na zahanati kwa kila kijiji ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kukamilisha shughuli zilizopangwa katika Mkutano huu wa Saba, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kutuongoza vizuri sana. Tulipokuwa tunakuja Dodoma kabla ya kufika hapa magazeti yalisema maneno mengi sana ungedhani Dodoma kungetokea mambo makubwa ya ajabu, lakini kwa busara zako mambo yamekwenda shwari tuko salama salmini. Aidha, namshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge hili Tukufu kwa kutusimamia vizuri. Namshukuru pia Katibu wa Bunge, Bwana Damian Foka na wataalamu wake kwa kazi nzuri ambayo imetuwezesha kufanya shughuli zetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza mwaka 1905-1908, Bwana Campbell Bannerman alikuwa anapenda sana miti. Siku moja alitembelewa na mgeni. Yule mgeni akagundua kuwa kila asubuhi Bwana Campbell alikuwa akipita kwenye bustani yake ya miti na kila alipofika katika miti ambayo alikuwa akiipenda sana alikuwa akiinama kwa heshima na kuisalimu, Habari za Asubuhi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia wito wangu kwa kila mmoja wetu kama Wabunge tuwatembelee wananchi, tuwasalimu na tujue matatizo yao. Tuwasaidie kutatua kero zao tunapokuwa nao katika maeneo yetu ya kazi. Aidha, tuwashirikishe kupenda kujiletea maendeleo. Nawatakieni nyote safari njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 12 Juni, 2007 saa 3.00 asubuhi litakapokutana hapa Dodoma. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bila shaka mtaungana nami kumpongeza Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kwa hoja hiyo ya Kuahirisha Bunge ambayo imetoa ufafanuzi uliopevuka kuhusu mambo mengi tuliyokuwa tunataka kuyafahamu.

Sasa kabla sijawahoji, kuhusu hoja hiyo, nilitaka kukumbusha tu kwamba kesho saa nne katika ukumbi wa Pius Msekwa tutakuwa na Tume ya Kukusanya Maoni ya Mchakato Kuharakisha Shirikisho la Afrika Mashariki, Mkutano huo utakuwa ni saa nne kamili asubuhi unaanza, tunaomba tutunze muda. Kesho kutwa siku ya Jumapili tutapokea taarifa za viongozi wa misafara ya Waheshimiwa Wabunge waliokwenda nchi za nje, saa tano asubuhi katika ukumbi huo huo. Matukio yote mawili yamesimamiwa kikamilifu kwa kuzingatia haki za Wabunge. *(Makofi)*

Siku ya Jumatatu tarehe 23 Aprili, 2007, saa nne asubuhi, tutakuwa na mkutano wa kutoa ushauri kuhusu Mchakato wa Bajeti ya mwaka 2007/2008, mkutano huo unaweza ukamilizika siku hiyo ya Jumatatu au unaweza ukaendelea siku ya Jumanne. Lakini tutaona, ila tutaanza siku hiyo, huo nao ni kama mkutano wa kawaida, kwa hiyo, umehudumiwa kwa kila hali. Niseme tu kwamba kwa ile ya kwanza ule wa maoni ya Afrika Mashariki na taarifa za ziara tutafanyia ukumbi wa Pius Msekwa. Lakini kupokea taarifa za Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na pengine na Waziri wa Fedha na sisi kuchangia kuhusu Bajeti ijayo tutafanyia katika ukumbi huu. *(Makofi)*

Baada ya hayo sasa napenda kusema kwamba Bunge…, nimesahau hata kuwahoji, sasa Waheshimiwa Wabunge naahirisha Bunge hadi siku ya Jumanne, tarehe 12 Juni saa Tatu asubuhi hapa Dodoma.

*(Hoja iliolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 01:54 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 12 Juni, 2007 saa tatu asubuhi)*